EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA METHALI ZA KIKUYU

NA

CHOMBA ESTHER NJOKI

Tasnifu hii Imewasilishwa kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili (M.A) Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Egerton

Oktoba 2005

Eger241187

2008/76028

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote .

CHOMBA E. N SAHIHI TAREHE 26/10/05

IDHINI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii .

DKT. ONYANGO J. SAHIHI TAREHE 26/10/

DKT. BEJA K. SAHIHI TAREHE 26/10/0

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia kakangu Peter Mwaniki Nga'ng'a.

Laiti Maulana angekujalia siku zaidi ili upate kushuhudia ukamilifu wa ndoto uliyosaidia kuagua. Rabana akuangazie mwanga wa milele.

SHUKRANI

Kwanza ningependa kutoa shukrani zangu kwa Maulana aliyenikirimia kila aina ya baraka.

Pia, natoa shukurani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu katika kazi hii Dkt. Karisa Beja na Dkt. James Ogolla Onyango, ambao walinionyesha jinsi ya kushika makasia na kunifunza katiba ya unahodha katika bahari ya usomi na utafiti. Bila usaidizi wenu kazi hii haingekamilika.

Namshukuru mkuu wa idara ya Lugha na Isimu Dkt. Kitetu pamoja na Dkt. Furaha walionipa mkongojo nilipotetereka, maelekezo yenu yalikuwa dira maasumu ya kuniongoza katika bahari tesi hii ya usomi.

Nawashukuru sana wahadhiri wa Idara ya Lugha na Isimu, hasa Bw. Chacha, Bw. Gwachi, Bw. Siteti na Bi. Juma. Mashauri yenu yalikuwa mlizamu wa kunawirisha kazi hii.

Namshukuru mume wangu Michael Chomba ambaye mbali na kuwatunza watoto wetu nilipokuwa nasoma, alinitia shime na kunishajiisha ari yangu ilipofifia. Asanteni pia wanangu Brian, Bernadette na Clarence. Uvumilivu wenu ulinipa ghera na ilhamu ya kukamilisha kazi hii.

Nawashukuru wahojiwa wangu wote. Hoja zenu zilikuwa amana muhimu kwa utafiti huu. Nawashukuru sana wanafunzi tulioabiri pamoja katika dau la masomo, Roseline Ogolla, Ndugu Kirobi, Raphael Gacheiya na Daniel Muthigwa. Mijadala tuliyokuwa nayo ilinifaa sana katika utafiti huu.

Mwisho nawashukuru wote walionikongolea chembe ya hali na mali wakati wa uhitaji.

FAHARASA

UNGAMO.....I

TABARUKU II
SHUKRANI.....III
FAHARASA IV

JEDWALI.....VII
ABSTRACT.....VIII

IKISIRI.....IX

SURA YA KWANZA.....1

1.0 UTANGULIZI.....1

1.1 Usuli wa mada.....1

1.2 Mada ya utafiti.....2

1.3 Madhumuni ya utafiti.....2

1.4 Nadharia tete.....2

1.5 Umuhimu wa utafiti.....2

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti.....3

1.7 Maelezo ya istilahi.....3

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA MACHAPISHO.....5

2.1 Utangulizi.....5

2.2 Asili ya tofauti kati ya wake na waume.....5

2.3 Taswira ya mwanamke.....6

2.4 Maandishi kuhusu methali.....11

2.5 Msingi wa nadharia.....12

SURA YA TATU.....16

3.0 MBINU ZA UTAFITI.....16

3.1 Utangulizi.....15

3.2 Uteuzi wa sampuli na ukusanyaji data.....16

3.3 Uchanganuzi wa data.....18

3.4 Hitimisho.....19

SURA YA NNE

4.0 JAMII YA WAKIKUYU.....20

4.1 Utangulizi.....20

4.2 Asili ya Wakikuyu.....21

4.3 Idhibati za kihistoria.....23

4.4 Hali ya kiuchumi.....24

4.5 Hali ya kisiasa.....27

4.6 Hali ya kijamii.....29

4.6.1. Ada za kuzaliwa.....30

4.6.2. Ada za tohara..... 33

4.6.3 Ada za ndoa.....40

4.6.4 Uzee na kifo.....46

SURA YA TANO

5.0 TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA METHALI.....50

5.1 Utangulizi.....50

5.2 Methali kuhusu ndoa.....52

5.3 Methali kuhusu malezi.....72

5.4 Methali kuhusu kazi.....79

5.5 Methali kuhusu utawala.....89

5.6 Methali kuhusu umilikaji mali.....96

5.7 Muhtasari wa matokeo ya uchanganuzi.....102

SURA YA SITA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....107

6.1. Utangulizi.....107

6.2 Hitimisho.....107

6.3 Matatizo 108

6.4 Mapendekezo.....108

MAREJELEO.....109

WAHOJIWA.....113

VIAMBATISHO

I Mwongozo wa maswali.....115

II Orodha ya methali.....117

ORODHA YA MAJEDWALI

5.7.1.1 Msambao wa nyanja mbalimbali zilizotafitiwa.....103

5.7.5.1 Jedwali linaloonyesha hadhi kwa mujibu wa methali.....105

ABSTRACT

This study analyzed the image of a woman as depicted by the Kikuyu proverbs. The main objective of the study was to establish the status and role of a woman in the Kikuyu society. This has been done with the view of establishing how a woman is portrayed by the Kikuyu proverbs given than the Kikuyu proverbs are means of propergating the society's ideals regarding marriage, parenting, work, property ownership and leadership. Owing to the coincidental nature of proverb usage, two means of collecting data were used. These are library research and interviews. Forty four proverbs were collected, translated and analyzed qualitatively with the aim of revealing how a Kikuyu woman is portrayed.

The results have been presented descriptively and in a tabular form. This study was guided by the theory of Feminism under Feminist Critical Approach. The findings of this research are expected to widen the knowledge of the readers as regards Kikuyu proverbs with special reference to women's portrayal. It is also hoped that the study will shed some light on the traditional beliefs that militate against women liberation efforts besides giving impetus to researchers who would wish to carry out investigations on related fields.

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia usawiri wa mwanamke katika jamii ya Wakikuyu kama inavyobainika kupitia kwa matumizi ya methali.

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchanganua methali zilizoteuliwa ili kubainisha mielekeo na mitazamo ya wanajamii kuhusu ndoa, malezi, kazi, umilikaji mali na utawala.

Kwa sababu methali hutumika bila kutarajiwa, mbinu mbili za ukusanyaji data zilitumika. Mbinu hizi ni mahojiano na utafiti wa kimaktaba. Methali arobaini na nne zilikusanywa, zikatafsiriwa na kuchanganuliwa. Maelezo pamoja na jedwali yalitumiwa kufafanua matokeo. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uelemea Kike, mkabala wa Ufeministi Hakiki. Utafiti huu unakusudiwa kutoa mchango adhimu katika nyanja ya fasihi kwa kupanua uwanda wa maandishi yanayohusu methali za Kikuyu. Aidha, utafiti huu utakuwa kichocheo kwa watafiti ambao wangependa kutalii nyanja zingine za fasihi simulizi mbali na kumulika methali kama mojawapo wa vipengele vya utamaduni vinavyodumaza na kutinga maendeleo ya mwanamke.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa mada

Methali ni sehemu ya lugha na hutumiwa kuyatafakari, kuyapima maisha na kufunzia jumuiya. Huibua falsafa na hekima ya wale wanaozitumia pamoja na kufunza maadili ya kijamii na itikadi zao. Kwa mujibu wa Abdilatif (1978: 1) katika Wandera (1996) hakuna fasihi yoyote ambayo imechipuka na kuendelea kuishi katika ombwe tupu. Fasihi yoyote (methali zikiwemo) hupata uhai wake na maudhui yake kutoka kwa jamii inayoichipuza. Tofauti ya kijinsia na mielekeo hasi kumhusu mwanamke ni mojawapo wa maswala ya kitamaduni yanayorithishwa kupitia kwa kitendo cha ujamiishaji kinachohalalishwa na kuendelezwa na asasi mbalimbali za kijamii kupitia kwa methali, ngano, miiko na hata vichekesho.

Hata baada ya mikakati ya kitaifa na kimataifa ya kumuendeleza mwanamke, nafasi yake hasa katika mataifa ya Kiafrika haijabadilika. Hii inaashiria umuhimu wa kushughulikia swala hili.

Katika kupiga mwangwi maoni ya Momanyi (1998), haitoshi kudondoa maeneo na kutoa santuri kuhusu ugandamizwaji wa mwanamke. Misingi ya ugandamizwaji huo unaoyakinishwa na mila na utaratibu wa utamaduni haina budi kuchunguzwa. Halliday(1978) anatoa kauli kwamba mtoto anapojifunza lugha huwa pia anajijengea taswira ya uhalisia uliomzunguka. Methali kama chombo cha ujamiishaji kinachotumia lugha kama msimbo wa kupitishia ujumbe wake huakisi hali halisi ya maisha ya wanajamii. Ifahamike kuwa lugha hutumika kama ishara ya kuifasiria mifumo na miktadha ya kijamii na kiutamaduni. Mtoto huishilia kujifunza majukumu yake yaliyoainishwa na jamii kulingana na uana wake (Coates 1986).

Ni muhimu kuchunguza amali hizi zinazopitishwa kama mirathi kwani ni bayana kuwa hadhi ya mwanamke haitokani na silika bali jinsi alivyoainishwa kuwa katika utamaduni uliosheheni taasubi za kiume.Utafiti huu uliangalia jinsi mwanamke alivyosawiriwa kupitia kwa mitazamo ya wanajamii inayopitishwa katika methali *(thimo)* za Wakikuyu ili kubainisha kama mielekeo hiyo inamdunisha au kumtukuza mwanamke.

Jambo hili limetupa picha halisi ya mwanamke wa Kikikuyu.

1.2 Mada ya utafiti

Jamii ya Wakikuyu ni jamii inayozingatia mfumo wa itikadi ya kuumeni. Ingawa inafahamika kuwa jamii hii inatawaliwa na itikadi hii, jambo hili halijachunguzwa kwa kina katika nyanja ya fasihi simulizi. Utafiti huu ulichunguza jambo hili kwa kina na kutoa mapendekezo yaliyotokana na matokeo ya utafiti.

1.3 Madhumuni

1. Kudhihirisha jinsi methali zinavyomchora mwanamke katika jamii ya Wakikuyu.
2. Kuchanganua nafasi ya mwanamke na majukumu yake katika jamii ya Wakikuyu kama inavyobainika katika methali.
3. Kuonyesha kuwa methali katika jamii ya Wakikuyu hubainisha uhalisia wa mahusiano kwa mujibu wa uana.

1.4 Nadharia tete

1. Methali za Kikikuyu humsawiri mwanamke kwa njia fulani inayomdunisha.
2. Methali hubainisha nafasi na majukumu maalum ya mwanamke katika jamii ya Wakikuyu.
3. Methali huibua uhalisia wa mahusiano kwa mujibu wa uana katika jamii ya Wakikuyu.

1.5 Umuhimu wa utafiti

Kama zao la mazingira maalum ya kijamii, methali huakisi harakati za jamii husika na kutoa jukwaa la kutathmini michakato ya kimaendeleo ya jamii husika. Utafiti huu utachangia nyanja ya fasihi kwa kupanua uelewa wa methali za Kikikuyu na utamaduni wa jamii ya Wakikuyu hasa kuhusu swala la mwanamke kwani methali kama sehemu ya fasihi hutuchorea picha halisi ya maisha ya jamii husika.

Kumekuwa na machweo mapya kuhusu nafasi ya mwanamke katika maendeleo ya jamii. Mlacha (1993) anaonyesha jinsi mielekeo, mitazamo na tabia zinazomhusu mwanamke huendelezwa kupitia mawasiliano ya kitamaduni kama methali, vitendawili na ngano.

Ni muhimu kuchunguza vipengele hivi vya utamaduni vinavyozidi kumsakama mwanamke na kumnyima nafasi ya kujiendeleza katika miktadha ya kijamii. Ni bayana kwamba wanaotetea haki za wanawake hawajaangazia maeneo mengine kama methali. Utafiti huu utatoa nafasi ya kuchunguzwa kwa vipengele vya kitamaduni vinavyoibua tofauti ya hadhi baina ya wanajamii. Chambilecho Okindo (1995), methali hugusia maadili na amali za kijamii zinazoeleweka na kukubalika katika muktadha wa kitamaduni.

Tafiti nyingi zinazohusiana na methali hujikita katika maana na matumizi bila kuangalia kwa uyakinifu maswala fulani ya kijamii yanayowasilishwa na methali hizo. Utafiti huu umeonyesha uhusiano uliopo baina ya methali na hali halisi ya maisha ya Wakikuyu.

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza methali kama chombo cha ujamiishaji. Utafiti huu ulichunguza methali arobaine na nne zinazoangazia maeneo ya ndoa, malezi, kazi, umilikaji mali na utawala. Maeneo haya yameteuliwa kwa sababu yanawakilisha jukwaa maalum ambapo uhusika na nafasi ya mwanamke inaweza kutathminiwa kwa uyakinifu zaidi.

Mtafiti aliangazia Wakikuyu wanaotoka katika maeneo ya Thika sehemu ya Gatanga, Nyandarua sehemu ya Kipipiri na Kiambu sehemu ya Rironi. Wahojiwa walikuwa wazee wa rika la *Irungu* wanaojulikana kwa jina lingine kama rika la *Maina*. Wazee hawa wana umri wa kati ya miaka 60 – 70.

Maelezo ya istilahi

Methali - Vifungu vya maneno vinavyotumika kijazanda na vinavyotoa muhtasari wa muktadha wa kitamaduni, tukio au tajiriba na hutumiwa kuonya, kuasa, kufahamisha, kufariji na kufafanua jambo.

Utamaduni - Maisha ya kawaida ya watu husika; mazoea yao kama vile dini, mila,siasa na mfumo wa kiuchumi (Wandera 1996).

Jamii - Kundi la watu mahsusi wanaotofautiana na makundi mengine kwa misingi ya lugha, desturi na mila.

Itikadi - Mfumo wa mawazo na maadili yaliyopendekezwa na jamii ili kuwaongoza waanajamii katika kufanya maamuzi yanayohusu amali na hali mbalimbali anazokumbana nazo mwanajamii katika maisha.

Uyakinifu - Habari ya kweli na wazi, yenye mambo yaliyokubalika na yaliyomo katika hali halisi.

Jinsia /Uana - Hali ya kuwa mwanamke au mwanamume kimaumbile, kigezo kinachotumiwa kugawa majukumu katika jamii.

Ubabeume - mfumo wa kijamii unaozingatia itikadi ya kuumeni. Huzichukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida za kufuatwa katika jamii nzima.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliangazia maandishi ya wasomi mbalimbali pamoja na tafiti zilizofanywa kuhusiana na mada hii. Amemulika kwa makini machapisho yanayomhusu mwanamke na vilevile yale yanayohusu methali kwa mujibu wa upeo na mipaka ya utafiti huu. Kufanya hivi kumemuwezesha mtafiti kubainisha mshabaha na tofauti iliyopo baina ya utafiti huu na wa wasomi wengine.

Kama wajibu, na kwa kuzingatia mihimili ya nadharia iliyoongoza utafiti huu, mtafiti amejadili kwa kifupi asili ya tofauti za kiuana kulingana na historia. Mtafiti amejadili mikabala mbalimbali ya nadharia ya uelemea kike huku akionyesha udhaifu wa kila mojawazo. Ameonyesha vilevile ufaafu wa nadharia aliyoichagua.

2.2. Asili ya tofauti ya nafasi ya wanawake na wanaume katika jamii.

Kulingana na Engels (1975), nafasi ya mwanamke ina kitovu chake katika migawanyiko ya kitabaka. Anadai kwamba jamii za jadi zilikuwa na uthamini sawa wa wanawake na wanaume. Jamii hizi pia ziliishi maisha ya ujima.

Jamii hizi zilibadilika na kuwa jamii zenye ustarabu na zilianzisha ubabeume kama mfumo unaotawala mahusiano yote ya jamii ile. Hali hii ilizuka pale ambapo kazi za wanaume kama vile uwindaji na ufugaji zilianza kuleta faida kuliko kazi za wanawake za nyumbani. Kuongezeka kwa mali upande wa wanaume kulizua wazo la mali ya kibinafsi. Matokeo haya yalisababisha kurundikiziwa umuhimu kwa shughuli zote zinazohusiana na mwanamume. Mwanamke alianza kumtegemea mwanamume kiuchumi. Mwanamke kwa mujibu wa Engels alifikia kikomo cha kuchukuliwa kama mtu mwenye hadhi sawa na mwanamume.

Maoni haya ya Engels yalimpa mtafiti mshawasha wa kutaka kujua kama hali hii inajitokeza katika jamii ya Wakikuyu kupitia matumizi ya methali zao. Hii ni kwa sababu jamii hii hujihusisha na shughuli ya usasi na ufugaji. Kwa kuangalia ugawaji wa majukumu katika jamii hii kama yanavyoibuliwa na methali zifuatazo, tumeweza kupata picha halisi ya mwanamke wa Kikikuyu.

Hivyo maoni ya Engels yalimfanya mtafiti kuangazia majukumu haya kwa kina. Mifano ya methali zinazotuibulia tofauti ya majukumu kati ya watu wa uana tofauti ni kama vile;

'Nyondo cia mundurume itiri iria'

(Matiti ya mwanamume hayana maziwa)

'Mundu utaumagaraga augaga no nyina urugaga wega'

(Mtu asiyetembea hudhani kuwa ni mama yake pekee anayejua kupika)

2.3 Maandishi kuhusu taswira ya mwanamke

Upekuzi wa vitabu, majarida na tasnifu ulikuwa dafina kubwa kwa utafiti huu. Hata hivyo hakuna habari zilizopatikana miongoni mwa kazi hizi iliyoshughulikia usawiri wa mwanamke katika methali za Kikikuyu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa jambo hili halikuwa limeshughulikiwa.

Akizungumzia swala hili Fennie (1904) anadokeza kwamba mwanamke anakumbwa na shida nyingi zinazomgubika daima. Rosaldo (1974: 21) na Goldenberg (1979: 25) nao wanaongezea kwa kudai kuwa kutokana na kumpa mamlaka mwanamume, hadhi na thamani zimeishilia kurundikwa na kuambatanishwa na shughuli za mwanamume. Utafiti huu umejaribu kuangalia kama madai haya yana mashiko katika jamii ya Wakikuyu. Mwanamume amepewa nguvu za kiungu, ukweli unaoyakinishwa na beti zifuatazo kutoka katika *Utendi wa Mwanakupona*.

26. Siku ufufuliwao
    Nadhari ni ya mumeo
    Taulizwa atakalo
    Ndilo takalotendeka

27. Kipenda wende peponi
    Utakwenda dalhini
    Kinena wende motoni
    Huna budi utatiwa

Ingawa hii ni kazi ya kubuni na kwa hivyo kuna uwezekano wa kupiga chuku, ni ukweli usiopuuzika kuwa msanii hupata maudhui yake kutokana na tajiriba yake katika jamii inayomkuza.

Hivyo Mwanakupona alipata malighafi yake kutoka kwa jamii ya wakati wake. Maoni haya ya Mwanakupona yanaafikiana na methali ya Wakikuyu isemayo kwamba unyende wa mwanamume huitikiwa na mfalme.

'Mbu ya mundurume itikaguo ni muthamaki'

Methali hii inawasilisha wazo kuwa mwanamume si mtu wa kawaida na kwa hivyo anapopiga unyende, lazima kuwe kumetokea jambo lisilo la kawaida ambalo linahitaji kusuluhishwa na mfalme au mtu mwenye mamlaka makubwa.

Kwa kuangazia methali za Kikuyu, mtafiti amejaribu kuangalia kama dhana hii inajitokeza.

Kipury (1983) anasema kuwa katika jamii ya Wamaasai, wanawake hufanya kazi nyingi. Kazi walizotengewa ni kama vile kujenga nyumba, kutafuta kuni, kuteka maji, kukamua ng'ombe na kutayarisha chakula, kunadhifisha nyumba na maboma ya mifugo pamoja na kulea watoto. Ingawa kazi ya kulisha mifugo ni kazi ya wanamume, wanawake huulizwa mara kwa mara kusaidia.

Kipuri ametofautiana na mtafiti kwa vile yeye ameangazia fasihi simulizi katika upana wake. Utafiti huu umeangazia nyanja mahsusi ya methali za Kikuyu.

Matteru (1982) anadokeza kuwa katika hadithi fupi mwanamke amesawiriwa kama duni, chombo cha kumalizia uchu wa mwanamume na kifaa cha kufanya kazi za sulubu. Utafiti huu wa Matteru umetusaidia kuchanganua nafasi ya mwanamke hasa katika asasi ya ndoa na mitazamo ya watu wa jamii ya Wakikuyu kuhusu swala hili kupitia kwa methali mbalimbali tulizochanganua. Waandishi wengi wametumia miwani hii ya Matteru kumtazama mwanamke. Kifungu kifuatacho kilichonukuliwa kutoka Mbilinyi na Omari (1996: 147) ni ithibati kamili ya baadhi ya kazi za kifasihi zinazombeza na kumdekua mwanamke.

> "Miguu yake ya kuchonga ilibeba kiwiliwili cha mwili mwororo...kiuno cha bapa....Mabega yake ya kadiri yaliyoning'iniza mikono ya mbinu, huku katikati ya mabega haya kukiwa kumehifadhiwa kifua chembamba chenye kubeba titi changa na chonge zilizotuna na kuwachungulia vijana wa kila aina...utadhani titi hizo zilikuwa zikiwakonyezea!"

Baada ya kumrundikizia sifa hizi kemkem, mwandishi anatubadilishia mkondo wa mawazo kwa kumsawiri mwanamke huyu kama aliyepungukiwa na akili kwa kusema-:

> "Shingo lake fupi kidogo lilibeba kichwa chenye busara kidogo na nywele tititi."

Ingawa haya ni maoni ya mwandishi, jamii yake imesaidia kuyaumba kwa sababu imebainika waziwazi kuwa msanii huchota maudhui yake kutoka kwa mazingira anamokulia.

Mtazamo huu kumhusu mwanamke umesakini sana katika jamii nyingi za Kiafrika. Ni bayana kuwa waandishi wengi wa kazi za kifasihi wameishilia kuelezea hali ilivyo kuhusu mitazamo ya wanajamii kumhusu mwanamke bila kufukua mizizi ya shida zile.

King'ei (1982) ameshughulikia methali za Kikamba kwa kufuata misingi ya methali za Kiswahili. Yeye amejikita zaidi katika muundo wa methali.Utafiti huu umeenda hatua moja zaidi kwa kuzingatia maudhui katika kuchunguza jinsi mwanamke alivyosawiriwa na methali za Kikikuyu.

Chesaina (1989) ametafiti jukumu na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia. Ameshughulikia tamthilia ya *Hatia (*1972) na *Nguzo Mama* (1982). Tofauti iliyopo baina ya utafiti huu na wa Chesaina ni kuwa mtafiti ameangazia utanzu wa fasihi simulizi ilhali Chesaina alijihusisha na fasihi andishi. Tofauti nyingine ni kuwa yeye alichanganua matini ilhali mtafiti wa kazi hii alienda nyanjani na kuwahusisha wanajamii hawa kupitia kwa mahojiano.

Mekacha (1993) akichambua nyimbo pendwa anatupa picha ya mwanamke aliyejaa uovu. Anatamatisha kazi yake kwa madai kuwa mwanamke ana uchu uliokithiri. Pia ana wivu ambao umeonyeshwa kuwa ndio chanzo cha maovu yote katika jamii. Utafiti wake, tofauti na huu umeegemea sana upande wa maovu ya mwanamke. Mtafiti anatambua kwamba Mekacha ameangazia utanzu ambao maudhui yake hutegemea kizazi kinacholengwa. Isitoshe wasanii wengi wa nyimbo pendwa hulitalii soko la nyimbo zao kabla ya kuzitoa. Hii ina maana kuwa wanayoyaimba hutegemea hadhira. Jambo hili ni tofauti kabisa na nyanja tuliyoishughulikia.

Lugano (1989) amehakiki usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya nne za Euphrase Kezilahabi. Anadai kuwa Kezilahabi anamtamausha mwanamke kwa kuonyesha ukombozi wake kama maṣigazi ambayo hayawezi kufikiwa. Kwa mujibu wa Lugano, Kezilahabi anaendeleza falsafa ya jamii yake kongwe kuhusu mwanamke- falsafa ambayo inamchukulia mwanamke kuwa kiumbe duni aliye chini ya utawala wa mwanamume.
Utafiti huu umetofautiana na wa Lugano kwani uliangalia methali na jinsi zinavyomsawiri mwanamke zikiwa kama mojawapo ya vipengele vya utamaduni wa Wakikuyu .

Ndungo (1985) ameshughulikia jinsi ambavyo taswira ya mwanamke imebadilika katika vipindi na mazingira mbalimbali vya kihistoria. Ameangalia enzi ya umwinyi ikiwakilishwa na *Utendi wa Mwana Kupona* (1860), Kipindi cha ukoloni mkongwe kikiwakilishwa na *Kaburi Bila Msalaba* (1969) na kipindi cha baada ya ukoloni kikiwakilishwa na *Utengano* (1980). Ndungo anatoa kauli kwamba ukombozi wa tabaka la chini utategemea kuangushwa kwa tabaka la juu.
Utafiti wa Lugano na Ndungo umejikita katika riwaya na tenzi ilhali utafiti wetu umeshughulikia methali za Kikikuyu.

Mbughuni (1982) ameandika makala kuhusu taswira ya mwanamke katika maandishi ya kiriwaya ya Tanzania. Anatoa hoja kuwa taswira inayoendelezwa kupitia kwa riwaya ni ile inayomsawiri mwanamke kama mlaghai na mhalifu katika jamii. Mbughuni anamtumia mhusika Hawa katika Biblia kama kielelezo mwafaka cha mwanamke. Utafiti huu umemwangazia mwanamke kama anavyosawiriwa na methali za Kikikuyu .

Kazi ya Senkoro (1982) imewahakiki wahusika wa kike katika riwaya ya Kezilahabi- *Dunia Uwanja wa Fujo*. Anatoa rai kuwa fasihi ipatikanayo katika mfumo wa kibepari imembidhaaisha mwanamke na kumwonyesha kama kiumbe duni ambaye jukumu lake kubwa liko jikoni na kitandani. Ingawa majukumu haya yanakubalika na jamii nyingi, waandishi wengi wameiangalia hali ile kama inayomdunisha mwanamke.

Utafiti huu umetudhihirishia kuwa haya ni baadhi tu ya majukumu anayoyatekeleza mwanamke kwa sababu ya maumbile yake na wala hayaonyeshi uduni kwa vyovyote vile.

Mule (1991) ameshughulikia taswira ya mwanamke kama inavyojitokeza katika tamthilia za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa kike Sheila Ari Ryanga na Ali Katini Mwachofi kutoka Kenya na Peninah Muhando na Anjelina Chogo wa Tannzania. Ushabihiano uliopo baina ya utafiti huu na ule wa Mule ni kuwa tafiti zote mbili zinajishughulisha na taswira ya mwanamke. Tofauti kubwa ni kuwa Mule anashughulikia tamthilia. Mule aliongozwa na nadharia ya Ujamaa wa kike ilhali utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ulemea kike mkabala wa Ufeministi hakiki.

Wandera (1996) amechunguza usawiri wa mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa karne ya 1800 hadi 1900. Katika utafiti wake aligundua kuwa picha ya mwanamke Mswahili imejengwa na mielekeo ya utamaduni wa wakati huo. Utamaduni huo haukuwa wa kugandamiza mwanamke wala mwanamume bali ulitenganisha majukumu na nafasi ya kila mmoja kwa misingi ya vigezo kama uana, maumbile, sheria ya dini ya Kiislamu, mila, siasa na mfumo wa kiuchumi. Ingawa utafiti huu sawa na utafiti wa Wandera unaangazia tanzu za fasihi simulizi, tofauti iliyopo ni kuwa utafiti huu unaangazia picha ya mwanamke katika jamii ya Wakikuyu kutokana na methali bila kuweka mipaka ya wakati.

Utafiti ulioshabihiana kwa kiasi kikubwa na huu ni ule wa Okindo (1995). Tofauti uliyopo baina ya tafiti hizi ni kuwa Okindo anaangazia jamii ya Wakisii ilhali utafiti huu unaangazia jamii ya Wakikuyu. Okindo alitumia tafsiri huru na tafsiri sabilia. Katika utafiti huu, tafsiri maana ilikimu mahitaji ya utafiti. Hii ni kwa sababu tunataka kutumia mizani sawa kwa methali zote ili pasiwe na tofauti itakayosababishwa na matumizi ya njia tofauti za kutafsiri. Okindo amechanganua methali thelathini na nne zilizokusanywa kutoka katika jamii ya Abagusii. Amedhihirisha kupitia kwa uchunguzi wake kuwa methali nyingi za Kikisii husisitiza juu ya utiifu na tabia njema kwa wasichana ili watakapoolewa wawe watu wa kutegemewa.

Fauka ya hayo, aligundua kuwa wasichana hutumiwa kama chambo cha kunasia mali kupitia kwa njia ya ulipaji mahari. Kwa mujibu wa Okindo, mwanamke katika jamii ya Wakisii amesawiriwa kama kiumbe dhaifu na mwoga ambaye daima anahitaji kulindwa na mwanamume. Kazi yake hata hivyo ilikuwa mlizamu ulioamsha mshawasha wa kutaka kuchunguza jinsi methali zinavyomsawiri mwanamke katika jamii ya Wakikuyu.

2.4 Maandishi kuhusu methali

Methali ni utanzu wa fasihi simulizi.Methali hata hivyo zimeendelea kuhifadhiwa katika maandishi tofauti na ilivyokuwa zamani. Fasili ya methali hutegemea mkabala anaochukua mfasili na vilevile lengo lake. Kulingana na Wamitila (2001:ix), methali ni msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu au uzito, wenye muundo au sifa za kishairi na unaokusudiwa kuadibu au kuelekeza, kuelimisha na kushauri. Fasili hii inatuibulia umuhimu wa kuangalia machapisho mbalimbali yanayohusu methali.

Oduyoye (1979) alitafiti kuhusu uhalisia wa hali ya mwanamke wa Asante kama inavyobainishwa na methali. Aligundua kuwa lugha kuhusu mwanamke hasa katika methali hubainisha nafasi na jukumu lake katika jamii. Anasema kuwa picha yake kupitia kwa methali huhalalisha majukumu anayotekeleza. Utafiti wetu uliangazia maeneo ya ndoa, malezi, kazi, umilikaji mali na utawala tofauti na alivyofanya Oduyoye. Nketia akizungumzia methali katika jamii ya Akan katika Finnegan (1970:389-390) anasema kuwa thamani ya methali miongoni mwa wanajamii hawa haitokani na ufunuo wa mawazo ya zamani. Anagundua kuwa methali ni kielelezo cha lugha yenye nguvu zaidi. Utafiti wetu unaafikiana na kauli hii ya Nketia lakini mtafiti atapiga hatua zaidi na kuangalia kipengele cha maudhui .

Finnegan (1970) akitafiti kuhusu fasihi simulizi miongoni mwa Waafrika aligundua kuwa methali huyapa uhalisia mawazo dhahania. Finnegan alishughulikia uwanda mpana wa fasihi simulizi. Kauli hii ilikuwa kauli ya jumla. Utafiti wetu ulichunguza methali kama mojawapo wa utanzu wa fasihi simulizi. Tulijikita katika jamii ya Wakikuyu.

Ifahamike kuwa methali tofauti na tanzu zingine za fasihi kama vile ngano hutumia maneno machache kufumbata mada pana. Sifa hii huzifanya methali kutumika zaidi katika mazungumzo ya kawaida.

2.5. Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uelemea kike mkabala wa ufeministi hakiki. Uelemea kike ni dhana iliyobuniwa na mwanasoshiolojia wa Kifaranza anayejulikana kama Charles Fourier katika mwanzo wa karne ya kumi na tisa. Wakati ule ilitumika kurejelea mwamko wa mwanamke aliyezinduka na hivyo kutaka kubadilisha hali yake katika jamii. Leo hii dhana hii hutumika kurejelea mitazamo mbalimbali ya tofauti baina ya wake na waume katika jamii, asili yake na jinsi inavyoweza kuboreshwa (Mitchel na Oakley 1986). Nadharia ya uelemea kike ina mikabala mbalimbali inayodhihirisha sifa zifuatazo-:

1. Mikabala yote inakubaliana kuwa mahusiano baina ya uana yana kasoro inayohitaji kurekebishwa. Wanauona uana kama chanzo cha matatizo ya mwanamke.
2. Hukashifu mambo ambayo yanaonekana kama ya kawaida na ya kimaumbile.
3. Huangazia maswala yote ya kihistoria na siku za usoni za jamii.
4. Uelemea kike sio dhana tu, hudhamiria kubadilisha ulimwengu na hasa mahusiano baina ya uana ili kila mmoja aweze kuyaishi maisha kwa ukamilifu wake.
5. Mapendekezo ya uelemea kike hukabiliana na pingamizi nyingi.

Uelemea kike unajumuisha mikabala mbalimbali inayoelezea tofauti baina ya tajiriba ya wake na waume katika jamii. Miongoni mwa mikabala hii ni kama ifuatayo-:

2.4.1. Ufeministi Huru

Ufeministi huru una kitovu chake katika muktadha wa filosofia huru ya karne ya kumi na sita na kumi na saba baada ya Masiha. Mkabala huu unashikilia kuwa wake na waume wanashabihiana kithamani kwa mujibu wa maumbile lakini wanawake wamenyimwa nafasi ya kutambulisha uwezo wao kwa sababu ya uana wao. Wanasisitiza kuwepo kwa marekebisho ya kisheria na kuwapa wanawake na wanaume nafasi sawa. Wanaamini kuwa ujamiishaji wa kiuana ndio chanzo cha tofauti zilizoko katika jamii.

Kwa hivyo wanaamini kuwa mabadiliko katika mtindo wa ujamiishaji unaweza kuleta ukombozi na usawa katika mahusiano ya kiuana.

Wanaufeministi hawa wanaamini kuwa kila mwanadamu anapaswa kutazamwa kama binadamu ila si mume au mke. Wana maono ya ulimwengu uliomilikiwa na binadamu sawa. Udhaifu wa mkabala huu ni kuwa wana maoni yanayokinzana. Huku wakitetea usawa wa kiuana, wanaegemea zaidi kumtetea mwanamke hasa wa tabaka la juu.

2.4.2. Ufeministi wenye msimamo mkali

Mkabala huu ulizuliwa katika miaka ya sitini. Uliasisiwa na kundi la wanawake wa umri wa makamo waliokuwa wamepata elimu ya juu. Wanawake hawa mwanzoni walikuwa wanachama wa mashirika mengine yaliyopigania amani, haki na uangamizaji wa taasisi zilizoendeleza unyanyasaji. Baada ya kugundua unyanyasaji ulioendelezwa kwa misingi ya uana, waliamua kuunda mashirika yaliyokuwa na lengo la kuangamiza taasisi na ngome zote walizodhania kuwa zilimgandamiza mwanamke. Wanaufeministi wenye msimamo mkali wanaamini kuwa unyanyasaji wa wanawake ndiyo mbegu inayozalisha maonevu yote ya kiuana. Kulingana na waitifaki hawa, maonevu haya yana historia ndefu, yalianzia pale ambapo itikadi ya kuumeni ilianzia.

Ufeministi wenye msimamo mkali unaangazia itikadi ya kuumeni na ugandamizwaji wa wanawake unaotokana na hali hii kuanzia kwa mahusiano ya kinyumbani hadi kufikia maisha ya hadharani.

Wanasisitiza kutazamwa upya kwa sifa za wanawake za ubunifu na ulezi, thamani ambazo zimechafuliwa na kuchakaishwa katika jamii iliyotawaliwa na itikadi za kuumeni. Wanaufeministi wa msimamo mkali humtazama mwanamke kama kitengo cha jamii kilichonyanyaswa ulimwenguni kote; katika ulimwengu unaodhibitiwa, kumilikiwa na kutawaliwa na mwanamume (Ramazanoglu 1982:13) katika Ndungo (1988:48). Wanauona udunishwaji wa wanawake katika jamii zote zinazoshikilia itikadi ya kuumeni kama idhibati ya uwezo wa mfumo huu kuamua juu ya hadhi ya wanawake. Wanawaona wanaume kama wanaomiliki asasi zote za kijamii.

Ili kuikabili hali hii Wanaufeministi hawa wanapendekeza kutenganishwa kwa wake na waume katika hali zote.

Wanaosifika sana kwa msimamo huu ni wale wanaufeministi wa New York ambao husisitiza kuwa na maduka ya wake peke yao, barabara na hata vyumba vya starehe. Udhaifu wa mkabala huu ni kuwa unafifisha asasi ya ndoa na hivyo kuangamiza maisha ya baadaye ya jamii. Kasoro nyingine ni kwamba wanaufeministi wa msimamo mkali wanapendekeza ubasha, jambo ambalo limezusha mjadala mkali hasa kati ya viongozi wa kidini.

2.4.3. Ufeministi wa Kijamaa

Una asili yake katika mawazo ya Karl Marx iliyozuka katikati ya karne ya kumi na tisa kutokana na mapinduzi ya viwandani. Wanaufeministi wa kijamaa wanashikilia kauli kwamba chanzo cha ugandamizwaji wa wanawake ni kwenye mifumo ya kibepari na ile ya kuumeni. Kwao, ubepari na ubabeume hushirikiana ili kumdhalilisha mwanamke, ingawa wanatambua umuhimu wa mfumo wa matabaka na mahusiano ya kiuchumi ya kibepari.

Ingawa mkabala huu una misingi yake katika umilikaji mali, wanaufeministi hawa huamini kuwa ujamaa ungewawezesha wanawake kumiliki mali na hivyo kuwa katika jukwaa sawa na wanaume.
Udhaifu ulioko ni kuwa Wanaufeministi wa kijamaa huangazia tofauti ya uwezo hasa wa kimali baina ya wanawake na wanaume.

2.4.4. Ufeministi Hakiki

Mkabala huu umeelezwa kwa kina na Kolodney (1986). Alionyesha umuhimu wa kuangazia jinsi tofauti ya uwezo kati ya wanawake na wanaume inavyobainishwa katika kazi za kisanaa. Mkabala huu una mihimili ifuatayo ambayo imekuwa nguzo muhimu ya utafiti huu-:

1. Miundo mipya ya kazi za usomi ni zao la mitindo ya kiutamaduni iliyokuweko tangu zamani. Maendeleo ya kazi za sanaa husababishwa na misukosuko ya kiuchumi na kijamii katika mpangilio wa jamii na utamaduni kwa jumla.
   Mhimili huu unaamini umuhimu wa kutazama historia ili kuelewa yaliyopo.
   Inatambua yaliyopita kama malighafi ya kuundia historia ya sasa na ya wakati ujao.

Matokeo yake ni kuwa utathmini wa fasihi, hasa fasihi simulizi iliyopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine hutuwezesha kuelewa hali ya wakati uliopita.

Kutokana na mhimili huu mtafiti alibidika kuangalia historia ya jamii ya Wakikuyu ili kubaini picha ya mwanamke wa Kikikuyu ya wakati uliopita na wa sasa.

2. Mhimili wa pili wa mkabala huu ni kuwa upataji wa maana kutoka kwa matini semwa au andikwa humtegemea msomaji au hadhira. Msomaji au hadhira inaweza kupata maana iliyotofautiana kutokana na madhanio, hali, mandhari na mahitaji. Kutokana na kipengele hiki maana ya methali ilifafanuliwa. Lugha iliyotumika pia iliangaziwa.
3 Mkabala huu pia hujaribu kuvumbua jinsi thamani za kijumisia zinaafikiwa na msikilizaji, msomaji na mtazamaji. Vilevile huangalia ni amali zipi za kijamii zinazopaliliwa na mitazamo hii ya thamani. Mkabala wa Ufeministi hakiki hutoa uhitaji wa kuelewa njia ambazo mifumo ya kiutamaduni ya jamii hushamirishwa na kuzatitishwa na fasihi ya jamii fulani. Kutokana na kipengele hiki, taswira ya mwanamke ilifafanuliwa kwa mujibu wa thamani anayopewa katika methali. Hii ilibainika kutokana na lugha iliyotumiwa na maudhui yaliyozungumziwa.

Kwa kutumia mkabala huu, mtafiti aliweza kuhusisha hali ya mwanamke wa Kikikuyu kama anavyosawiriwa kupitia methali na uhalisia wa utamaduni wa mwanamke katika jamii hii. Mtafiti aliweza kuchunguza sura ya mwanamke inayoendelezwa na jamii husika na kutambua kama uana ni sababu kuu ya nafasi anayopewa mwanamke katika jamii hii.

Sura ya mwanamke ni mwangwi wa maisha ya mwanamke na tajiriba yake katika maisha. Ni kupitia kwa mkabala huu ambapo mtafiti alielewa maana haswa ya kuwa mwanamke katika jamii ya Wakikuyu. Mkabala huu ulimuwezesha mtafiti kutoa maelezo na kutathmini nafasi ya mwanamke na vilevile kuelewa jinsi picha ya mwanamke katika jamii ya Wakikuyu inavyoundwa na ulimwengu wa utamaduni unaomzunguka.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ameelezea kwa kina mbinu na hatua alizozingatia katika kuikusanya data yake. Sura hii imegawanyika katika sehemu mbili; sehemu ya kwanza inahusu uteuzi wa sampuli na ukusanyaji data ambayo pia imegawanyika katika sehemu mbili na sehemu ya pili inayohusu uchanganuzi wa data.

Matumizi ya methali katika maongezi ya kawaida hayabashiriki. Hutokea kama jambo la sadfa na kwa hivyo mtafiti alitumia njia mbili za ukusanyaji data katika hatua tofautitofauti za utafiti huu. Njia hizi ni:- mahojiano na uchunguzi wa kimaktaba.

3.2 Uteuzi wa sampuli na ukusanyaji data

Utafiti huu ulitekelezwa kwa njia mbili zifuatazo-:

(a)Utafiti wa kimaktaba

Utafiti wa kimaktaba ulihusisha kutembelea maktaba mbalimbali kama vile maktaba ya chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Egerton na bewa la Laikipia. Nia kuu ya kutembelea maktaba hizi ni kufanya upekuzi wa vitabu, tasnifu na majarida ili kubaini tafiti zilizofanywa katika nyanja ya fasihi na hasa kumhusu mwanamke. Lengo la pili lilikuwa kukusanya methali nyingi iwezekanavyo kumhusu mwanamke kutoka katika jamii ya Wakikuyu. Upekuzi huu wa vitabu ulikuwa kijalizi cha utafiti wa nyanjani kwani ulimwezesha mtafiti kukusanya methali zilizoandikwa vitabuni. Kutokana na mbinu hii, data iliyokusanywa ni methali za Kikikuyu zinazohusiana na uana.

(b)Utafiti wa nyanjani

Utafiti huu ulihusisha mahojiano na udadisi. Mahojiano yameelezwa na Seitel (1972) kama njia mwafaka zaidi ya kukusanya data kuhusu methali.Utafiti ulifanyika katika wilaya tatu za mkoa wa kati. Wilaya hizi ni Thika, Kiambu na Nyandarua. Kata moja iliteuliwa kutoka katika kila wilaya. Wahojiwa walitoka katika kata za Kipipiri (Nyandarua), Rironi (Kiambu) na Gatanga (Thika). Sababu ya kuteua maeneo haya ni kuwa wakaaji wa maeneo haya ni kiwakilishi mwafaka cha jamii pana ya Wakikuyu.

Isitoshe, hizi ni sehemu za mashambani na kwa hivyo wakaaji wake hawajazugwa sana na utamaduni wa kigeni wala kuathiriwa na miamko ya makundi ya akina mama wanaohubiri usawa wa kiuana.
Mtafiti aliwahoji wasailiwa kumi na watano waliokuwa wa rika la *Irungu* wenye miaka kati ya sitini na sabini. Wasailiwa hawa walitosheleza mahitaji ya kazi hii kwani kulingana na Milroy (1987:84), kundi ndogo la sampuli humwezesha mtafiti kupata habari za kina kuhusiana na mada yake.

Sababu ya kuchagua rika hili ni kuwa ndilo rika lililo kongwe sana miongoni mwa wanajamii hawa. Watu wa rika hili walitahiriwa kabla ya kutangazwa kwa hali ya hatari nchini Kenya na kwa makadirio yangu walikuwa na umri wa kati ya miaka sitini na sabini. Umri huu unafaa sana kwani methali hutumiwa zaidi na wazee katika jamii. Mtafiti alihusisha wanawake na wanaume. Mtafiti hakujishughulisha na kiwango cha elimu cha wasailiwa wake kwani ni bayana kuwa matumizi ya methali hayategemei kiwango cha elimu.
Mtafiti aliwahoji wasailiwa kuhusu methali alizokuwa amezikusanya. Alifanya hivyo kwa makusudio ya kuelezwa maana na matumizi ya methali zile. Mtafiti pia alidadisi kuhusu miktadha zilimotumika na vilevile mtazamo wa wanajamii hawa kuhusu mwanamke kwa kuzingatia methali husika. Mtafiti aliwahoji wasailiwa hawa mmoja mmoja au wawiliwawili pale walipokuwa mume na mkewe. Aliwatembelea wahojiwa kama mgeni wa kawaida baada ya kuelekezwa. Alijitambulisha na kisha kueleza madhumuni ya matembezi yake. Mtafiti aligundua ya kuwa wanajamii wa umri huu walikuwa radhi kueleza mambo yote waliyoyajua kuhusu methali na kuhusu maisha ya wanajamii wa Kikuyu wa wakati wao. Ingawa maswala mengine yalikuwa nje ya upeo wa utafiti huu, mtafiti aliyanakili kwani kuwakata kalima kungeonekana kama utovu wa adabu.

Mahojiano yalitumika katika kupata , maana , matumizi na ufafanuzi uliohitajika.Udadisi ulitumika kupata maoni kuhusu swala la wanawake katika jamii ya Wakikuyu.

Methali nyingi zilikusanywa lakini zile tu zilizomhusu mwanamke ndizo zilizochanganuliwa kwa sababu ya kuzingatia upeo na madhumuni ya utafiti huu. Kupitia mbinu hii, data zifuatazo zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa:-

1. Historia ya Wakikuyu.
2. Methali zinazohusiana na uana.
3. Maoni juu ya maana ya methali.
4. Maana juu ya tofauti za kiuana katika methali.

3.2 Uchanganuzi wa data

Hatua ya kwanza ilikuwa kutafsiri data iliyonukuliwa nyanjani kutoka Kikikuyu hadi Kiswahili. Hii ni kwa sababu habari yote iliyokuwa imenakiliwa ilikuwa kwa lugha ya Kikikuyu. Mtafiti alitumia utafsiri maana. Data ya historia ya Wakikuyu ilikusanywa, kuchujwa na kuelezwa katika sura ya tatu. Baada ya hii, methali ziliwekwa katika matapo kutegemea maudhui na nyanja mbalimbali za maisha ya wanajamii kama alivyoazimia mtafiti. Nyanja hizi ni ndoa, malezi, kazi, utawala na umilikaji mali. Methali hizi zilichanganuliwa kutumia mpango wa uchanganuzi ulioundwa kutokana na mihimili ya nadharia iliyoongoza utafiti huu kama ifuatavyo:-

A **Maudhui** - Mtafiti aliyachanganua maudhui yaliyowasilishwa na methali husika. Maudhui haya yalimuelekeza mtafiti katika kuweka methali zile katika matapo aliyoazimia kuangazia.

B **Nyanja ya maisha**- Hili ni eneo maalum la maisha lililolengwa na methali. Maudhui yalimtambulishia mtafiti nyanja maalum inayomulikwa na methali kwa mujibu wa maswala yaliyoibuka. Nyanja zilizoangaziwa na mtafiti ni ndoa, malezi, kazi, utawala na umilikaji mali.

C **Lugha**- Mtafiti alichunguza lugha iliyotumika ili kuona kama istilahi zilizotumika zinamtweza au kumtwaza mwanamke.

D **Maana**- Maana iliyowasilishwa na methali ilielezwa ili kuibua mtazamo wa wanajamii wa Kikuyu kuhusu mwanamke.

E **Taswira ya mwanamke**- Taswira ya mwanamke kutokana na methali husika ilibainishwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti. Katika hatua hii, mtafiti aliyaweka wazi maswala yafuatayo;-

(a) Jinsi methali za Kikikuyu zinavyomchora mwanamke. Mtafiti alibainisha kama mwanamke amedunishwa au ametukuzwa.

(b) Kubainisha majukumu aliyotengewa mwanamke na jamii yake.

(c) Kuibua uhalisia wa mahusiano kwa mujibu wa uana kama yanavyowasilishwa na methali.

Maoni juu ya maana ya methali na taswira ya mwanamke inayowasilishwa na methali yalichujwa. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo na jedwali katika sura ya tano.

3.3 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amejaribu kuelezea kuhusu eneo la utafiti wake, njia alizotumia kuteua sampuli pamoja na kukusanyia data pamoja na hatua alizozingatia katika uchanganuzi wa data yake. Sababu ya kuchagua kundi husika pia imedokezwa .

SURA YA NNE

4.0. MSINGI WA KIHISTORIA WA JAMII YA WAKIKUYU

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ataangazia jinsi ambavyo mwanajamii wa jamii ya Wakikuyu anajamiishwa tangu anapozaliwa hadi anapofikia uzeeni. Hii ni kwa sababu methali kama mojawapo wa tanzu za fasihi huwakilisha maisha katika uhalisia wake na kama asemavyo Okindo (1995), fasihi huibuliwa na asasi mahsusi za kijamii.
Munene (1995) anahusisha methali katika jamii ya Wakikuyu na hali halisi ya kijamii kwa kusema-:

> *"Agikuyu maturaga na ndundiro ciao cia ihoto ciitagwo thimo, kuuma kiimerera kiao."*
>
> (Wakikuyu huishi daima wakiongozwa na ukweli unaopatikana katika methali kuanzia utotoni)

Kwa kuzingatia kauli hii, ni bayana kuwa ukweli wa baadhi ya methali utamulikwa kwa uyakinifu zaidi kwa kutalii maisha ya mwanajamii tangu utotoni hadi anapofikia hatima ya maisha yake. Ifahamike pia kwamba utamaduni wa jamii unaodhihirika kutokana na historia yao huibua mitazamo na falsafa ya wanajamii hao kuhusu maisha na mazingira yanayowazunguka.

Swala la uana ni jambo linalooteshwa mizizi na tajiriba na mielekeo ya watu kuhusu uwezo, siasa, utamaduni na maingiliano ya kila siku. Dhana ya majukumu yaliyoainishwa kulingana na uana, tabia na matarajio ya jamii hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa ujamiishaji. Kwa mujibu wa Wallace na March (1991:3), watoto hufunzwa kuhusu uana wao tangu wanapozaliwa. Wanajifunza kutenda mambo ili kuonekana kama mvulana au msichana na hivyo kukubalika katika jamii husika. Mhimili wa tatu (Tazama sura ya pili nambari 2.4.3) wa nadharia ya uelemea kike mkabala wa Ufeministi Hakiki unashadidisha umuhimu wa kuangalia maisha ya mwanamke katika jamii husika kwani methali huakisi maisha ya mwanamke na tajiriba yake katika maisha. Kama anavyosema Karega (1994 :34), uchunguzi wa fasihi simulizi huhusisha utalii wa hali ya jumla ya maisha ya wanajamii husika.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

Ni kulingana na kauli hii na nguzo ya nadharia husika ambapo mtafiti alibiidika kuangazia nyanja zifuatazo za maisha ya mwanajamii Mkikuyu kama ngazi ya kufafanua zaidi maana za methali na taswira ya mwanamke wa Kikikuyu.

4.2 Asili ya Wakikuyu kulingana na visasili

Jamii ya Wakikuyu ilikuwa na imani kubwa kwa Mungu wao aliyeitwa Ngai. Mungu huyu aliishi katika kilele cha mlima Kirinyaga (mlima Kenya). Inasemekana kuwa baada ya kuumba nchi nzuri, Ngai aliumba mwanamume aliyejulikana kama Gikuyu ili aweze kutunza na kudhibiti nchi nzuri aliyokuwa ameumba Ngai. Ngai alimuumbia Gikuyu msaidizi aliyeitwa Mumbi.Watu hawa wawili waliteremka kutoka mlima Kirinyaga na kuelekea upande wa kusini.Walifanya makao yao mahali palipoitwa *Mukurwe wa Nyagathanga.*

Walijaliwa kupata watoto kumi lakini wote walikuwa wa kike. Gikuyu hakupendezwa na jambo hili. Walipofikia umri wa kuolewa, Gikuyu alimwomba Ngai ili amjalie wavulana wa kuwaoa mabinti zake. Ili kumshawishi Mungu asikie dua yake, Gikuyu alitafuta mbuzi wa kiume wa rangi moja na kumchinja kama kafara chini ya mti wa mkuyu (*Mugumo*)

Mti huu ulikuwa na umuhimu mkubwa wa kidini miongoni mwa Wakikuyu. Mahali pale palitazamwa kama mahali patakatifu na chini ya kivuli chake ndipo palipotumika kama madhabahu.

Gikuyu alimtoa sadaka mbuzi ndume. Alimchinja na kumchoma. Aliamini kuwa harufu tamu ya nyama ingesafirishwa na upepo hadi kufikia kilele cha mlima Kirinyaga palipoaminika kuwa makao ya Muumba wake. Tendo hili la kumtolea Mungu sadaka chini ya mti wa '*mugumo*' lilikuja kuwa mashuhuri miongoni mwa jamii ya Wakikuyu hasa pale ambapo jamii hii ilikumbwa na janga lolote.

Gikuyu aliporejea pale chini ya mti wa mugumo kama alivyoagizwa na Muumba wake, alikuta mabarobaro kumi. Waliandamana na mabarobaro hawa hadi kwake na akawaoza binti zake. Kuanzia wakati huu jamii hii ilianza kufuata mfumo wa itikadi ya kukeni.

Majina ya mabinti hawa yalikuja kutambulisha mbari za jamii ya Wakikuyu. Mbari hizi ni kama zifuatazo-:

MZAZI	MBARI (MUHIRIGA)
1. Wanjiku	Agachiku
2. Wangari	Angari (aithekahuno)
3. Wambura	Ambura (ethaga)
4. Wamuyu	Aichakamuyu
5. Wairimu	Airimu (agathigia)
6. Wanjeri	Achera
7. Wamboi	Amboi
8. Wangui	Angui (aithiegeni)
9. Wanjiru	Anjiru
10. Wangeci	Angechi (aitherandu)

La kutatanisha ni kuwa mbari za jamii ya Wakikuyu zinajulikana kuwa tisa. Sababu ya jambo hili ni kwamba ulikuwa mwiko kuhesabu viumbe vyenye uhai na haswa watu kwa kuhofia kuwa wangepatwa na mkosi wa aina fulani. Hii ndio maana mbari hizi hazitajwi kuwa kumi mbali 'tisa zilizojaa' (*kenda muiyuru*). Umuhimu wa mbari katika jamii ya Kikikuyu ni mkubwa mno. Hili ni jambo tunalolipata kutokana na methali ifuatayo-:

'Muhiriga ti muhirigo'

(Mbari si kama ukuta ambao unaweza kubomolewa kwa urahisi)

Methali hii inasisitiza ukweli kuwa mfumo wa kimbari ni mfumo unounganisha jamii hii.Mbari zilitumiwa kama kigezo cha kumpa utambulisho mwanajamii. Watu wa mbari moja walishirikiana katika shughuli nyingi hasa wakati wa hafla za tohara na ndoa. Ushirikiano huu uliimarisha mahusiano kati ya watu wa mbari moja na kwa hivyo ilikuwa muhali kwa mwanajamii kudai kuwa hana mbari.

Jamii ya Gikuyu na Mumbi iliongezeka na kusambaa kutoka eneo lao la asili.

Inasemekana kuwa jamii kama vile Wakamba na Wameru ni miongoni mwa Wakikuyu walioranda mbali na makazi yao ya asili. Hii ni kutokana na ukweli kuwa baadhi ya mila zao zinalandana na zile za Wakikuyu. Lugha yao vilevile inakaribiana na ile ya Wakikuyu.

Jamii ya Wakikuyu ilizingatia itikadi ya kukeni kwa muda fulani.Wanawake walikuwa na madaraka na mamlaka makubwa. Utawala wao uliwahini na kuwadhalilisha wanaume. Jamii hii iliongozwa na jagina Wangu wa Makeri. Baada ya kusongwa sana na uonevu wa wanawake, wanaume walipanga njama ya kutwaa utawala . Jambo hili hata hivyo halikuwa rahisi kwa sababu ala zote za vita zilikuwa chini ya ulinzi wa mwanamke. Njia mwafaka ya kutekeleza lengo hili ilikuwa kupanga njama ya mapinduzi ya amani.

Baada ya kukutana, walikubaliana kwamba kila mwanamume aliyekuwa na mke ampachike mimba. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa methali ya Kikuyu,

'Mundu muka wi ihu na wi kironda ni undu umwe'

(Mwanamke mwenye mimba na aliye na jeraha hawana tofauti)

Walifahamu kuwa katika hali hii mwanamke hataweza kupigana wala kutetea haki zake kwa dhati.

Kupitia kwa njama hii, mwanamume alifaulu kuyatwaa mamlaka na basi mfumo wa itikadi ya kukeni ukapigwa kumbo na itikadi ya kuumeni.

Visasili vya wakikuyu vimerejelewa na wasanii kama vile Ngugi wa Thiong'o (1970:70). Anasema:

> "Kabla ya Agu na Agu, mwanzo wa yote *Murungu* (Mungu)muumba aliumba Gikuyu na Mumbi, baba na mama wa jamii ya Agikuyu. Aliwafanya kusimama katika mlima mtakatifu, akawaonyesha arthi yote ile.

Hili ni dhihirisho kuwa visasili hivi viliaminiwa sana na wanajamii hawa.

4.2.1 Hitimisho

Katika sehemu hii mtafiti ameangalia asili ya Wakikuyu kulingana na visasili vyao. Amebainisha jinsi ambavyo itikadi ya kuumeni ilivyopenyeza katika jamii hii kupitia kwa asasi ya ndoa na jukumu la mwanamke la kuzaa.

4.3. Asili ya Wakikuyu kulingana na ithibati za kihistoria

Wakikuyu ni tapo moja la kundi la watu wajulikanao kama Wabantu wa mashariki. Kulingana na idhibati za kihistoria, Wakikuyu, Wakamba, Wamijikenda, Wadigo, Waduruma wa jamii zingine zinazohusiana zilighura kutoka eneo linaloaminika kuwa

Kusini mwa Congo. Waliteremka kusini mashariki wakipitia kusini mwa ziwa Victoria na kukalia maeneo ya milima ya Taita. Nadharia hii inakiri kuwa wengi walielekea upwa na kupanda hadi kusini mwa Somalia, sehemu ijulikanayo kama Shungwaya. Sehemu hii ilikuwa na rotuba na lishe ya mifugo wao. Palitokea vita baina ya Wabantu hawa na Wagalla kwa sababu ya malisho. Tukio hili liliwalazimisha Wabantu kuhama kati ya mwaka 1200-1600. Walitawanyika katika maeneo mbalimbali ya kati na upwa wa Afrika Mashariki.

Mababu wa Wakikuyu wanasemekana kutoka katika eneo la Meru linalomilikiwa na Tharaka na Igembe katika karne ya 16. Wengine wanadai kutoka Ithanga na Thigicu huko ukambani. Waliteremka na kukalia eneo la Sagana. Wengine walielekea kaskazini na kukalia maeneo ya Mathira na Mukurwe-ini katika nusu ya kwanza ya karne ya 18 . Kutoka hapa walisambaa katika maeneo ya Nyandarua, Kabete, Uthaya na Aguthi. Leo hii, Wakikuyu wanakalia maeneo ya Murang'a, Nyeri, Nyandarua na Kiambu.

4.3.1 Hitimisho

Katika jitihada za kuwafahamisha wasomaji kuhusu maeneo ya Kijeografia yanayokaliwa na Wakikuyu, mtafiti ameelezea kuhusu walikotoka Wakikuyu, jamii zinazohusiana na Wakikuyu pamoja na walivyosambaa katika jamhuri ya Kenya.

4.4 Hali ya kiuchumi ya jamii ya Wakikuyu

Jamii ya Wakikuyu ilijihusisha sana na ukulima. Jamii hii huitazama ardhi kama uti wa mgongo wa maisha yao. Arthi inakuwa kama kumbukumbu ya mababu wao ambao waliwapokeza arthi ile. Miongoni mwa jamii hii, mchanga huheshimiwa sana na kiapo cha kudumu ni kile ambacho kiliapwa kwa mchanga *'koirugo,'(* Kenyatta (1938:21). Kuna methali nyingi katika jamii ya Wakikuyu zinazorejelea shamba. Hii ni idhibati ya shughuli walizojihusisha nazo. Mfano ni methali ifuatayo-:

'Gicigo kia mugunda gitinyihaga'

(kipande cha shamba hata kiwe kidogo vipi kitakufaa)

Methali hii ina maana kuwa mwanajamii hapaswi kuhalalisha uzembe wake kwa kudai kuwa kipande alicho nacho ni kidogo.

Licha ya kiasi cha shamba alichokuwa nacho mwanajamii alipaswa kujibiidisha na kuhakikisha ya kwamba ameikimu jamii yake. Bidii kazini ilikuwa jambo lililoenziwa sana miongoni mwa Wakikuyu.

Mfumo wa ukulima ni ule wa kufyeka sehemu ya msitu kwa minajili ya kupanda chakula. Wanaume ndio waliohusika na ufyekaji ilhali kupanda na kupalilia kuliachiwa wanawake. Jambo hili linatudokezea kuwa ugawaji wa majukumu ni jambo lililoendelezwa na jamii hii. Isitoshe, hii ni amali ambayo inapitishwa na kurithishwa kupitia kwa ujamiishaji.

Wavulana walirithi kipande cha shamba kutoka kwa baba baada ya kutahiri. wasichana hawakuwa na haki yoyote ya kudai urithi wa shamba kutoka kwa baba zao. Baada ya kifo cha baba, mvulana wa kwanza alichukua hatamu ya kuiongoza familia ile. Alijulikana kama '*Muramati*'. Mwanamke hakuwa na haki ya kudai urithi kwa sababu kulingana na Wakikuyu, yeye ni mpita njia. Wao husisitiza ukweli huu kupitia kwa methali – *'Mundu muka ni mutuga kwene'*. Yaani mwanamke hufaidi watu wengine ila si jamaa yake. Kwa kuzingatia imani hii, mwanamke alinyimwa nafasi ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za utungaji sheria .

Maswala na kesi zote zilizohusiana na shamba zilitatuliwa na baraza la wazee. Mabaraza haya yalijumuisha wanaume waliokuwa na ujuzi wa maswala haya na kama anavyosema Kenyatta (1936), ingawa kulikuwa na kamati zilizoshugulikia mambo ya wanawake, kamati hizi zilikuwa zikiendeshwa na wanaume. Baadhi ya mimea iliyokuzwa na wanajamii hawa ilikuwa ni ndizi, mihogo, viazi vitamu, viazi vikuu na wimbi .

Kama nilivyotaja katika sehemu ya 1.1 fasihi simulizi huelezea mazingira na hali ya maisha ya jamii husika. Hii ndio maana baadhi ya methali kama ifuatayo huufunua uhalisia wa mambo yanayomzunguka mwanajamii.

'Gutiri nyoni njega mwerei-ini'

(Hakuna ndege mwaminifu mbele ya mtama)

Kutokana na methali hii, tunadhibitikiwa na ukweli kuwa Wakikuyu walijihusisha na ukulima wa nafaka kama vile mtama, wimbi na maharagwe.

Jamii hii pia ilijihusisha na ufugaji wa wanyama kama vile mbuzi na kondoo. Kila mwanajamii alifahamu jukumu lake.

Majukumu yalitolewa kwa mujibu wa uana, hadhi na umri. Wanaume walihitajika kujenga nyumba, kuwinda na kutunza mifugo ilhali wanawake walihitajika kukandika nyumba kwa kutumia udongo na kinyesi cha ng'ombe, kusuka na kufinyanga vyungu. Ufugaji wa nyuki pia ni jambo lililozingatiwa kwani pombe iliyotumika wakati wa hafla mbalimbali ilitengenezwa kwa asali, miwa na aina maalum ya matunda ya mti uliojulikana kama *'muratina'*.

Ukweli kuhusu ugawaji huu wa majukumu unasisitizwa na methali kama-:

'muka wa mwathi ahingaga na kuguru etereire kigurumuki acoke'

(Mke wa msasi hapati usingizi hadi pale ambapo mumewe atarejea kutoka usasini)

Inabainika wazi kutokana na methali hii kuwa usasi uliendelezwa wakati wa usiku. Sababu kuu ni kuwa wanyama wengi hulala wakati wa mchana na kutafuta chakula wakati wa usiku. Kwa mujibu wa uana, wazo linalopitishwa na methali hii ni kuwa wanawake hawakuruhusiwa kwenda usasini. Hii ni kwa sababu wanajamii hawa waliamini kuwa kulikuwa na hatari nyingi kule hasa za kukutana na wanyama wanaotisha kama vile simba na nyoka. Jambo hili linasisitiza ukweli kuwa wanajamii hawa walimlinda mwanamke kutokana na hatari mbalimbali. Mwanamke anasawiriwa hapa kama mtu mwoga ambaye hawezi kupata usingizi hadi pale ambapo mumewe atarejea.

Uhunzi uliendelezwa kwa njia hii-: Vipande vidogo vya chuma vilikusanywa kutoka kwa changarawe iliyotoka kwenye kingo maalum za mito. Vipande hivi vilichemshwa kwa makaa yaliyotokana na miti fulani na migomba ya ndizi iliyokauka. Makaa haya yaliwekwa kwenye tanuu . Kabla ya kuyeyushwa vipande hivi, maombi maalum yalitolewa ili kuwafukuzilia mbali mapepo ambao wanaweza kuzusha balaa. Chuma kilichopatikana kilitumika kutengenezea mikuki na mishale ya kujikinga pamoja na visu vya kuchinjia na kutahiria kama methali ifuatayo inavyokiri,

'Kahiu getainwo na rweji'

(Kisu na kifaa cha kunyolea ni ndugu)

Usukaji ulifanywa wakati wa ziada na wanawake. Vifaa vilivyopatikana kutokana na usukaji huu ni kama '*kiondo*' (kikapu), '*getaruru'(*ungo*)* na '*gititi*'(pakacha).

Vifaa hivi vilitumiwa kuwekea nafaka. Ushonaji wa mavazi kwa kutumia ngozi za wanyama ulifanywa. Wanawake walivalia vipande vitatu vya nguo. Vipande hivi ni: ' *nguo ya ngoro'* iliyofunika kifua cha mwnamke , '*Muthuru'* iliyofanana kama rinda na '*mwengu*' iliyofunika sehemu ya mbele kuanzia kiunoni.

Wanaume walivalia vazi lililojulikana kama '*githii*' na '*githere*' iliyovaliwa wakati wa tamasha.

Biashara ilifanywa kwa kubadilishana vitu. Hii ni kabla ya ujio wa sarafu. Thamani ya kitu ilikadiriwa kwa kutumia mbuzi na kondoo. Ibainike kuwa wanyama hawa walitekeleza jukumu kubwa katika maisha ya wanajamii hawa. Mbuzi walitumika kulipia mahari ili hali kondoo walitumika katika matambiko na shughuli za kidini.

4.4.1 Hitimisho

Nyanja ya kiuchumi ndiyo nyanja inayodhihirisha tofauti ya kimajukumu kwa uwazi zaidi kati ya wanawake na wanaume. Wanaume walitengewa majukumu yaliyohitaji nguvu nyingi na yaliyokuwa hatari kama uwindaji. Ni dhahiri kuwa kutokana na haya, mwanamke alilindwa kutokana na madhara ya wanyama hatari. Hata hivyo mwanamke hakuruhusiwa kumiliki mali kama vile mifugo na shamba. Kazi walizojihusisha nazo wanaume kama uhunzi na usasi zilipewa umuhimu mkubwa kinyume na kazi za wanawake.

4.5 Maisha ya kisiasa ya Wakikuyu

Wakikuyu huzingatia itikadi ya kuumeni. Mamlaka na madaraka yote ya kuendesha jamii hii yalikuwa chini ya baraza la wazee. Wazee hawa walikuwa wazee wenye umri wa zaidi ya miaka hamsini. Utawala ulipokezanwa kutoka kizazi kimonja hadi kingine. Kulikuwa na vizazi viwili- *Mwangi* na *Maina* waliojulikana kwa jina lingine kama *Irungu*. Watoto wa kizazi cha *Mwangi* walijulikana kama *Maina* nao wa kizazi cha *Maina* waliitwa *Mwangi.* Kizazi kimoja kiliongoza kwa miaka 30 - 40 kisha usukani ukachukuliwa na kizazi kinachofuatia.

Uongozi ulikuwa umegawanyika katika ngazi. Katika ngazi ya chini kabisa kulikuwa halmashauri ya jamii (*ndundu ya mucii*). Kiongozi wa halmashauri hii ni mzazi wa kiume aliyetazamwa na familia yake kama kichwa cha boma lile.

Daraja ya pili ilikuwa halmashauri ya kijiji (*kiama gia itura*) Hii ilijumuisha wakuu wa familia kadhaa pale kijijini. Aliyekuwa na umri wa juu zaidi ndiye aliyeongoza halmashauri ile.

Daraja ya tatu ilikuwa halmashauri ya eneo (*kiama kia rugongo*). Hii ilijumuisha wanachama kutoka vijiji tofauti tofauti. Waliongozwa na aliye kuwa na umri wa juu zaidi na aliyeonekana kuwa na hekima zaidi (*muciiri).*

Daraja la juu zaidi lilijumuisha wanachama kutoka halimashauri ya eneo.

Kulikuwa pia na baraza la vijana wa umri wa makamo (*njama ya ita*) ambao jukumu lao kubwa lilikuwa ni kulinda jamii. Hawa walikuwa na umri kati ya 20-40.Makundi haya ya mabaraza ya wazee yaliendeleza umoja miongoni mwa wanajamii. Yalikuwa na majukumu ya kuamua kesi mbalimbali zilizohusu watu binafsi na jamii nzima kwa jumla.Umuhimu wake ulisisitizwa na methali kama-:

'Nyumba itari ndundu ihuragwo na njuguma imwe'

(Watu wasio na mabaraza ya kuwaunganisha hutawanyika kwa haraka)

Madaraka katika mabaraza haya yalitegemea ujuzi na juhudi za mhusika. Hakuna nafasi yoyote ya uongozi iliyopatikana kupitia kurithi. Wanabaraza hawa walikuwa na mamlaka ya kumtimua yeyote ambaye tabia zake zilikiuka mbeko zilizoongoza makundi haya . Kila kiongozi au mshiriki alipaswa kujali maslahi ya jamii pana ya Wakikuyu. Hakukuwa na majumba maalum ya kufanyia kesi na maamuzi. Kesi zilifanywa kwenye maeneo wazi chini ya mti iwapo zilihusisha kundi kubwa la watu. Zilizohusisha familia zilifanyiwa kwenye nyumba ya mzazi wa kiume iliyojulikana kama *'thingira'.*

4.5.1 Hitimisho

Maisha ya mwanajamii wa Kikikuyu yaliongozwa na msingi wa sheria zilizopitishwa kwao kupitia kwa mafunzo yaliyotolewa katika hatua mbalimbali za kukua. Utungaji wa sheria hizi na utoaji wa hukumu kwa walioasi ulitekelezwa na zile halmashauri nne za jamii ya Wakikuyu. Halmashauri hizi ziliundwa na wanaume. Wanawake walihusishwa kwa nadra sana.

4.6 Maisha ya kijamii

Maisha ya Mkikuyu hayakuwa na maana yakitenganishwa na matendo na maisha ya wanajamii wenzake. Hoja hii inasisitizwa na ukweli kuwa ilikuwa muhali kwa mwanajamii hasa mtoto kumwita mwanajamii mwenzake kwa jina. Njia iliyokubalika ya kuwataja watu hawa ilikuwa kuwahusisha na watoto wao au jamaa zao. Wao huitana baba fulani, mama fulani au nyanya wa fulani. Watoto na vijana ndio walioitwa kwa majina yao. Shughuli zote zilizoendelezwa katika jamii hii zilifanywa kwa ushirikiano wa kila mwanajamii. Mtoto alipozaliwa na kukua hadi kufikia utu uzima alipitia hatua mbalimbali ambazo zilisaidia kumuelimisha kuhusu kushirikiana na watu wengine. Kabla ya kuamua kufanya lolote, mwanajamii angetafuta ushauri kutoka kwa jamaa yake au rafiki wake wa karibu. Hali hii hupigiwa methali kuwa

'Ugi wa mundu umwe ndurimaga'

(Werevu wa mtu mmoja hauwezi ukakamilisha kazi yote ya shamba)

Methali hii ilitumiwa kuwaonya wale ambao walijiona werevu kuwa werevu wao una mipaka. Walitahadharishwa kuwa huenda wakahitaji msaada wa wanajamii wenzao wakati mmoja. Ikumbukwe kuwa Wakikuyu walitumia methali kupitisha amali mbalimbali za jamii yao.

Kulingana na Akivaga na Odaga (1982 :116), maadili na mafunzo ya kijamii huhifadhiwa na kupitishwa na fasihi simulizi. Methali nyingine iliyotumiwa kusisitiza umuhimu wa mahusiano ya kijamii ni kama vile-:

'Rurira rutithambagio rui'

(Uhusiano wa watu wa jamii moja hauwezi ukaoshewa mtoni)

Ushirikiano kati ya watu wa jamii moja hudhihirika waziwazi kupitia kwa hatua mbalimbali anazopitia mwanajamii. Hatua hizi huwa kama kaida na anayekiuka kaida hizi hutengwa na kuonekana kama muasi. Tabia za kila Mkikuyu huongozwa na mila na desturi zilizowekwa na ambazo zinazingatiwa kama katiba ya kuwaongoza wanajamii katika mahusiano yao ya kila siku. Hatua hizi zitasaidia kupambanua na kudhihirisha mtazamo wa wanajamii hawa kuhusu uana, jambo ambalo litashadidishwa na methali zilizochambuliwa. Katika sehemu ifuatayo, tutaeleza sherehe zinazoambatanishwa na kila hatua ya maisha ya Mkikuyu.

4.6.1. Kuzaliwa kwa mtoto

Mwanamke alipofikisha wakati wa kujifungua, mkunga aliitwa. Walishirikiana na wanawake wengine kumhundumia mwenye uchungu. Iwapo mtoto aliyezaliwa ni wa kiume, wanawake hawa walipiga vigelegele vitano (*ngemi ithano cia kahii*) kama ishara kuwa ni mvulana. Babake mtoto alienda shambani na kukata miwa tano. Maji matamu ya muwa yalimiminwa mdomoni mwa mtoto huyo kama ishara ya mwanzo mwema. Iwapo mtoto aliyezaliwa ni wa kike, tendo lilelile lingerudiwa lakini wakati huu vigelegele vilikuwa vinne na miwa vilevile. Tofauti kati ya vigelgele vilivyopigiwa mtoto wa kiume na yule wa kike ni dhihirisho la mtazamo wa wanajamii hawa kuhusu tofauti ya kiuana. Mtoto wa kiume alithaminiwa zaidi ya yule wa kike, hii ndiyo sababu ya kuwa na nderemo na vigelegele vingi yule wa kiume alipozaliwa. Isitoshe mwanamke aliyejaliwa watoto wa kike peke yao alibekuliwa kwa kuitwa '*nyina wa irigu*'. '*Irigu*' ni dhana inayotumiwa kuwarejelea kimadharao kurejelea wasichana ambao hawajatahiri.

Mwanamume aliyejaliwa watoto wa kiume pekee alipata shinikizo la kuoa mke mwingine atakayempatia watoto wa kiume. Ni bayana kuwa kwa kuzingatia mkabala huu, mwanamke alitazamwa kama kiwanda cha kumtengenezea mwanamume warithi (*aramati*). Haiba ya mwanamke ilipimwa kwa mizani ya kizazi chake. Hali hii inakinzana na ukweli wa kisayansi unaoonyesha kuwa mbegu za mwanamume ndizo zinazoamua uana wa mtoto. Utaratibu huu wa kumthamini mvulana kuliko msichana unakubalika kama inavyodhihirika kutokana na methali ifuatayo-:

Kahii ni ithigi ria mucii.

Mvulana ni ngao ya boma.

Methali hii inabainisha kuwa majukumu aliyotekeleza mvulana yalipewa umuhimu mkubwa. Ulinzi kwa jamii ni mojawapo ya majukumu haya.

Mtoto wa kwanza wa kiume hupewa jina la babu yake wa upande wa baba. Ikiwa ni msichana alipewa jina la nyanya yake wa upande wa baba, wa pili angepewa jina la kaka yake baba ikiwa ni wa kiume na dada yake baba iwapo ni wa jinsia ya kike. Wanaofuata hutajwa kutoka upande wa mama. Ingawa jambo hili lilichukuliwa kama kawaida ya maisha, jambo moja linalojitokeza wazi ni kuwa upande wa mwanamume ulitajwa kwanza.

Jambo hili linaonyesha kuwa kulikuwa na mapendeleo ya upande wa kuumeni. Ifahamike kuwa utoaji wa majina katika jamii ya Wakikuyu ulichukuliwa kama jambo la maana sana. Mtoto alipopewa jina la mwanajamii, ilimaanisha kuwa mwanajamii huyo ataendelea kukumbukwa kwa muda mrefu. Wakikuyu waliyaona maisha kama ni mseleko. Kifo hakikuwa mwisho mbali mwanzo wa maisha mapya ambayo yanajitokeza kupitia kwa watoto wanaozaliwa.

Mtoto akiwa mchanga alitegemea maziwa ya mamake. Baada ya miezi mitatu, mtoto alianza kulishwa ndizi zilizotafunwa pamoja na uji wa mtama.

Mtoto huyu alifungwa kwa ngozi kuanzia shingoni kwenda chini. Mafunzo ya kwanza kuhusu utamanduni wa jamii yake yalipitishwa kwa watoto kupitia kwa bembelezi. Hata ingawa katika kiwango hiki mtoto alikuwa mchanga sana kiasi cha kutoweza kuelewa yaliyopitishwa kupitia kwa nyimbo hizo, wanajamii hawa waliamini kuwa zingekuwa na athari fulani katika maisha ya mtoto. Nyimbo hizi zilisheheni maudhui kadhaa kulingana na uana na umri wa mtoto. Watoto wa kiume walihimizwa walale kwani wakati wao wa kuchunga na kuwinda bado haujafika. Wale wa kike nao walielezwa kuwa wakati wao wa kupika na kulea watoto bado haujawadia.

Hali hii inaenda sambamba na maoni ya Khasiani na Njiro (1993:33) wanaposema:

> "Katika jamii inayozingatia ubabeume, wanawake na wanaume wanajamiishwa kukubali nafasi yake, iwe duni au tukufu. Wake kwa waume waliitia hali hii mawazoni mwao. Wanaume wanahimizwa kuwa na ushari, uwazi, uhuru na ushindani ilhali wanawake hufunzwa kuwa watulivu, wategemezi, wasio na uwazi na watiifu"

Ni dhahiri kwamba ujamiishaji huu ulioanza wakati huu wa uchanga ulimwelekeza mwanajamii katika njia ambayo inatarajiwa na jamii, njia iliyokuwa imeainishwa kulingana na uana.

Watoto walithaminiwa kwani walikuwa ishara ya uhai wa jamii na bima ya siku za usoni. Watoto hasa wa kiume walithaminiwa hata zaidi kwani wangekuwa warithi wa mali ya baba yao. Mapendeleo haya ya kiuana huelezwa kupitia kwa methali kama-:

'Kahii kogi ta ithe kabaritaga ta migwi.'

Mvulana mwerevu kama baba yake hupeperuka kama mshale.

Tunachokipata hapa ni kuwa mzazi wa kiume anapatiwa sifa ya werevu. Si ajabu kuwa watoto watundu walihusishwa na mama yao. Mama aliyepata watoto wa kike peke yao alitafutiwa mke mwenza atakayempatia mume yule mrithi. Kinachodhihirika hapa ni kuwa wanawake walitumiwa kama vyombo vya kuendeleza kizazi.

Kulingana na Murote (2005), Mwanamke katika jamii ya Wakikuyu alikuwa na majukumu matatu muhimu. Majukumu haya ni; kufanya kazi shambani ili kuipatia familia yake riziki, kutosheleza mahitaji ya kimwili ya mume wake, kuzaa watoto hasa watoto wa kiume watakaoendeleza ukoo.

Jukumu la kuwalea watoto lilikuwa la mama. Hata hivyo jamii nzima ilishiriki katika kuwaadabisha. Watoto wa kike kuanzia miaka mitano walimsaidia mama yao kutekeleza kazi za nyumbani.

Wale wa kiume walimsaidia baba yao kuchunga pamoja na kutekeleza kazi zingine zilizotengewa wanaume. Baada ya shughuli za mchana kutwa ,watoto hao walikutanika jioni kwa nyanya yao au babu yao kutambiwa hadithi, kutegewa vitendawili na hata kufunzwa nyimbo.Vikao hivi vilitumiwa na wanajamii kama shule ya kuwafunzia wanajamii maswala yanayohusu jamii yao. Wasichana walifunzwa kuhusu jinsi ya kupika, ususi, kutunza watoto na kazi zingine za nyumbani ilhali wavulana walifunzwa kuhusu ufugaji, ukulima , uhunzi, usasi na uchongaji. Ni bayana kuwa kazi walizotengewa wanawake zilinuiwa kuwafunga nyumbani na hivyo kukosa nafasi ya kushirikiana na wanawake wenzao. Nyimbo na hadithi hizi zilishamirisha tofauti iliyopo kati ya wake na waume. Majagina wa hadithi walipewa majina ya wanaume ili hali wanawake walipewa majina ya wake wenza wenye wivu na waliojaribu kuwasumu watoto wa wenzao. Jambo hili lilimshushia hadhi mwanamke na lilinuiwa kukomelea wazo kuwa uwezo wa mwanamke ni pungufu. Katika kusisitiza haya, Wakikuyu walitumia methali:

Mwaki wa mucii uthegeagwo ni mutumia.

Moto wa boma hupekechwa na mwanamke.

Wazo linalowasilishwa kwetu ni kuwa mwanamke anapaswa kukaa jikoni na kubakia huko. Taasubi hii ya kiume ilikolezwa katika tafakuri za watoto kiasi cha kuwafanya waamini kuwa wanawake wanapaswa kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume.

Wakati wa kipindi hiki, watoto walifunzwa mambo mengi kama miiko na itikadi za jamii yao. Katika jamii ya Wakikuyu, wavulana waliokuwa na kati ya miaka kumi na minane hadi arobaini walipewa jukumu la kuilinda jamii. Kutokana na jukumu hili watoto wa kiume walithaminiwa sana kwani walionekana kama wanachama wa kudumu wa mbari yao. Wasichana baada ya kuolewa walijiunga na mbari zingine na kwa hivyo kuendeleza ukoo wa mbari hizo.

Hatua ifuatayo ilitumiwa kama daraja la kuwavusha wanajamii kutoka utotoni hadi utu uzima. Hatua hii ni ya tohara na ilitumiwa kuwatayarisha wanajamii kuchukua majukumu yao kama wanajamii halisi.

4.6.1.1 Hitimisho

Kuzaliwa ni hatua ya mwanzo ya maisha ya mwanajamii. Mambo yalioendelezwa wakati huu na yanayoonyesha tofauti ya kiuana ni:-

1. Mvulana alipozaliwa alipigiwa vigelegele vitano ilhali msichsna alipigiwa vigelegele vinne.
2. Baada ya kuzaliwa mtoto wa kiume alikatiwa miwa mitano na kumiminiwa maji matamu ya miwa hii mdomoni. Mtoto wa kike alikatiwa miwa minne.
3. Mwanamke aliyezaa watoto wa kike peke yao alibenzwa kwa kuitwa mama wa wasichana wasiotahiriwa bado (Nyina wa irigu). Mwanamume hakupewa jina kama hili la kuikejeli hali yake licha ya ukweli wa kisayansi kuwa ndiye anayeamua uana wa mtoto. Badala yake alihimizwa kuoa mke mwingine atakayempatia mrithi.

4.6.2 Shughuli za tohara

Wakati wa tohara ulikuwa wakati wa kukumbushwa kuhusu kaida zilizotawala jamii na pia wakati wa kukaza fundo lililofunganisha jamii. Uwezo wa kustahimili uchungu ulikuwa jaribio tosha la kumweka mhusika makali na kumshujaisha kuyakabili maisha .

Nyimbo zilizoimbwa wakati wa kipindi hiki zilitumiwa kupitisha maadili ya kijamii na hivyo kuwaelimisha na kuwahamasisha vijana kuhusu yanayoenziwa na jamii yao. Jambo hili linaafikiana na anayoyasema Chesaina (1991:6) anaposema kuwa tohara ilisaidia kuinadhifisha jamii kutokana na visa vya utovu wa adabu na kuweka usalama. Katika jamii ya Wakikuyu, tohara ilisaidia kushamirisha uhusiano miongoni mwa watahiriwa.

Wakikuyu husisitiza ukweli huu kupitia kwa methali-:

'Rika na nyumba itiumagwo'

(Ukoo na rika ni mambo mawili yasiyokimbilika)

Kama asemavyo Kenyatta (1978 :133), katika Jamii ya Wakikuyu, tohara ilikuwa ishara muhimu kama ilivyokuwa miongoni mwa Wayahudi. Tukio hili lina umuhimu wa Kidini, kijamii na kielimu kwa wanajamii hawa.

Tohara ya wasichana na wavulana ilikuwa asasi muhimu miongoni mwa Wakikuyu. Ingawa tohara ya wasichana ilipigwa vita sana na wamishionari, kitendo kile kilikuwa na dhima kubwa katika jamii husika. Ni kupitia kwa tohara ambapo mwanajamii alizamishwa kabisa katika mila na utamaduni wa jamii yake. Kutahiriwa kwa wavulana na kupashwa tohara kwa wasichana lilikuwa ni jambo la lazima miongoni mwa Wakikuyu. Wavulana ambao hawajatahiriwa bado walirejelewa kimadharau kama ' *ihii'* nao wasichana waliitwa *'irigu'*. Mvulana asiyepitia hatua hii hata awe mzee vipi hakupewa heshima. Hangeshirikishwa katika halmashauri yoyote kati ya zile nne zilizotajwa katika sura zilizotangulia. Si ajabu kuwa umuhimu wa hatua hii unapigiwa methali kuwa,

Kurua ni kwara itara.

Kutahiri ni kutayarisha dari.

Yaani kutahiri ni kama kuandaa sehemu ya dari ambayo hutumiwa kuhifadhia kuni. Jazanda hii inatumiwa na wanajamii hawa kurejelea majukumu ambayo mwanajamii anayatekeleza baada ya tohara. Kipindi hiki kilikuwa cha kuwafunza vijana kuhusu matarajio ya jamii yao na pia kuwaainishia majukumu kwa mujibu wa uana.

Kulingana na Kinuthia (2005), wasichana walifunzwa jinsi ya kuwatumikia waume wao watakapoolewa nao wavulana walifunzwa kuhusu kutamalaki na kuilinda jamii dhidi ya uvamizi. Mafunzo haya yalimtayarisha mwanamke kuchukua nafasi ya mtumishi naye mwanamume kuchukua nafasi ya ubwana. Hali hii inazungumziwa na Oduyoye (1988 :4) anaposema;

> "Katika jamii za Kiafrika, wanawake wanachukuliwa kama watu wa hadhi ya chini. Wanachukuliwa na kutumiwa na wanaume kama mali ya kibinafsi; wanadhulumiwa, kutumikishwa na kubekuliwa"

Utumishi wa mwanamke hata hivyo haudaiwi kwa nguvu. Mfumo wa ujamiishaji hutekeleza wajibu mkubwa wa kuhakikisha ya kwamba mwanamke anaikubali hali hii bila manung'uniko. Hatua hizi za maisha kama tohara zilitumika kama skrubu za kukazia sheria za jamii.

Ilikuwa mwiko pia kwa msichana Mkikuyu asiyetahiriwa kuolewa au kushiriki katika tendo la ngono na mwanamume. Iwapo jambo hili lingetokea ingawa lilikuwa nadra, mwanamume aliyehusika alifanyiwa matambiko *'gutahikwo migiro'*. Madharau haya yanabainishwa na methali ifuatayo:

> *'Ihii citithiaga uthoni'*.
> (Wavulana ambao hawajatahiriwa hawashirikishwi wakati wa kuwatembelea wakwe).

Tohara ya wasichana ilidhaniwa kuwa ingewapunguzia nyege na hivyo kuwaepusha na vitendo vya usherati. Dhana hii iliwanyima wanawake nafasi ya kufurahia tendo la ndoa. Wanajamii hawa walifahamu kuwa tohara ya wasichana ilikuwa na athari ya kuwapunguzia nyege lakini hili halikushughulikiwa ipasavyo. Imani ya Wakikuyu inashabihiana na ya Mtume Paulo. Anawaambia Wakorintho hivi:

> Mke hana amri juu ya mwili wake, bali mumewe....(1 kor 7:4)

Haya yalikuwa maonevu kwa mwanamke. Mbali na hili, tohara ilitazamwa kama mfumo wa kumfunzia mtahiriwa kaida, sheria, mila na utamaduni wa jamii yake. Ni baada ya tohara ambapo mtu alifunzwa mambo haya na pia kuruhusiwa kufanya mambo ambayo awali hangeshiriki.

Tohara pia ilifanya jamii kushirikiana kwani ulikuwa wakati wa jamii kuja pamoja na kusherehekea. Nyimbo zilizoimbwa wakati huu zilisheheni mafunzo yaliyowatayarisha vijana kuchukua majukumu kulingana na uana wao. Vijana wa kiume walichochewa kuwa wajasiri ilhali wale wa kike waliulizwa kuwa watiifu kwa waume zao na kuwa na bidii kazini. Watu waliotahiri pamoja walirejelewa kama wa rika moja *(riika)*. Jina la rika lilitokana na hali iliyokuweko. Waliotahiri wakati wa majilio ya wazungu wangeitwa *'rika ria nyakeru'* rika la mweupe.

Jambo hili lilisaidia kuweka kumbukumbu ya matukio yaliyoipitikia jamii.

Hivyo tohara ilikuwa na umuhimu mkubwa miongoni mwa wanajamii hawa.
Majuma mawili kabla ya tohara watakaotahiriwa walilishwa kwa chakula kulichodhaniwa kuwa na lishe bora. Hii hi kwa sababu wangepoteza damu wakati wa shughuli hii. Wasichana walishauriwa na ngariba wao kuhusu matarajio ya wanajamii wakati wa tohara. Pia aliwasaili wasichana ili kujua kama kuna yeyote ambaye ana hedhi au aliyevunja ubikira. Iwapo yupo, ilibidi afanyiwe utakaso ' *gutahikio*'. Siku nne kabla ya siku ya tohara, watahiriwa walikusanyika katika nyumba moja. Jamaa yote na watahiriwa pamoja na marafiki na wanakijiji walijumuika kwa tamasha zilizoendelea usiku kucha. Pombe maalum iloyotengenezwa kwa miwa ilinywewa. Wote waliokuja kwa sherehe hizi walihitajika kukesha usiku kucha huku wakiimba na kucheza. Sherehe hii iliitwa *'kuraria Murungu'*. Ilinuiwa kuwafukuzilia mbali mapepo na kuwasihi wale wazuri wawakinge watahiriwa kutokana na janga au hatari yoyote. Kutokana na hili, hakuna mtahiriwa yeyote aliyetakikana kulala, kwani kitendo cha kulala kilionekana kama mwaliko wa mukosi.

Asubuhi iliyofuatia watahiriwa wa kiume walipakwa mchanga mweupe kwenye paji la uso wao. Mchanga huu ulitolewa mlima Kirinyaga – makao ya Muumba wao.
Wale wa kike walipakwa mafuta yaliyotolewa kwa mmea ujulikanao kama *'Mbariki'*.
Walitumia maneno ya kuwabarikisha hao watakaotahiri. Maneno haya ni:-

"Ciana irogia thayu . Thaai , thathaiya Ngai thaai
Ciana irogia thayu. Thai thathaiya Ngai thaai."

" Watoto wapate amani. Tumsihi Mungu (Ngai) atupe amani
Watoto wapate amani. Tumsihi Mungu (Ngai) atupe amani"

Baada ya sala hii watahiriwa wanarejea nyumbani kila mmoja kwao. Siku moja kabla ya sherehe yenyewe wasichana walinyolewa nywele na kukwatuliwa kwa shanga walizopewa kama zawadi na wanawake jamaa zao. Msichana alivikwa pia njuga kwenye mguu wake wa kulia na kisha alisindikizwa na waimbaji katika msafara kuelekea mahali watakapokaa baada ya tohara.

Nyimbo nyingi ziliimbwa njiani na walipofikia mahali watakapokaa kila mmoja wa watakaotahiriwa anakuwa ameandamana na kundi kubwa la watu.

Wakati wa alasiri siku hiyo kunakuwa na nyimbo, nderemo na vifijo mahali ambapo watakaotahiriwa watakaa. Mahali penyewe panatakaswa kwanza na mganga (*Mundu mugo*) na kisha panarashiwa pombe ili kupata radhi za mababu.

Jioni panawekwa mgomba wa ndizi kwenye lango pamoja na miwa, iliyoundwa kwa umbo la tao. Tao hili linanakshiwa kwa aina mbalimbali za matawi yanayodhaniwa kuwa na nguvu fulani. Kutokana na jambo hili, watu waovu hawangedhubutu kwenda mahali pale baada ya kukamilika kwa ujenzi wa tao. Pembe inapopulizwa, wavulana wanapiga foleni na kisha wanakimbia kuelekea mahali palipo na mti wa '*Mugumo*', palipoaminiwa kuwa mahali patakatifu. Watu wanakuwa tayari wamekusanyika pale chini ya mkuyu ili kuona ni mvulana yupi atakayefika pale akiwa wa kwanza. Atakayefika wa kwanza alishangiliwa na kufanywa kiongozi wa kundi lile. Tukio hili liliwazungukia vijana wa kiume. Wale wa kike hawakupewa nafasi ya kuonyesha uwezo wao.

Baada ya kufika kwenye shina la mti huu (*Mugumo)* ,wavulana hawa waliupanda na kukata matawi yake. Matawi yanayoanguka chini wakati wa shughuli hii yanakusanywa na wasichana wanaojitayarisha kupashwa tohara. Majani haya baadaye hutumiwa kutengeneza matandiko yao baada ya kutahiriwa. Tendo la kupanda juu ya mkuyu lilikuwa na umuhimu wa kidini miongoni mwa Wakikuyu. Ikumbukwe kuwa shughuli zote za kidini zilifanyiwa chini ya mti huu. Kuupanda mti huu kulikuwa kama ishara ya kuonyesha kuwa vijana hawa wa kiume walimkaribia Muumba wao zaidi kimadaraka. Vijana wa kike waliobakia chini ya mkuyu walifanya kazi ya kunadhifisha mazingira yale kwa kuokota yale matawi yaliyoangushwa na wavulana. Tendo hili la kuokota matawi haya liliashiria kazi ya kunadhifisha nyumba iliyokuwa imetengewa wasichana. Walihitajika kuweka mazingira yao yakiwa masafi.

Matawi ya mkuyu waliyookota wasichana yalitumiwa kutengenezea malazi ya watahiriwa. Wanawake kwa mujibu huu walikuwa na jukumu la kuwatayarishia waume wao na watoto mahali pa kulala.

Baada ya hii, wavulana walikula yamini kuwa watailinda jamii yao na kutunza siri zote za jamii. Wasichana kwa upande wao hawakula kiapo cha aina yoyote. Baada ya hii walirejea kwenye boma ambapo watakaa baada ya tohara. Sherehe za kuachana ziliendelezwa na kisha kila mmoja alielekea nyumbani kwao.

Jogoo wa kwanza alipowika, wasichana walilishwa kwa chakula maalum. Kisha walivuliwa nguo na kubakia na mkufu ambao watautoa kama zawadi kwa ngariba wao. Hii ni ishara kuwa watabakia marafiki wa kufa kuzikana. Kisha msichana alisindikizwa hadi mahali ambapo alipaswa kukutana na wenzake.

Baadaye waliongozwa hadi kwenye mto uliotengwa kwa shughuli hii. Tukio hili lilifanyika alfajiri na mapema wakati ambapo maji ni baridi mno. Waliangusha matawi majini kama ishara ya kufukuzilia mbali tabia za kitoto. Jambo hili lilifanywa mapema ili kuzifanya sehemu za uzazi kufa ganzi na hivyo kupunguza uchungu zitakapokatwa. Watahiriwa walijitosa majini. Kina cha mto ule kilipaswa kuwawezesha vijana wale kufunikwa na maji hadi kiunoni

Baada ya dakika kama thelathini, watakaotahiriwa waliambatana kuelekea mahali ambapo tohara itafanyika. Wakati huu nyimbo, zilizoimbwa ni nyimbo za huzuni. Walielekea sehemu iliyotengwa rasmi kwa jambo hili (*Iteeri).* Hapa ngozi ya ng'ombe ilitandikwa na juu yake matawi ya mti maalum (*mathakwa*) kupangwa. Wasichana waliketi juu ya matawi haya huku wakizungukwa na wanawake jamaa zao. Hakuna mwanamme yeyote aliyepaswa kukaribia eneo hili. Wasichana hawa walirashiwa maji baridi kwenye sehemu zao za siri. Gwiji wa tohara alijongea huku akiwa amevalia mavazi ya kutisha yenye rangi za kuogofya. Aliwatahirisha wale wasichana mmoja baada ya mwingine. Baadaye, waliotahiriwa walirushiwa maziwa yaliyochanganywa na dawa yenye uwezo wa kuponya haraka. Wasichana hawa ambao walijulikana sasa kama '*irui'* (watahiriwa) walielekezwa kukaa katika nyumba maalum. Waliamrishwa kulala sakafuni walikotayarishiwa. Kitanda kilikuwa majani maalum yenye harufu nzuri (*mirerecwa*). Majani haya yalinuiwa kuwafukuzilia mbali nzi na kuondoa harufu mbaya.

Kwa muda wa siku nne hakuna mgeni anayeruhusiwa kuwaona watahiriwa hawa. Nyumba walimokaa ililindwa ili kuhakikisha kuwa hakuna mtu hasa mwenye jicho baya alikaribia mahali pale.

Tohara ya wavulana iliendelezwa kwa njia ile ile lakini katika mahali tofauti na ile ya wasichana. Jamaa za watahiriwa walileta chakula cha kila aina mahali wanapokaa kwa miezi minne, watahiriwa hawa hawakuruhusiwa kufanya kazi ila kutembelea jamaa zao.

Tohara katika jamii ya Wakikuyu ni jambo lililopewa umuhimu mkubwa. Hafla hii ilitarajiwa kwa hamu na wanajamii wote kwa sababu ulikuwa ni wakati wa kula na kunywa na vilevile kuunganika pamoja. Wanajamii waliokuwa wamekosana walipata fursa ya kujumuika pamoja na kusameheana. Jambo hili liliendeleza umoja wa jamii. Kwa watahiriwa, huu ulikuwa ni wakati wa maana sana kwani ungewafungulia milango ya siri za jamii hasa kuhusu unyumba na utawala. Si ajabu wanasema kuwa mtu hajuti kwa sababu ya kutahiri, kuoa na kulipa deni.

'Kurua, kugurana na kuriha thiri gutiiriragwo'

4.6.2.1 Hitimisho

Shughuli zilizozungukia tukio la tohara zilimulika zaidi majukumu yatakayotekelezwa na vijana. Wavulana walitayarishwa kuchukua hatamu ya uongozi ilhali wasichana walitayarishwa kuwa watumishi. Mambo yanayoibua tofauti baina ya uana ni kama vile:-

1. Kuimba nyimbo zilizosheheni ujumbe kuwa wavulana wanapaswa kuwa hodari kwani wana jukumu la kuilinda jamii yao dhidi ya uvamizi (waliitwa ua *(fence)* la boma). Hii ilizatitisha imani kuwa majukumu ya vavulana ni muhimu kuliko ya wasichana.
2. Kuukwea mkuyu kwa wavulana ilikuwa ishara kuwa sasa wamepata madaraka zaidi. Wasichana walibakia katika shina la mkuyu na kuokota matawi yaliyoangushwa na wavulana- ishara ya utumishi.
3. Wavulana walikuwa na majina maalum ya marika yaliyotambulisha hatua hii. Wasichana kwa upande wao walichukuliwa kuwa hawana rika kama methali ifuatayo inavyokiri*: Aka matiri rika* (wanawake hawana rika).
4. Mojawapo wa umuhimu wa tohara kwa wanawake ulikuwa ni kuwapunguzia nyege na hivyo kuwafanya waaminifu. Jambo hili halikushughulikiwa katika upande wa wavulana.

5. Baada ya tohara wavulana walipewa sehemu ya urithi wao. Wasichana kwa upande wao hawakupewa na wala hawakuwa na haki ya kudai chochote.

4.6.3. Ada za ndoa

Ndoa katika jamii ya Wakikuyu ni jambo lililothaminiwa sana. Ubasha, ukapera na useja ni mambo yasiyojulikana katika janibu hizo. Kila mmoja wa wanajamii alikuwa na hamu ya kuendeleza mbari yake kupititia kwa ndoa. Ndoa ilikuwa jambo lililohusisha jamii nzima na wala halikuwa jambo la mtu binafsi. Ukamilifu wa ndoa ulipatikana kupitia kupata watoto. Utasa na ugumba ni jambo lililotazamwa kama laana kutoka kwa mababu au dhihirisho la hasira za miungu. Ingawa ukosefu wa watoto unaweza kusababishwa na mwanamume, lawama zote zilirundikiziwa mwanamke. Ukweli huu unaibuliwa na methali ifuatayo-:

'Mutumia utari mwana angikura ndonaga wa kumutahira mai'

(Mwanamke asiye na mtoto hukosa mtu wa kumtekea maji anapozeeka)

Utekaji maji na kazi zingine za nyumbani zilitekelezwa na watoto wa kike. Methali hii ilitumiwa kuonyesha kuwa mahusiano kati ya msichana wa kike na mama yake ni wa karibu sana. Mtoto wa kike anakuwa mwenzi wa mamake katika shuguli zote za pale nyumbani.

Katika jamii ya Wakikuyu, mvulana au msichana alikuwa na uhuru wa kuchagua mchumba. Hata hivyo uamuzi wa mwisho ulikuwa wa wazazi. Mvulana alipovutiwa na msichana fulani, aliwafunulia siri hii marafiki zake wa karibu. Marafiki hawa hujihusisha na kuchunguza kama msichana yule ana bidii kazini. Mara kwa mara walijificha karibu na mahali msichana yule anapofanya kazi ili kuchunguza kama kweli ana bidii. Ni bayana kuwa ufaafu wa msichana ulichunguzwa zaidi ya ule wa mvulana. Wakikuyu waliamini kuwa msichana, ambaye alitarajiwa kuwa mama baada ya muda mfupi, alikuwa na uwezo wa kuathiri mkondo wa maisha ya watoto wake. Wazo hili lilipitishwa kupitia kwa methali:

'Kana ka ngari gakunyaga ta nyina.'

Mwana wa fisi hukwaruza kama mama yake.

Iliaminika kuwa mwanamke muovu huweza kupalilia tabia hii kwa wanawe kupitia kwa malezi. Tofauti ya kiuana ilidhihirika kupitia kwa uchunguzi aliofanyiwa msichana kabla ya kuolewa.

Vijana marafiki wa mchumba wakiridhika kuwa msichana yule anafaa, walitembea nyumbani kwao ili kumfahamisha kuhusu nia ya mmoja wao. Iwapo wangekubalika, mvulana alirudi nyumbani na kuwafahamisha wazazi wake ambao walitayarisha pombe ambayo ilipelekwa kwa wazazi wa msichana.

Walipofika kwa wazazi wa msichana, walikaribishwa na kupewa chakula. Baada ya kusema lengo lao, msichana aliitwa na kuulizwa ampe baba yake pombe kwa kutumia pembe maalum (*ruhia*) iliyotengewa kazi ile. Kabla ya kumpa babake pombe ile, alipaswa kuonja kidogo kama ishara ya kukubali kwake kuposwa na waliokuja. Baada ya kuwa na uhakika kuwa dua yao imekubalika, wazazi wa mvulana walirejea kwao na kuanza kukusanya mbuzi na kondoo ambao watapelekwa kwa wazazi wa msichana kama sehemu ya kwanza ya malipo ya mahari (*ruracio).*

Katika jamii ya Wakikuyu, malipo ya mahari huendelea kwa kipindi kizima cha uhai wa wahusika. Hata wazazi wa mvulana wakiwa wana uwezo wa kulipa mahari yale kwa wakati mmoja, ni mwiko kufanya hivyo. Jambo hili huonekana kama dua mbaya . Malipo ya kwanza hufuatiwa na malipo zaidi hadi kufikia kiwango ambacho kitawaruhusu kupewa msichana.

Ulipaji huu wa mahari ulitazamwa kama ni kununua yule msichana. Imani hii ilimfanya mvulana kuwa na mamlaka makubwa juu ya mkewe. Familia ya akina mvulana pia ilimtarajia msichana huyu kuitumikia na kufuata maadili yake. Dhuluma kwa mwanamke ziliendelea kudhihirika katika mahusiano ya ngono. Mwanamume alichukulia kuwa ana haki ya kushirikiana kimapenzi na mke wake wakati wowote apendao bila kuwekewa vikwazo vyovyote. Maadamu amemlipia mahari, basi ana haki ya kumtendea apendavyo. Wachege (1992) akitafiti kuhusu mahusiano haya miongoni mwa Wakuria anasema kuwa mwanamume wa Kikuria alikuwa na uhuru wa kumtoa mkewe akidhi mahitaji ya kimwili ya rafiki yake. Ingawa jambo hili lilikubalika katika jamii husika, lililo dhahiri ni kuwa mwanamke alichukuliwa kama mali ya mwanamume na kwa hivyo alikuwa na uhuru wa kumtoa ili awafurahishe marafiki.

Baada ya kutoa kiasi cha mahari kilichoulizwa na wazazi wa msichana, siku inatengwa ambapo kunatayarishwa sherehe kubwa inayoitwa *'guthenya ngoma'*. Marafiki na jamaa wa pande zote mbili wanaalikwa kwa sherehe hii. Wanakuja na chakula na vinywaji vingi vitakavyotumika katika sherehe. Kwa kawaida kulichinjwa kondoo sita au watano na ndama ikiwa wazazi wa msichana ni tajiri. Figo za kondoo aliyechinjwa kwanza zilipewa msichana anayeposwa. Ifahamike kuwa miongoni mwa Wakikuyu, kuna baadhi ya sehemu za nyama ambazo mwanamke hakuruhusiwa kuzila. Sehemu hizi ni kama vile kifua cha mbuzi au kondoo. Sehemu hizi zinajulikana kuwa tamu na kwa hivyo mwanamke hakustahili kula sehemu tamu. Isitoshe, mwanamke hakuruhusiwa kumchinja mnyama. Iwapo alikuwa mjane na hakuwa na mwana wa kiume aliyetahiriwa, alibidika kumtafuta mwanamume ili amchinjie. Jambo hili linamsawiri mwanamke kama binadamu aliyepungukiwa. Si ajabu Wakikuyu hupigia jambo hili kijembe kwa kudai kuwa,

'Mutumia ndaturaga mutwe.'

Mwanamke hapaswi kupasua kichwa cha mnyama aliyechinjwa.

Iwapo msichana hajabadili nia alizila figo zile na hivyo tamasha ziliendelea. Upande wa mvulana unatoa zawadi nyingi kwa wazazi wa msichana. Zawadi hizi zinafidia vifaa nyote alivyokuwa amepoteza msichana.

Baada ya siku hii, msichana anakuwa sasa ameposwa rasmi na mvulana yule. Sherehe hizi zinakuwa kama ilani kwa ukoo mzima na majirani kuwa msichana yule sasa alikuwa mali ya wenyewe.

Baada ya kutayarisha nyumba na vifaa vilivyohitajika, mvulana aliwafahamisha marafiki zake kuwa yuko tayari kuoa. Marafiki wale walimfahamisha mamake mvulana kuwa kuanzia siku ile hadi baada ya siku nane kutakuwa na mgeni. Hii ilikuwa kumtahadharisha kuwa anapaswa kupika chakula kingi kwani walaji wameongezeka.

Marafiki wale walichunguza alipokuwa msichana na baada ya kuhakikisha alipokuwa, walimnyemelea na kumwinua kimzegamzega huku wakimwelekeza nyumbani kwa akina mvulana. Msichana kwa upande wake alijifanya kutokubali na hivyo hupiga mayowe na kulia kwa shaki. Mayowe na kilio hiki kinafahamiwa na wanajamii na hakuna aliyeshugulika nacho isipokuwa wanawake wachache waliojifanya kuwa anataka kumwokoa.

Kitendo hiki cha kumnyakua msichana kilishusha hadhi ya msichana. Kilimfanya mwanamke kuonekana kama aliyeolewa bila hiari. Pia kilialika dhana kuwa mwanamke wakati wote lazima alazimishwe kufanya jambo. Dhana hii ilijipenyeza katika asasi ya ndoa na kumfanya mwanamke kuwa kama kifaa kilichoelekezwa kwa shemeretua.

Pindi aolewapo, mwanamke alihitajika kumtii mumewe kwa heri na shari. Wazo hili linashadidishwa na methali isemayo;

> *'Mumbia arume omburaguo na njuguma.'*
>
> Anayewakatalia jambo wanaume huadhibiwa kwa fimbo.

Thairu (1975:47) akilizungumzia jambo hili anasema;

> "Jamii nyingi za Kiafrika humpa mwanamke nafasi duni kwa kuzingizia kuwa ni majaaliwa au ni utamaduni au ni kwa sababu ya maumbile"

Katika jamii ya Wakikuyu msichana baada ya kunyakuliwa, alipelekwa hadi nyumbani mwa mchumba wake. Marafiki zake na jamaa walimtembelea huku wakimletea zawadi. Hakuruhusiwa kuonekana ovyo ovyo na watu.Alibakia katika nyumba kwa muda wa siku nane. Aliapotoka ndani ya nyumba, kwa mfano alipoenda kuoga mtoni, alipaswa kujifunika uso na kusindikizwa na marafiki zake ambao wanatumika kama kizibo.
Swala la ubikira lilikuwa la muhimu sana miongoni mwa Wakikuyu. Baada ya mvulana kuletewa mchumba wake, usiku ule wa kwanza, shangaziye mvulana alitandika ngozi maalum kitandani mwa maharusi hawa. Ngozi ile iliwekwa kwa makusudio ya kudhibitisha ubikira wa msichana. Siku ya pili baada ya kujamiana, ngozi ile ilipaswa kuwa na damu. Hiki ni kiashiria cha ubikira kwani ni ishara kuwa kizinda cha msichana hakikuwa kimetobolewa. Mvulana alipaswa kumpelekea shangaziye ngozi ile ili akague. Ikiwa msichana alikuwa bikira, aliheshimiwa sana na wazaziwe walipewa zawadi nyingi.Kupitia kwa kitendo hiki, tunaona ya kuwa thamani ya msichana ilipimwa kwa mizani ya ubikira. Nafasi yake kama binadamu wa kuheshimiwa ilidhalilika au kuimarika baada ya hali ya ubikira wake kujulikana. Mvulana kwa upande wake hakuwa na kigezo chochote cha kupimia thamani yake kulingana na ubikira. Kwa sababu ya maumbile yake, haingebainika kama yeye ni bikira au la. Jamii ilimpendelea mwanamume kwa vile hali yake katika jamii haikutegemea ubikira. Mvulana angetambulika kuwa hakuwa bikira pale tu alipomtunga msichana mimba.

Iwapo hili lingetokea, mvulana yule alihitajika kumuoa yule msichana. Jambo hili lilipigiwa kijembe kupitia kwa methali kuwa;

'Wahira ihu wi kironda niwe ukagura'

Ukimpachika mimba msichana aliye na kidonda ndiye utakayeoa.

Ikiwa hakutaka kumuoa, mvulana alihitajika kumlipia kiasi fulani cha mbuzi kutegemea makubaliano yake na wazee wa msichana.

Mvulana na msichana katika jamii hii walidadisiwa na shangazi ili kupata ukweli kuhusu uwezo wao wa kuendeleza uzazi. Iwapo kulikuwa na kasoro, jambo hilo liliripotiwa kwa halmashauri ya wazee. Wazee hawa walilizumgumzia na kisha kutoa uamuzi ufaao kabla ya siku nane kuisha.

Ikiwa mambo ni shwari siku ya tisa ilikuwa siku ya sherehe maalum za kumkubali rasmi msichana kama mmoja wa ukoo wa mvulana. Kondoo mnono alichinjwa na mafuta yake yalipakwa msichana yule. Kuanzia siku ile msichana yule alishiriki kikamilifu katika shughuli zote za ukoo ule. Lilikuwa ni jambo la kawaida kwa wanaume kuoa zaidi ya mke mmoja hasa ikiwa familia ile ilikuwa tajiri. Mara nyingi pendekezo la kuoa wake wengine lilitoka kwa mke wa kwanza ambaye alipewa heshima kubwa. Wake walioolewa baadaye walipaswa kumtumikia yule wa kwanza *(nyakiambi)* na kusikiliza wakati wote ushauri wake.

Jamii ya Wakikuyu haikumruhusu mwanamke kuolewa na wanaume zaidi ya mmoja. Aliyekaidi jambo hili alitazamwa kama malaya na alitengwa na wanajamii wengine. Jambo hili linadhihirisha uhuru aliokuwa nao mwanamume akilinganishwa na mwanamke.

Hata hivyo kulikuwa na uhasama na ushidani baina ya wake wenza, jambo ambalo liliibuliwa kupitia kwa methali kama;

'Aka eri ni nyungu igiri cia urogi'

Wake wawili ni kama vyungu viwili vya urogi.

Swala la uke wenza ni swala ambalo limeshughulisha kalamu za waandishi wengi wa Kiafrika. Chacha (1982) katika tamthilia yake ya *Mke Mwenza* anatuenyesha athari ya uke wenza kupitia kwa mhusika Boke na Robi.

Boke anapoelezwa na mumewe Chahe kuwa ananuia kumwoa Robi, Boke anapanga njama ya kumuua kwa kumsumu. Wivu wa kumwona Robi akiwa na Chahe unamwelekeza kutenda kitendo hiki cha unyama.

Ingawa uke wenza ni jambo lililokubalika katika jamii nyingi za Kiafrika, asasi hii husababisha wivu, mafarakano na hata mapigano miongoni mwa wahusika. Jambo hili huenda lisionekane waziwazi lakini hubakia katika mioyo ya wake wenza hawa na kusambaa hadi kwa watoto wao.

Swala la talaka lilikuwa nadra sana miongoni mwa Wakikuyu. Kabla ya kufikia hatua hii ya kutalikiana, kisababisho kilijadiliwa kwa mapana na marefu na wazee. Mambo ambayo yangehalalisha talaka ni kama vile uchawi, wizi wa kiwango cha juu na usinzi kwa upande wa mwanamke. Ibainike kuwa mwanamume mzinzi hakupewa talaka na mkewe. Jamii ililiangalia jambo hili kama la kawaida. Angeliadhibiwa tu kama alizini na mke wa mwanamume mwingine. Kuwepo kwa watoto hata hivyo kulikuwa kikwazo kwa talaka. Hii ni kwa sababu watoto walichukuliwa kama kiunganishi cha daima kati ya watu hao wawili na mbari kwa jumla.

Iwapo hapakuwa na budi kuruhusu talaka, watoto walitunzwa na mama yao. Mume alikuwa na idhini ya kudai nusu ya mahari aliyotoa na ikiwa yule mwanamke aliolewa na mume mwingine mahari yote yangerejeshwa. Hii ni kwa sababu mahari yalitazamwa kama gundi iliyoshikanisha na kudumisha uhusiano baina ya familia na koo mbili hizi.

4.6.3.1 Hitimisho

Ni bayana kuwa asasi ya ndoa ni kipengele mojawapo cha kijamii kilichompa mwanamke nafasi duni. Kutokana na tuliyoyaeleza katika sehemu hii, mambo yanayolenga kauli hii ni kama vile:-

1. Kuviziwa na kunyakuliwa kimzegamzega kwa msichana wakati wa kuolewa.
2. Kuongezwa au kupunguzwa kwa kiasi cha mahari anacholipiwa msichana kulingana na hali yake kwa mujibu wa ubikira.
3. Kuchukuliwa kama mojawapo wa mali ya mwanamume baada ya kulipiwa mahari.
4. Kutalikiwa anapopatikana na kosa la uzinzi ilhali mwanamume anayepatikana na kosa kama hili haadhibiwi.

5. Kuruhusiwa kwa mwanamume kuwa na wake wengi huku mwanamke akinyimwa uhuru ule.

4.6.4. Swala la kifo

Mzee yeyote, licha ya umri hakuruhusiwa kushiriki katika baraza la wazee ikiwa hakuwa na watoto waliotahiriwa. Weledi wa maswala ya kijamii na hadhi ya mwanajamii vilikuwa vigezo muhimu katika kumkweza mtu ngazi za uongozi.

Iwapo kulitokea sintofahamu yoyote au mafarakano katika jamii, mwanamume kama kichwa cha nyumba alikuwa na wajibu wa kutafuta suluhisho. Ni baada ya kukosa suluhisho ndipo angeliwaendea wazee na mabaraza mengine ya kiwango cha juu.

Kadiri umri wa mwanajamii ulivyozidi kukua ndivyo alivyozidi kuheshimiwa kwani alionekana kama aliyebusarika kadiri ya mpito wa wakati.

Wanaume waliokuwa na mali wangeweza kuoa mke mmoja baada ya mwingine hadi kifo kiwatenganishe na tabia hii. Walipozeeka kiasi cha kutoweza kufanya kazi walitunzwa na wake zao, watoto wao, wajukuu na hata vitukuu. Wanawake kwa upande wao walitunzwa na wakazawana wao pamoja na wajukuu na vitukuu. Hata hivyo lilikuwa jukumu la wanajamii wote kuwatunza wazee waliokuwa miongoni mwao. Kazi ya pekee ya wazee wa umri huu ilikuwa kubarizi chini ya mti wakati wa mchana huku wengine wakivuta ugoro. Waliohitaji ushauri waliwatembelea. Walitazamwa na jamii kama raslimali kubwa kwa sababu umri huo ulishabihishwa na hekima na busara nyingi. Wao wanashabihishwa na jiwe kongwe ambalo halifunikwi na maji,

(*Kahiga gakuru gatiagararagwo ni maii*).

Methali hii ina maana kuwa busara ya wazee hawa ni kubwa sana na imani yao haiwezi ikatikisika.

Wakati wa jioni walikuwa na wajibu wa kuwatongolea hadithi na kuwashauri watoto ambao walikuwa bado kutahiriwa. Kupitia kwa elimu hii watoto waliweza kufunzwa kuhusu historia ya jamii yao, mila, desturi na kaida zilizoitawala jamii yao. Kungesikika vicheko vya watoto kutoka makao ya wazee hawa (*thingira).*

Mzee alipoona kuwa anachungulia kaburi, angewaita watoto wake wa kiume hasa aliyekuwa mkubwa. Aliwaalika pia wazee wengine ili kuwa mashahidi wa wosia wake.

Wakati wa kipindi hiki familia yake na hata jamii nzima walikuwa waangalifu sana ili wasije wakawaudhi kwa lolote. Iliaminika kuwa hasira za mzee kama huyu zingeleta balaa kubwa na laana kwa wahusika na hata jamii nzima kwa jumla. Mara nyingi methali ifuatayo ilitumika kuwatahadharisha wanajamii dhidi ya kuwaudhi wazee:

'Kirumi kia mudu wi muoyo ni kiuru gukira mudu mukuu'

(Laana ya mtu aliye hai ni hatari zaidi kuliko ya aliyekufa)

Walipokutanika katika nyumba yake *(thingira)* aliwaeleza kwa utaratibu mipaka ya shamba lake. Aligawia watoto wa kiume kila mmoja kipande chake. Aligawa hata na mifugo kwa njia ile. Mkewe hakuwa na fursa ya kutoa maoni yake kuhusu urithi na wala watoto wa kike hawakuwa na haki ya kudai chochote. Jambo hili linadhihirisha nafasi duni aliyopewa mwanamke katika jamii hii. Baada ya kutahiri, vijana wa kiume walichukua nafasi ya pili kwa uongozi katika familia. Baba yao alipokwenda safari ya mbali wavulana hawa hasa yule wa kwanza alichukua nafasi ya baba yao.Wanawake walijaribu sana kudumisha uhusiano mwema kati yao na watoto wao wa kiume kwa sababu walikuwa na uwezo wa kumshawishi babao na kuathiri uamuzi wake.Wazazi wengi wa kike waliwasiliana na waume zao kupitia kwa watoto wao.

Hadhi ya mwanamke katika jamii hii inazungumziwa na Kabira (1994 :79) anposema kuwa wanawake wangefanya biashara na Wakamba na Wamaasai kwa kubadilisha nafaka kwa mbuzi au kondoo, lakini walipofika nyumbani hawakuwa na budi kuikabidhi mifugo ile kwa waume zao au watoto wa kiume iwapo walikuwa wajane.

Mtoto wa kwanza wa kiume alichukua hatamu ya kuongoza familia ile baadaa ya kifo cha babake.Wakikuyu waliamini kuwa hata baada ya kifo, roho ya aliyekufa ilibakia katika familia na hivyo kutozingatia ushauri wa aliyekufa kungealika adhabu kutoka kwa pepo wake.

Baada ya wosia ilikuwa kawaida kwa mzee kama huyu kufa siku chache baadaye. Ilikuwa muhali kwa mtu kufia nyumba. Waliamini kuwa mtu alipofia nyumba, nyumba na eneo lile litamilikiwa na mapepo ya kifo. Kuepukana na jambo hili, mtu alipoonekana kuwa mahututi aliondolewa nyumbani na kupelekwa kichakani. Alisubiriwa hadi afe na baada ya kufa mwili wake uliachwa pale. Mwili wake ulililiwa na wanyama. Yule ambaye hakuliwa alisemekana kuwa mchawi.

Ingawa watoto na watu wa umri wa makamo walifariki pia ,jambo hili lilichukuliwa kama laana, uchawi au hasira za miungu. Kifo cha wazee kilitazamwa kama ada tu ya maisha na kilitarajiwa.

Mtu aliyeua mwenzake alihitajika kulipa fidia kwa kutoa mbuzi mia moja ikiwa aliyeuliwa ni mwanamume na ikiwa ni mwanamke, muuaji alitoa mbuzi thelathini. Tofauti hii ya idadi ya mbuzi zinazotolewa kama malipo ni dhihirisho la thamani inayoambatanishwa na maisha ya mwanamume. Wanajamii hawa huendeleza ubaguzi huu kupitia kwa methali zinazomtukuza mwanamume. Utawasikia wakisema:

'Maitho ma arume ti ma mambo.'

Macho ya wanaume si ya '*mambo*'.

Mambo ni mdudu mdogo kama sisimizi aliye na macho madogo. Tashbihi hii inatumiwa na wanajamii hawa kumpa mwanamume uwezo mkubwa wa kuona na kutambua mambo akilinganishwa na mwanamke. Wakikuyu vile vile hunena kuwa ,

'Ugi wa arume utemaga ta ruhiu'

Werevu wa mwanamume hukata kama kisu

Itikadi ya kuumeni sawa na methali hizi nilizotaja husaidia kukoleza imani kuwa mwanamke ni duni akilinganishwa na mwanamume. Kasumba hii imezama kikiki katika mawazo ya wanajamii hawa kiasi cha kuwafanya waamini kuwa malipo yale yanapaswa kuwa vile.

4.6.4.1 Hitimisho

Kifo kama hatima ya maisha ya mwanajamii kiliibua mtazamo wa wanajamii kuhusu umilikaji mali. Mambo yafuatayo yaliyo na muegemeo wa kiuana yalitekelezwa :-

1 Mwanamume alipokaribia kufa aliwaita watoto wake wa kiume na kuwapa wosia. Wosia huu ulihusu jinsi ya kugawana mali baina yao. Mwanamke hakuwa na mengi ya kuwarithisha watoto wake kwani hakuruhusiwa kumiliki chochote zaidi ya mavazi yake na vyombo vyake vya nyumba.

2 Ni watoto wa kiume peke yao waliorithi mali ya babao baada ya kufa. Wale wa kike walitazamwa kama wageni katika familia zao.

3 Baada ya kifo cha mzazi wa kiume, mali aliyoacha ilikuwa chini ya ulinzi wa mwanawe wa kwanza wa kiume (*Muramati*). Mjane alihitajika kushauriana naye wakati wowote alipotaka kuitumia mali ile.

SURA YA TANO

TASWIRA YA MWANAMKE KATIKA METHALI

5.1 Utangulizi

Methali ni utanzu wa fasihi ambao hutumika sana katika mazungumzo ya kawaida ikilinganishwa na tanzu zingine kama vile vitendawili. Methali hupatikana katika jamii nyingi ulimwenguni na umuhimu wake katika mazungumzo ya kawaida haupuuziki. Wakikuyu wenyewe wanafahamu umuhimu wa methali kwani wenyewe husema;

'Ciunagwo rukomo, kimenyi akamenya ikiunwo.'

(Methali hutumiwa ili werevu waweze kung'amua yanayoendelea)

katika kusisitiza ukweli huu, Munene (1995 :48) anasema-:

> *" Thimo ni ndundiro cia kihoto ina ngarango nyingi thiini wacio na itari irathimurwo ndungihota kumenya ndeto cia cio. Thimo ni cia kuhoreria kana kuhe mundu irio cia meciria.Cie bata muno kwi Mugikuyu tondu nicio igina cia kugereka ngerekano cia Mugikuyu ndakae kwera maundu-ini make no arungiririe ta mugwi mugereke ni mwathi....Maundu maria mekagwo ni Mugikuyu ekaga emutongorie ni thimo nigetha athingate nuti ya ruriri rwa Agikuyu."*
>
> *(Tafsiri)*
>
> (Methali ni hazina ya ukweli. Zina mambo mengi ndanimwe na bila kufasiriwa huwezi kuzielewa. Methali hutumiwa kutuliza au kumpa mtu chakula cha fikra. Zina umuhimu mkubwa kwa Mkikuyu kwa sababu hutumika kama dira ya kumuelekeza ili asitetereke bali alenge ndipo kama mshale uliolengwa na msasi....Mambo anayotenda Mkikuyu hufanya kwa kuongozwa na methali ili afuate mila za jamii ya Kikuyu.)

Ukweli huu kuhusu methali umekubalika miongoni mwa jamii nyingi kama kauli zifuatazo kutoka maeneo mbalimbali ulimwenguni zinavyokiri. Mineke (1992)

1. Methali ni pambo la uzungumzi. Kauli hii inatoka nchi ya Iran.
2. Methali mia moja, ukweli mara mia (kutoka Uhispania)
3. Uzungumzi usio na methali ni kama chakula kisicho na chumvi. (kutoka Amharic Ethiopia).
4. Methali ni farasi wa usemi (kutoka Yoruba Nigeria).

Bali na kuwa mirathi ya kitamaduni, methali huwa kama kitambulisho kwa wanajamii kama ilivyo lugha na husaidia katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Ifahamike kuwa utamaduni wa jamii huchangia falsafa ya jamii hiyo na mtazamo wake wa maisha.

Methali huhusishwa na miktadha zinamotumika na hudhihirisha kaida na amali za jamii husika. Wanaanthropolojia hutoa kauli kuwa kujua methali za jamii husika ni kuijua jamii yenyewe (Mineke :1992).

Kwa kuzingatia kauli hii na madhumuni ya utafiti huu, mtafiti ameweza kubainisha taswira ya mwanamke inayoibuliwa na methali za Kikikuyu.

Katika sura hii, mtafiti ananukulu hoja na kuchanganua methali zilizotolewa na wazee wa rika la *Irungu* ili kupata picha halisi ya mwanamke kutokana na methali hizo.

Katika uchanganuzi wake, mtafiti atazingatia pendekezo la mpango wa uchanganuzi kama ulivyoelezwa katika sehemu ya 3.2.

Mfano ufuatao ni kielelezo cha jinsi na hatua alizozifuata mtafiti katika kuchanganua data yake.

Methali kwa Kikikuyu : '*Uhii ni umagwo no uka ndumagwo.*'

(Tafsiri)

Tafsiri kwa Kiswahili : Mvulana hubadilika anapotahiri lakini mwanamke hubakia vivyo jinsi alivyokuwa.

(a) Maudhui : Methali hii inawasilisha ujumbe kuwa mvulana anapopita daraja la tohara, anatazamwa kwa njia tofauti. Anapewa majukumu ambayo yanamkweza ngazi na pia anaruhusiwa kuoa na kumiliki mali. Mwanamke kwa upande wake hapati mamlaka wala mali. Mabadiliko anayoyapata yanakuwa madogo sana yakilinganishwa na ya mvulana.

(b) Nyanja : Nyanja ya maisha inayolengwa na methali hii ni ile ya umilikaji mali.

(c) Lugha : Methali hii imetumia lugha sahili lakini yenye kufumba ujumbe. Tukio muhimu (tohara) katika maisha ya mwanajamii wa Kikikuyu limetumiwa kama kiashiria cha mtazamo wa wanajamii kuhusu uana.

(d) Maana : Methali hii ina maana kuwa nafasi ya mwanamke haibadiliki licha ya mabadiliko ya kimwili anayoyapitia. Pindi atahiripo, mvulana anapewa sehemu ya urithi- ishara kuwa anaweza kumiliki mali.

Pia inaashiria uhuru wa kujiamulia mambo yake. Mwanamke kwa upande wake hana urithi na anabidika kutafuta ushauri kwa baba yake au kwa mume wake iwapo ameolewa.

(e) **Taswira** : Methali hii inasadifu yale maudhui ya kwanza. Mwanamke anapewa nafasi duni licha ya kuwa katika kiwango sawa na mwanamume. Hali yake haiboreshwi na hatua anazozipitia kama mwanamke, kinyume na ilivyo kwa mwanamume.

Methali zifuatazo zitachanganuliwa kwa mkabala wa maswala haya matano yaliyoangaziwa hapo juu. Kutokana na kigezo cha maudhui, uchanganuzi umedhihirisha ya kwamba methali zinazomsawiri mwanamke zimegawanyika katika matapo matano. Kuna methali zinazohusu mwanamke katika ndoa (5.2), zinazolenga malezi (5.3), zinazolenga kazi (5.4), zinazohusu utawala (5.5) na umilikaji mali (5.6). Kutokana na vigezo vya nyanja, lugha, maana na taswira, matokeo ya uchanganuzi yametolewa kwa maelezo ya kijumla katika kila methali.

5.2 Methali zinazolenga ndoa

5.2.1 Gutiri njamba ya mwera umwe

(Tafsiri)

Hakuna jimbi wa mtamba mmoja

Jimbi ni kuku wa kiume. Inatambulika kuwa kutokana na silika, jimbi mmoja hutumiwa kuzalisha mitamba wote waliokomaa katika boma. Tabia hii inadhihirika pia katika wanyama wengine kama mbuzi, kondoo na ng'ombe.

Methali hii huwalenga wanaume. Jimbi katika methali hii ametumika kijazanda kuwakilisha mwanamume. Hii ni kwa sababu katika jamii ya Wakikuyu, mwanamume amepewa uhuru wa kuwa na wake zaidi ya mmoja. Wanawake kwa upande wao hawakuwa na uhuru huu. Mwanamke aliyekaidi kaida hii alichukuliwa kama malaya. Wanajamii walimtenga na kumsengenya kiasi kwamba alikosa rafiki kwani hakuna mwanajamii yeyote angetaka kujiainisha naye. Mwanamume mwenye wake wengi alionekana kuwa na uwezo wa kudhibiti boma lake na kutawala wake hao.

Mwanamume alijua kuwa alikuwa na uhuru wa kuoa wake wengi apendavyo mradi awe na uwezo wa kuwalipia mahari. Methali hii ilitumiwa kumtuliza mke hasa wa kwanza *(Nyakiambi)* aliyekasirishwa na kitendo cha mumewe cha kuoa wake wengine. Kwa upande mwingine, methali hii ilitumiwa kuwachochea wanaume waliokuwa na mke mmoja ili kuwafanya kuoa wake zaidi. Wanaume waliokuwa na mashamba makubwa na mifugo wengi walikuwa na nafasi ya kuoa wake wengi kwa sababu wangeweza kugharimia mahari waliyoitishwa. Wake wengi waliweza kupalilia shamba la mume wao na hivyo kuzalisha chakula kingi.

Kazi walizozifanya wanawake hawa zilimsaidi mwanamme kukwea ngazi ya kiuchumi. Faida ya jasho la bibi zake ilimnufaisha mwanamume. Walichokipata wanawake kama fidia ya nguvu zao ni chakula kilichopatikana kutoka shambani na mavazi. Ongezeko la mali kwa upande wa mwanamume lilikuwa sababu tosha ya kumfanya mwanamume kufikiria kuoa wake zaidi, maadamu ataweza kuwalipia mahari. Kila bibi alihitajika kupika chakula na kumpelekea mumewe katika *'thingira'*-nyumba maalum aliyokaa mume huyo. Kadiri mume alivyokuwa na wake wengi ndivyo alivyoletewa chakula kingi. Baada ya kula na kusaza, mwanamme huyo aliwapa marafiki wake waliomtembelea au watoto wake wa kiume ambao hawajatahiri bado *(ihii)*

Wanawake wenyewe waliikubali hali hii. Sababu kuu ni kwamba walikuwa wametayarishwa kupitia kwa malezi kuwa jambo hili ni jema.

Kulingana na Kariuki (2005), wake wenza walisaidiana kufanya kazi nyakati za sherehe (*mambura*). Mmoja wao alipopata mtoto alihudumiwa na wale wake wengine mpaka atakapopata nguvu. Mwanamke alipopoteza maisha yake akiwa na mtoto mdogo, mtoto yule alichukuliwa na mke mwenzake. Alitunzwa vizuri na hata kunyonyeshwa naye. Yamkini ndio maana kuna methali kuwa -:

' *Muka umwe ni rigu wa gatema'*

(Mke mmoja ni kama tonge la mwisho la chakula cha mgonjwa anayeugua kipindupindu)

Methali hii inasisitiza hatari ya kuwa na mke mmoja. Mke huyu akiaga dunia familia ile itakumbwa na masaibu makubwa kwani ingawa jamii nzima itaomboleza pamoja nao, baadhi ya majukumu aliyotekeleza mke huyo yatakosa mtu wa kuyatekeleza.

Hii ndio maana mke mmoja anafananishwa na tonge la mwisho ambalo likishaliwa linamuacha mgonjwa bila matumaini ya kuishi. Jambo lingine tunalolipata kutokana na methali hii ni kwamba wanaume wengi walioa wake wengi kwa sababu ya kutaka kuongeza mali yao au kwa sababu ya kutimiza haja zao za mwili. Taswira tunayochorewa hapa ni ya mwanamke aliyenyimwa uhuru wa kuwa na waume wengi. Anastahili kuhimili uchungu wa kuwa na wake wenza huku mumewe akiruhusiwa kuoa wake wengi kadiri ya uwezo wake. Anayejikakamua na kuhusiana na wanume zaidi ya mmoja anatazamwa kama malaya.

5.2.2 Mumbia arume omburagwo na juguma

(Tafsiri)

Anayewakatalia jambo wanaume huadhibiwa kwa fimbo

Kuwakatalia jambo wanaume ni kutofuata mashauri na maagizo wanayotoa. Wazo kuwa mwanamume ndiye kichwa cha nyumba ni jambo lililokubalika katika jamii ya Wakikuyu. Kwa sababu hii baba au mume alistahili kutiiwa na familia yake. Mtu yeyote aliyekataa kumtii baba yake au mume wake aliadhibiwa vikali. Wakikuyu waliafiki jambo hili kwa msemo kuwa:

'Mundurume ni ngai ya keri'

Mwanamume ni mungu wa pili.

Jamii ya Wakikuyu ilimpa mwanamume nguvu zaidi akilinganishwa na mwanamke.

Hii ina maana kuwa jinsi binadamu anavyomhusudu Mungu, ndivyo ambavyo mwanamke anapaswa kumtii na kumheshimu mumewe. Mshabaha huu unaibua wazo kuwa kama vile ambavyo binadamu hawezi kumuuliza lolote au kumtetesha Mungu , ndivyo ambavyo mwanamke anapaswa kuhusiana na wanaume. Lugha iliyotumika katika methali hii ni sahili na ujumbe unajitokeza moja kwa moja.

Mwanamke hapaswi kumkatalia chochote mwanamume. Neno *'arume'* ni wingi wa neno *'mundurume'* lenye maana ya mwanamume.

Jambo hili lilimfanya mwanamke kuwa katika kitengo kimoja na watoto wanaohitajika kumtii mwanamume kama mkuu wa boma bila kuuliza swali. Kuuliza maswali kungemfanya mwanamke na watoto kustahili adhabu ambayo ilipaswa kumfunza adabu.

Simon de Beauvoir (1960) akizungumzia jambo hili alisema kuwa unyenyekevu wa wake kwa waume hauna chanzo chake katika hali ya kumwogopa tu mwanamume bali hutokana na jinsi mwanamume ametawala kwa muda mrefu. Ujadi huu anaouzungumzia Simon unajidhihirisha kupitia kwa vipengele vya fasihi kama vile methali, vitandawili na ngano ambazo zimepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kasumba ya kumpa mwanamke majukumu aliyotengewa na utamanduni katika jamii zinazotawaliwa na wanaume ni njia moja ya kumshushia hadhi. Mwanamke hufanya jitihada za kumbembeleza mumewe kwa kuwa mtiifu na mcheshi.

Akielezea kauli hii Ndege (1992) anatoa kauli kuwa jamii inayozingatia itikadi ya kuumeni humpa mwanamke hadhi duni . Yeye mwenyewe huikubali hali hii kwa sababu ya matayarisho aliyopokea anapojamiishwa. Radhi hii ya mwanamke inaifanya ndoa kuwa na amani.

Wakikuyu wanaruhusu tabia ya mwanamume ya kumuadhibu mkewe kwa kutumia methali kuwa;

Mundu murume ni wa karugi

Mwanamume hakawii kutenda jambo hasa kwa sababu ya kupandwa na mori.

Methali kama hii inanuiwa kumtia hofu mwanamke na hivyo kumfanya amtii na kumyenyekea mwanamume. Ni bayana kuwa wao huamini kuwa mwanamume anapokasirishwa ana haki ya kumtendea lolote mwanamke. Mwaura (2005) anaeleza masaibu waliyowakumba wanawake kwa kudai kuwa wengi wao walipigwa kwa kutumia kinga cha moto, ufito na hata upanga. Vita hivi wakati mwingine vilisababisha majeraha mabaya kwa mwanamke lakini jamii ilimtarajia kuvumilia.

Nafasi hii anayotengewa mwanamke na jamii inakaririwa na wosia wa Mwanakupona kwa binti yake anaposema-:

27. Enda naye kwa imani
Atakalo simkhini
We naye sikindaneni
Ukindani huumia

La kutatanisha ni kuwa ni wanawake wenyewe ambao wanaendeleza hali hii. Ifahamike kuwa wanawake katika jamii ya Wakikuyu hawakushirikishwa katika utungaji wa sheria na kwa hivyo hawakuwa na nafasi ya kupinga baadhi ya kaida hizi. Sheria ziliwekwa na wanaume waliokuwa katika zile halmashauri nne za jamii ya Wakikuyu. Hii ina maana kuwa hawakuwa na nafasi ya kuendeleza maslahi yao katika nyanja hii.

Kezilahabi (1971 :17) anatuchorea hali hii kupitia kwa mawaidha ya mhusika Regina kwa mwanawe Stella.

> "...ni lazima upige magoti kila mara ukimpatia babako kitu fulani."

Kutokana na mashauri haya ya Regina, ni bayana kuwa wanawake katika jamii yake sawa na ya Wakikuyu hawakuwa na uhuru wa kutenda wapendavyo. Walizingatia sheria zilizowekwa na wanaume na walihitajika kuzifuata bila kuuliza swali. Hapa tunasawiriwa mwanamke anayepaswa kutekeleza anayoulizwa na mumewe bila kuuliza swali.

Lake ni kutii mumewe na kumchukulia kama mungu. Mnyampala (1965:6) anaelezea umuhimu wa kuwa huru katika mishororo ifuatayo:

> "Ungalishwa vya mafuta
> na isiwepo kukiri
> bwana mkubwa kukwita
> na uso upate nuru
> mtu hakosi kujuta
> madhali hana uhuru
> hali ya nchi huru
> utumwa hauna heri"

5.2.3 Aka eri ni nyungu igiri cia urogi

(Tafsiri)

Wake wenza wanafananishwa na nyungu mbili za uchawi

Methali hii ilitumiwa kueleza hali ya uke wenza. Boma lililokuwa na wake wenza lilikuwa daima katika mizozo. Sababu ni kuwa wake hawa walioneana wivu, walisengenyana na hata kuwakataza watoto wao washirikiane.

Kulingana na Kariuki (2005), asili ya uke wenza ni kuwa katika jamii ya Wakikuyu laana na magonjwa mabaya yangepitishwa kutoka kwa mzazi hadi kwa mtoto. Mwanamume aliyeoa wake wengi aliamini kuwa hata kama baadhi ya wanawake walikuwa na laana au magonjwa mabaya, wale wake wengine wataendeleza ukoo wake.

Ingawa wazo hili ni jema, wanaume wengi walioa wake wengi kwa sababu ya uchu wa mwili au mali- jambo lililopelekea wake wenza kuwa na ushindani baina yao.

Ni kweli kuwa kuna baadhi yao walioshirikiana vizuri lakini si wengi. Sheria za mume wao ndizo mara nyingi zilizowaunganisha. Hata hivyo hakukukosa vita vilivyoendelezwa kichinichini.

Katika familia nyingi za aina hii, mwanamume alipendelea mke yule mdogo. Hii ndio maana Wakikuyu walikuwa na methali iliyosema kuwa kuna mke anayependwa na yule asiyependwa-'*Kwi ngatha na nyagacu'*

Hii ilikuwa sababu tosha ya kuleta utengano kati ya wake wenza.

Ugomvi ulikuwa bayana katika familia zilizokuwa na zaidi ya mke mmoja. Hii ndio sababu iliyopelekea kufananishwa kwa wake wawili na chungu cha uchawi.

Uchawi ni jambo lililodharauliwa sana miongoni mwa Wakikuyu. Hii ni kwa sababu waliojihusisha na uchawi walionekana kuwa na uwezo wa kudhuru wanajamii wanzao. Ifahamike kuwa kuna tofauti kati ya uchawi na uganga. Uganga ulitazamwa kama taaluma iliyotunukiwa mhusika na miungu kwa nia ya kuinusuru jamii na kuitakasa kutokana na mawaa. Uwezo huu ulirithiwa kutoka kwa baba hadi kwa mwana. Hili lilikuwa jambo la kuinufaisha jamii. Uchawi kwa upande mwingine ni jambo lililohusishwa na madhara. Alipopatikana, mchawi aliadhibiwa kwa kuwekwa kwenye mzinga wa nyuki na kubingirishwa kutoka kilele cha mlima hadi shinale. Tendo hili lilifanywa hadharani ili kuwatahadharisha walio na nia ya kuwa wachawi kuchelea tabia hii.

Kuhusishwa basi kwa wake wawili na uchawi ni jambo linalonuiwa kueleza hali ilivyokuwa katika familia husika. Hata hivyo Tashbihi hii inamuumbua mwanamke kwa kumsawiri kama anayeweza kudhuru. Kinaya ni kwamba, miongoni mwa Wakikuyu, uoaji wa wake wengi ni jambo lililokubalika na lililomkweza ngazi ya kijamii mwanamume husika. Fauka ya hayo mwanamke wa kwanza ndiye mara nyingi aliyependekeza kwa mumewe mke atakayeolewa. Haieleweki basi kwa nini wake wenza walitazamwa kama waliojaa ufidhuli.

Gachanja (1992 :1) anashikilia kauli hii anaposema:-

> "Ingawa Kenyatta anautazama uke wenza kama asasi muhimu ya kuheshimika, tanzu nyingi za fasihi (zikiwemo ngano, methali na vitendawili) huisawiri hali hii kuwa nyeti sana miongoni mwa Wakikuyu. Visa vingi vinavyosimuliwa vimejaa utesi usiokwisha, wivu na mizozo inayojaa katika familia ya ukewenza".

Masimulizi mengi yanaeleza maovu ambayo wake wenza wanatendeana wao kwa wao na hata kwa watoto wa wenzao. Taswira tunayoipata kutokana na methali hii ni ya wanawake wanaochukiana. Wanawake wanajishushia hadhi wenyewe kwa kukosa maelewano baina yao. Ingawa ilikuwa asasi maarufu, ngano za Kikuyu zimefunua maovu yake zaidi ya utanzu wowote ule wa fasihi yao.

5.2.4 Wahira ihu wi kironda niwe ukagura

(Tafsiri)

Ukimpachika mimba mwanamke aliye na ulemavu ndiye 'utakayenunua'

Wakati wa zamani watu walikuwa na tabia nzuri. Ingawa kulikuwa na visa vichache vya utovu wa nidhamu, asilimia kubwa ya vijana walikuwa wanasikiliza mawaidha ya wazazi wao. Vijana walionywa dhidi ya kujiingiza katika vitendo vya aibu kama mapenzi nje ya ndoa na utungaji mimba. Wale wachache waliofanya hivyo walitengwa na kudharauliwa. Msichana alipoolewa, wazazi wake walipikiwa pombe na wazazi wa mvulana. Pombe ile ilitiwa kinyesi cha mbuzi *(mbimbi)* ikiwa msichana alikuwa bikira. Ikiwa hakuwa bikira pombe ile ilitiwa jivu. Wazazi wa msichana aliyekuwa bikira walifurahi sana ilipobainika kuwa msichana wao alikuwa bikira. Hii ni kwa sababu walijua kuwa watapewa mahari kochokocho.

Msichana aliyekuwa na tabia mbaya alidharauliwa na wavulana waliojihusisha naye walionywa kwa kuelezwa methali hii.

Mvulana aliyempachika msichana mimba katika jamii ya Wakikuyu alipaswa kuchagua kati ya mambo mawili- kumuoa au kulipa kiasi fulani cha mali kitakachoamuliwa na jamaa ya msichana . Methali hii ilitumiwa kuwatahadharisha vijana dhidi ya kujiingiza kwenye mambo yanayoweza kuwaletea aibu. Katika kusisitiza adabu njema Wakikuyu hutumia methali hii:

'Guthinga gwakira gutonga.'

Uadilifu ni bora kuliko mali.

Wakikuyu waliwahimiza vijana kuwa waadilifu na waangalifu hasa wanapohusiana na watu wa uana tofauti. Ilikuwa fahari kubwa kwa msichana na wazazi wake alipoolewa akiwa angali bikira. Baada ya 'fungate' yao, mvulana alihitajika kurejeshea shangaziye ngozi maalum waliyoilalia ili ikaguliwe. Nia haswa ya ukaguzi huu ilikuwa kudhibitisha kama msichana alikuwa bikira. Huu hata hivyo ni uonevu wa kiuana kwani hakuna kiashiria chochote cha ubikira katika upande wa mvulana. Kama msichana hakuwa bikira basi angetahayarika peke yake. Ikiwa mvulana hakuwa bikira, aliyefahamu ni Jalali na mpenzi wake pekee. Ubikira wa wavulana haukusisitizwa sana kwa sababu thamani yao haikuathiriwa kinyume na alivyokuwa msichana. Mvulana aliyempachika msichana mimba angeamua kulipa kiasi cha mbuzi atakachoitishwa. Msichana kwa upande wake alibakia na madhila ya kumlea mwana wake. Hangeolewa kama mke wa kwanza kwa sababu kama wasemavyo Wakikuyu wenyewe, ng'ombe aliyezeeka hatamaniki-

'Iri gukura ndiri mwiroreri'.

Jamii ilimtenga na angeolewa tu kama mke wa pili au wa tatu. Ili kujiondolea balaa hii, vijana wale walikubaliana kuwa mpango ufanyike mapema. Hata hivyo ukweli ungedhihirika baadaye.

Mushkeli uliopo kwenye methali hii ni kuwa badala ya kutaja mvulana aliyehusika atamuoa (*hikia*) muathiriwa , methali inazungumzia kununua (*kugura)* msichana. Kisawe cha neno '*kugura*' ni kununua. Matumizi ya dhana hii ni dhihirisho kuwa mwanamke katika jamii hii anatazamwa na kuchukuliwa kama bidhaa ambayo inayoweza kuuzwa . Ifahamike kuwa thamani ya maisha ya mwanadamu haiwezi kukadirika. Hata anapolipwa ridhaa ile ni fidia tu wala si thamani kamili ya maisha ya binadamu. Wazo hili la kumbidhaaisha mwanamke laonekana kutanda katika jamii nyingi za Kiafrika. Methali ifuatayo ya kilingala inakiri ukweli huu.

Mineke (1992:10) anatupa mfano wa methali ya Kilingala inayosema kuwa mwanamke ni kama pande la arthi, kila mmoja anaweza kumkalia.

Mwanamke katika jamii hii akipata mtoto kabla ya kuolewa alibenzwa na kutengwa na jamii. Mume aliyemuoa alipewa mbuzi aliyejulikana kama mbuzi wa kusimamisha matiti.

Hii ni kwa sababu alionekana kama aliyemuokoa msichana yule na wazazi wake kutokana na fedheha. Mkabala unaochukuliwa na jamii hii ni kuwa msichana ndiye mkosaji. Ingawa kosa la msichana ni sawa na lile la mvulana, lawama zote zinarundikiziwa msichana. Mahari yanayolipiwa msichana yule yalimwendea baba yake. Baada ya kulipiwa mahari, mwanamke alikuwa mali ya mumewe. Katika methali hii, tumepewa picha ya mwanamke ambaye thamani yake inakadiriwa kupitia kwa kiasi cha mahari anayolipiwa. Isitoshe, mahari ile inamnufaisha baba yake- mwanamume. Kulingana na utaratibu unaozingatiwa na jamii hii, msichana hawezi akaoa mume mbali mume ndiye anayeoa.

5.2.5 Muiritu mwega ahitukagira thome wa ngia.

(Tafsiri)

Mvulana masikini hawezi akampata msichana mrembo

Msichana mzuri ni yule aliyekuwa na bidii na urembo. Wakati wa kale watu hawakuwa wakioana ovyoovyo kama tunavyoona siku hizi. Kijana alipotaka kuoa au kuolewa alihitajika kufuata utaratibu fulani uliokuwa umewekwa.

Ilikuwa ni lazima kijana huyu akubalike katika mbari ya mwenzake. Mvulana alipaswa kwenda kwa wazazi wa msichana kupanda *'ithigi'* (ithigi ni tawi-huu ni msemo uliotumiwa kumaanisha kuwa msichana ameposwa rasmi)

Mvulana hakuenda kule mikono mitupu, alipaswa kupeleka mahari. Wavulana waliokosa mahari walikosa wachumba. Hii ni kwa sababu wasichana walitaka wazazi wao wapewe mahari ikiwa kama shukrani ya kazi ngumu ya ulezi waliyoifanya. Kwa hivyo wavulana waliokuwa fukara walikosa wasichana wazuri wa kuoa. Mvulana aliyependwa na mbari yake angesaidiwa katika utoaji wa mahari.

Methali hii humsawiri mwanamke kama anayevutiwa na mali na hivyo vijana waliokuwa fukara hawakuwa na nafasi ya kujipatia mwanamke mrembo. Hii ni kutokana na ukweli kuwa vijana kama hao hawakuwa na chochote cha kulipia mahari na kama wasemavyo wahenga, mkono mtupu haulambwi. Katika kiwango hiki ni muhimu kutaja kuwa baadhi ya wanaume walipokea mahari hata kabla ya msichana kuvunja ungo. Jambo hili lilifanywa kwa siri na wazazi (hasa baba) wa msichana na mvulana. Msichana alifahamishwa tu baada ya kufikia umri wa kuolewa.

Uhiari wa msichana haukuhitajika.

Kama anavyosema Kenyatta (1938), wasichana na wavulana waliokwisha tahiriwa walitangamana na hata kutongozana, lakini mzazi ndiye aliyetoa uamuzi wa mwisho kumhusu msichana.

Msichana/mwanamke alitazamwa kama aliyedhamini mali zaidi ya furaha yake na kwa hivyo hangediriki kuhusiana na kabwela asiyekuwa na mbele wala nyuma. Katika mkabala huu, mali yaliwekwa mbele badala ya mapenzi.

5.2.6 Njamba ya ndurume irundagwo ni aka.

(Tafsiri)

Mbuzi wa kiume huangushwa kwa urahisi na yule wa kike

'Njamba ya ndurume' ni mbuzi wa kiume aliyekuwa na nguvu nyingi. Mbuzi huyu alipohitajika kuchinjwa ilibidi wanaume kadhaa kushirikiana kumwangusha kwa sababu ya nguvu zake. Hata hivyo mbuzi huyu alinyenyekea mbele ya wale wa kike. Hii ni jazanda iliyomfananisha mbuzi wa kiume na mwanamume. Ilitumiwa kuwatahadharisha wanaume ambao walijihusisha na wanawake waovu na ambao wangewasaliti kwa maadui zao. Methali hii pia ilitumiwa kuwakashifu wanaume waliojifanya kuwa bingwa sana lakini baadaye wanaishilia kuwaoa wake wavivu. Ifahamike kuwa mtu mvivu alidharauliwa sana miongoni mwa wanajamii hawa. Mtu aliyekuwa mzembe alionekana kama mzigo kwa wenzake kwa sababu anapokosa chakula analazimika kuombaomba kwa wenzake. Watu kama hawa walikashifiwa kwa kuelezwa methali ifuatayo:

'Cia thuguri itiyuragia ikumbi.'

Chakula cha kuomba hakiwezi kujaza ghala.

Mbali na kuwa kama chambo cha kunasia mali, wanawake walitumiwa na jamii kurudisha uhusiano mwema na maadui wao. Walimtafuta msichana aliyekuwa mrembo na kumshauri kufanya urafiki na mvulana mmoja wa jamii iliyokuwa adui yao (Ng'ang'a :2005). Kwa sababu ya ashiki ya wanaume, mvulana yule alishawishika kumwoa mwanamke huyu mrembo na hapo kurudisha uhusiano mwema baina ya jamii hizi mbili. Wakikuyu wana methali kuwa wakwe hawasumbuliwi ovyo ovyo.

Ukwe ulileta mahusiano mema baina ya wahusika hawa. Msichana kama huyu alikuwa tayari kujitoa mhanga kuitumikia mbari au jamii yake.

Mwanamke, hasa yule mrembo amesawiriwa kama kiumbe aliye na uwezo wa kumnasa na hata kumfanya mwanamme ajiingize katika balaa. Ingawa uwezo huu alio nao mwanamke si wa nguvu za mwili, ni uwezo uliokithiri.

Kutokana na jambo hili. Wakikuyu humwona mwanamke kama aliyetunukiwa nguvu fulani na Maulana zilizofichama ndani ya uana wake. Mwanamke angelitumia nguvu hizi kuangamiza au kuokoa. Katika mkabala huu, mwanamke amesawiriwa kama mwokozi wa jamii yake. Hili ni jukumu linalomtukuza mwanamke .

Kwa upande mwingine tunaona kuwa nguvu hizi zingetumiwa na jamii kwa manufaa yake bila kutathmini faida au hasara itakayompata mwanamke huyo. Hii ni kwa sababu ndoa kama hii haikujengwa juu ya msingi wa mapenzi ya dhati mbali ni shinikizo la wanajamii. Wanawake waliohojiwa hata hivyo hawakuona uovu wowote wa jambo hili. Waliikubali hali ile na kuiona kama iliyoratibiwa hivyo na Mungu (*Ngai)* na kama imani yao ilivyo, Mungu habadiliki (*Ngai ndaugukagwo*)

5.2.7 Aka a kwene ni irima iriku

(Tafsiri)

Mke wa mume mwingine ni kama shimo la kina kirefu

Methali hii inafananisha mke wa mwenyewe na shimo la kina kirefu. Hii ina maana kuwa mwanamke asiye wako wa ndoa ana mambo mengi usiyoyajua.

Unaweza kufikiri kuwa ni mwema mno au ni muovu lakini huwezi ukajua jinsi anavyohusiana na jamaa zake au mumewe. Hii ndio maana Wakikuyu husema kuwa-:

'Micii ni ndogo'

Maisha ya unyumba ni kama moshi.

Maana inayowasilishwa na methali hii ni kuwa ukiwa nje huwezi kufahamu kwa uyakinifu kinachoendelea mle ndani, ukitaka kujua itakubidi umuulize mwenyeji.

Methali hii hutumiwa kuwaonya watu hasa wanaume dhidi ya kujihusisha na /au kuwatetea wake ambao mbele ya macho yao wanaonekana kuwa wema. Wanawake hawa wanaweza kuwa wameufunika udhaifu mwingi sana. Kupitia kwa methali hii, wanawake wameonyeshwa kama watu walio na uwezo wa kuficha mambo mengi na hasa yanayohusiana na mahusiano yao na waume zao.

Kinaya ni kwamba katika sura hii sehemu ya (5.5.2), mwanamke amesawiriwa kama aliye na udaku mwingi na ambaye hawezi akaficha lolote. Kukinzana kwa methali hizi kunatuonyesha kwamba mwanamke hakuwa na pa kujisetiri, akinyamaza anafananishwa na shimo la kina kirefu na akiongea anaitwa mdaku. Wanajamii hawa walishindwa kutambua kuwa kila mwanamke ana upekee wake kama binadamu yeyote.

5.2.8 Mutumia angikura atari mwana ndangiona wa kumutahira mai

(Tafsiri)

Mwanamke anayezeeka bila mtoto hapati mtu wa kumtekea maji

Mwanamke aliyekosa watoto aliitwa '*thata*' (tasa).Wanajamii walimbatiza hivi hata bila kudhibitisha kuwa mwanamke huyu hakuwa na uwezo wa kuzaa. Hii ni kwa sababu katika jamii ya Wakikuyu utawa haukujulikana. Hivyo kila mwanajamii alitarajiwa kuendeleza ukoo kwa njia ya kuzaa.Waliokawia kutekeleza jukumu hili teule walitazamwa kama waliokuwa na kasoro. Methali hii pia iliwahimiza wanawake kuzaa kwa kuwatajia madhara ya kukosa mtoto. Watoto walikuwa na umuhimu mkubwa miongoni mwa Wakikuyu. Ilisemekana kuwa ndio watakaowasetiri wazazi wao katika uzee wao. Lilikuwa jambo la huzuni kwa mtu kutotajwa na jamaa zake kupitia kwa watoto waliozaliwa. (Mfumo wa utoaji jina miongoni mwa Wakikuyu ulikuwa wa kuwataja jamaa wa kuumeni na kukeni).

Kukosa kuzaa kulihusishwa na uchawi na laana ya wazazi. Kwa sababu hii mwanamke aliyekosa kuzaa alipelekwa kwa waganga ili wamgangue au kumpa suluhisho la tatizo hilo. Kazi ya kuchota maji ilikuwa ya wasichana. Watoto walikuwa wamefunzwa kumheshimu na kumtumikia yeyote aliyehitaji msaada wao. Hivyo wangemsaidia mwanamke kama huyu lakini haikuwa rahisi kuwapata kwa sababu walitembelea maboma yaliyokuwa na watoto wa rika lao.

Jambo lingine ni kuwa mume wa mwanamke kama huyu alikuwa na uhuru wa kuoa wake wengine. Watoto wa mke mwenza wangemsaidia mama yao wa kambo lakini ni jambo lililofahamika katika jamii hii kuwa wake wenza wengi hawakuwa marafiki. Sababu nyingine ni kuwa mume wa mke kama huyu alimpuuza mke asiye na watoto kwa sababu anamnyima nafasi ya kupata mahari kupitia kuwaoza wasichana.

Watoto walimfanya mwanamke kuheshimiwa na kukumbukwa kwa muda mrefu baada ya kifo chake. Wakikuyu waliusisitiza ukweli huu kwa kusema:

'Muciari etiagire eciariire'.

Mzazi hujivunia mtoto aliyemzaa.

Ndoa katika jamii ya Wakikuyu huonekana kama msimbo wa kupokezana uhai na kupanua jamii. Mwanamke katika jamii hii ni msingi wa familia. Katika malezi yake mtoto wa kike hukuzwa na kuelekezwa katika njia itakayomfikisha katika uzazi na utunzaji wa watoto. Ndoa hutazamwa kama iliyo na dosari wahusika wasipajaliwa watoto. Mwanamke hudharauliwa na kutengwa na jamii. Ingawa ukosefu wa watoto unaweza kutokana na kasoro ya mwanamume, wanawake walionekana kama ndio haswa waliorogwa au kuchukua lawama ya miungu kwa kosa la wazazi wao.

Dhana ya '*dhata*' (tasa) ilitumika kuwarejelea wanawake ambao hawakujaliwa kupata watoto. Wanaume waliokuwa gumba hawakuwa na istilahi ya kuwarejelea. Mwanaume katika ndoa za aina hii aliruhusiwa kuoa mke mwingine kwani lawama ya utasa daima ilirundikiziwa mwanamke. Hadhi yake basi ilitegemea uwezo wake wa kutekeleza jukumu hilo la kuendeleza kizazi. Maisha yake yalistaaladhika au kudhalilika kutegemea uwezo wa kutekeleza jukumu hilo.

Ingawa ni dhahiri kuwa mwanamume aliyekuwa gumba alisikitishwa na hali yake, hali yake ilibakia kuwa siri ya mkewe. Hii ni kutokana na ukweli wa kimaumbile kuwa ni mwanamke anayechukua mimba.

Mwanaume kwa upande wake hajafungwa na silasila hizi. Yamkini ndio maana Wakikuyu wakasema kuwa ,

'Cia mundurume itiri iria'.

Titi za mwanamume hazina maziwa.

Pale ambapo ilibainika waziwazi kuwa ni mwanamume aliyekuwa na kasoro, walishauriana na mkewe kuwa ahusiane kimapenzi na wanaume wengine watakaoweza kumtungisha mimba lakini afanye hivyo kwa siri ili jambo hili lisigunduliwe na hivyo kumfanya mume huyu kuvunjiwa heshima. Hata katika hali hii ni mwanamume aliyemchagulia mkewe mume atakayemzalisha.

Kwa vyovyote vile mwanamke alishushwa kwani thamani yake ilipimwa kwa mizani ya kuwepo au kutokuweo kwa watoto. Mwanamume kwa upande wake alikuwa na uhuru wa kuoa zaidi ya mwanamke mmoja atambuapo kuwa yule wa kwanza ni tasa au kuletewa tu watoto wa nje iwapo ni yeye ana shida.Watoto hawa wanakuwa wake kihalali na ikiwa ni wasichana, anakuwa tayari kupokea mahari pindi wafikiapo umri wa kuolewa.

5.2.9 Mwanake wina indo doihanaga.

(Tafsiri)

Mvulana mwenye mali hapotezi muda wake kuwatongoza wasichana, badala yake ni wasichana wanaomtafuta

Wavulana walipotahiri walipewa sehemu ndogo ya urithi na baba yao. Wakikuyu husema kuwa kutahiri ni kama kutayarisha mahali pa kuweka kuni- yaani tohara ni tendo linalomuandaa mwanajamii kutekeleza majukumu fulani muhimu kulingana na uana wake.

'Kurua ni kwara itara'

Kutahiri ni kutengeneza '*itara*' (sehemu iliyotengenezwa darini na hutumiwa kuwekea kuni hasa zilizo mbichi ili zikauke .)

Mvulana mwenye busara alikuza na kuongeza mali hii kupitia kwa juhudi zake. Kijana kama huyu alipendwa sana na wasichana kwa sababu ya bidii yake. Ifahamike kuwa katika jamii ya Wakikuyu, msichana hakuruhusiwa kuwatongoza wavulana. Msichana aliyefanya hivi alitazamwa kama mtovu wa adabu. Wasichana walishauriwa na jamaa zao wafanye uchumba na vijana kama hawa ili wazazi wa msichana waweze kupewa mahari mengi. Kwa sababu hii, mvulana aliyekuwa na mali hakujishughulisha na kuwasaka wasichana kwani walimtafuta alikokuwa. Hata hivyo njia ya kumvutia mvulana ilikuwa kupitia kwa mama mvulana. Wasichana walimsaidia mama kama huyu kwa kazi za kuteka maji, kuvunja kuni na kazi zingine za shambani. Tofauti ya kiuana inayodhihirika hapa ni kuwa msichana hakuwa na uhuru wa kumtongoza msichana hata kama amempenda. Aliyefanya hivi alichukuliwa kama malaya.

Mali miongoni mwa Wakikuyu haikupatikana vivi hivi. Mbali na mali ya kurithiwa, watu wengi waliokuwa na mali walikuwa wameyapata kupitia kwa kazi ngumu. Kijana aliyekuwa na mali aliheshimiwa na kujulikana.

Cha ila ni kuwa mali haya yalionekana kama chambo cha kuwanasia wasichana. Basi mvulana aliyekuwa na mali hakuwa na sababu ya kujishughulisha kumtafuta mchumba kwani mali ile ilikuwa na uwezo kama wa sumaku wa kumvutia mrembo yeyote pale kijijini. Kwa kuzingatia maudhui haya tunabainikiwa na ukweli kuwa wanawake katika jamii ya Wakikuyu walionekana kama watu wasiothamini mapenzi ya dhati katika ndoa na badala yake hukimbilia mali.

Picha tunayoipata hapa ni ile ya kumwona mwanamke kama anayevutiwa tu na mali pasi na kuwa na mapenzi ya dhati.

5.2.10 Atumia matiri riika

(Tafsiri)

Wanawake hawana rika (katika ndoa)

Rika lilitokana na kuwa watu walitahiri pamoja. Watu waliotahiri pamoja waliitana 'wa rika langu'. Watu wa rika moja walipendana kama watu waliozaliwa na mama mmoja. Rika ni mojawapo wa mambo yaliyosaidia kuunganisha jamii ya Wakikuyu na pia kuimarisha uhusiano baina yao.

Wakikuyu waliamini kuwa wanawake hawana rika kwani wangeolewa na wanaume wazee kuwaliko. Mwanamke alipoolewa alichukuliwa kuwa wa rika la mume wake. Aliwakaribisha nyumbani kwake wazee wa rika la mumewe. Hata baada ya mwanamke kutahiriwa aliendelea kutawaliwa na wanaume hasa kaka zake waliokwisha tahiriwa na pia babake mzazi. Ndio maana kulikuwa na methali miongoni mwa Wakikuyu isemayo-:

'Uhii ni umagwo no uka ndumagwo'

Wavulana hubadilika wanapotahiriwa kwa mujibu wa hadhi lakini wasichana hawabadiliki.

Ibainike kuwa maumbile yalichangia pakubwa katika kuizatitisha methali hii. Hii ni kwa sababu mwanamke hupoteza uwezo wa kuzaa anapofikisha miaka arobaini na tano na kuendelea. Mwanamume kwa upande wake hubakia na uwezo wa kuzaa hata anapozeeka. Hivyo mwanamume mzee anaweza kuoa mke mchanga lakini kinyume chake hakiwezekani hasa katika muktadha wa jamii hii. Ikumbukwe kuwa lengo kubwa la ndoa katika jamii ya Wakikuyu lilikuwa kuendeleza ukoo kupitia kuzaa. Hivyo jambo lolote lililoonekana kuwa pingamizi kwa lengo hili liliepukwa.

Kama tulivyoona katika sehemu iliyotangulia ya ujamiishaji, mwanamume anakwea ngazi ya mamlaka kulingana na umri. Hii inamfanya kushirikishwa katika halmashauri mbalimbali za wazee. Mwanamke kwa upande wake hawezi kusimama kidete na kujitosa katika mabaraza haya licha ya umri wake mkubwa. Mwanamke alipoolewa alihesabiwa katika rika la mumewe. Hili ni jambo lililokubalika miongoni mwa wanajamii hawa. Mwanamke mchanga angeolewa na mzee aliyemzidi kwa umri mradi tu awe na uwezo wa kumlipia mahari. Mwanamke alibakia chini ya amri ya mwanamume tangu utotoni hadi mautini. Akiwa msichana alipaswa kutii amri ya baba yake na alipoolewa hakuwa na budi kumtumikia mumewe kwa utiifu. Wanjiru (2005) anatoa kauli kwamba wanawake hawakupendelea hali hii hasa kwa sababu waume na hata kaka zao waliruhusiwa na jamii kuwachapa. Hata hivyo anasema kuwa hakukuwa na lolote wangelilifanya ili kubadilisha jambo hilo kwa sababu mfumo wa mahusiano ya jamii ulihalalisha vita vile.

5.2.11 Muka uri mwana ndoraga

(Tafsiri)

Mke mwenye mtoto hatoroki kutoka kwa mumewe

Baada ya mwanamke kuolewa, watu walitarajia mtoto kwa hamu .Kitendo cha kuzaa kilikuwa cha kujisajili rasmi kama mwanachama wa kudumu wa familia ile. Mtoto alikuwa kama gundi ya kushikanisha koo zile mbili na kushamirisha urafiki baina yao. Kutalikiana kwa mke aliyekuwa na mtoto kulikuwa nadra sana. Ingewabidi wazee wa baraza la wazee kujadili kwa kirefu kuhusu jambo hili.

Mwanamke alivumilia mambo mengi kwa ajili ya watoto wake. Mwanamke hakuwawacha watoto wake kwa hiari. Hata mara nyingi ungewasikia wakikuyu wakisema :

'Ikuaga imaamiriirie matumbi'

Kuku hufia juu ya mayai akingojea kuangua

Jambo lingine ni kuwa mwanamke alipotoroka kwa mumewe bila sababu mwafaka ilibidi arudishwe pamoja na mbuzi wa kiume aliyejulikana kama 'mbuzi wa kuwasha moto.'

Hii ni kwa sababu aliacha boma lake bila yeyote wa kuwasha moto na isitoshe, mumewe amehisi baridi kwa muda wote huo aliokuwa ametoroka. Moto hapa ulitumika kijazanda kurejelea mahusiano ya kimwili kati yao.

Jukumu kubwa la mwanamke kama wahojiwa wengi walivyoeleza ni kuzaa na kuitunza familia. Ingawa hili lilikuwa jukumu lililotarajiwa kutoka kwa mwanamke, alitekeleza majukumu mengine muhimu kama vile kutunza na kupamba makazi yake na kufanya kazi shambani ili kutosheleza mahitaji ya chakula ya familia yake. Mwanamke aliyekosa uwezo huu alitazamwa kama aliyefifisha kizazi chake. Kuzaliwa kwa mtoto kulishangiliwa sana kwa sababu kulizifunga koo mbili kwa fundo lisiloweza kufunguka tena. Mwanamke alivumilia mambo mengi pale kwa mumewe kwa sababu ya kuhofia kuwa akiondoka watoto wake watateseka. Vita vilipozidi na labda mke kama yule akaamua kutoroka, alirejeshwa kwa mumewe na wazazi wake kwa sababu katika jamii ya Wakikuyu, mwanamme alipoamua kumfukuza mkewe ingembidi atafute wazee wawili au zaidi watakaomrejesha mkewe kwao. Kitendo hiki kilifungua jukwaa la mazungumzo kati ya mwanamke na jamaa zake na pia mwanamume yule na jamaa zake. Wakikuyu huamini kuwa unyumba hauvunjwi pasi na sababu maalum. Wao huamini kuwa hakuna kesi ngumu kuamua kama ya kuvunja ukwe hasa ikiwa wahusika wana watoto.

'Cira munene ni wa uthoni ugikua.'

Methali hii inatusawiria mwanamke aliyekuwa tayari daima kuitoa sadaka furaha yake kwa sababu ya watoto wake. Kutokana na jambo hili tunaweza kuhitimisha kuwa kutoondoka kwa mwanamke kunamwonyesha mwanamke kama mtu mvumilivu na mwenye uwezo mkubwa wa kustahimili idhilali nyingi.

5.2.12 Muka mucangacangi daagaga mwana.

(Tafsiri)

Mwanamke anayerandaranda huishilia kupata mtoto nje ya ndoa.

Mwanamke anayerandaranda ni yule ambaye hakutulia kwake. Kurandaranda hapa ni neno lililotumiwa kumaanisha kushiriki katika vitendo vya usherati. Methali hii ilitumiwa kuwaonya wanawake dhidi ya kujihusisha na vitendo vya usherati. Kinaya ni kwamba wanaume waliorandaranda hawakuhukumiwa. Badala yake walihimizwa kuwa na wake wengi kama methali ifuatayo inavyokiri:

'Gutiri jogoo ya mwera umwe.'

Hakuna jimbi wa mtamba mmoja.

Msichana alipopata watoto akiwa kwao alikosa mvulana wa kumuoa. Mvulana kwa upande wake hakukosa mke hata kama alijihusisha na usherati. Mara nyingi wasichana kama hawa waliishilia kuolewa na wazee wakongwe. Tena walibidika kufanya kazi ngumu ya kuwalisha na kuwavika watoto wao. Msichana kama huyu aliwanyima wazazi wake fursa ya kupata mahari mengi kwa sababu tayari binti yao ana dosari.

Lilikuwa jambo lililokubalika miongoni mwa Wakikuyu kwa mwanamume kuoa zaidi ya mke mmoja. Kwa mwanamume, hili lilikuwa jambo la fahari kwani uwepo wa wake na watoto wengi ulilinganishwa na kuwa na mali na uwezo. Mwanamke kwa upande wake alihitajika kuwa mwaminifu na alipoonekana kuwa na jicho la nje alipigiwa methali hii. Iwapo angetambulikana na idhibitishwe kuwa alitembea nje, hili lilikuwa kosa ambalo lilistahili adhabu ya kurejeshwa kwao. Angeruhusiwa tu kuwa na mpenzi mwingine pale ilipodhibitika kuwa mumewe alikuwa gumba. Hata ilipobainika vile, ni mumewe ndiye aliyekuwa na mamlaka ya kumchagulia atakayehusiana kimapenzi naye. Ingawa ni kweli kuwa yaliyompata kiboko na ngwena yalimngoja, wanaume waliepuka shutuma na mausio haya . Kuzaliwa kwa mtoto nje ya ndoa kulitazamwa katika muktadha huu kama adhabu ya kutangatanga. Adhabu yenyewe ilikuwa kwa mwanamke ambaye angelijitwika mzigo wa ulezi huku mwanamume aliyeotesha mbegu hii ya uhai akisamehewa na wanajamii. Haya ni mapendeleo makubwa kwa wamaume kwani wao waliporandaranda hawakushutumiwa kama walivyofanywa wanawake. Matatizo ya ng'ono kwa wanawake hayakushughulikiwa.

Hii ni sababu mojawapo iliyomfanya mwanamke kurandaranda. Kwa mujibu wa Mugo (1982) matatizo ya mwanamume yalishughulikiwa hivi:-

> "Mwanamume alipendelea kuoa mke mchanga katika uzee wake ili yule mke mwenye 'damu moto' ya ujana amhudumie na kumsisimua mzee. Katika kufanya hivi, mzee yule anakuwa anasisimuka kila wakati na kuchangamka na hivyo kuonekana mchanga kila uchao ."
>
> (Tafsiri yangu)

Mwanamke alinyimwa fursa hii ya kusisimuliwa.

5.2.13 Mwari mweru ndaraguragirwo

(Tafsiri)

Mwanamke mweupe hafanyiwi uganga

Wakati wa zamani kulikuwa na waganga. Waganga hawa walikuwa wakifanya kazi nzuri katika jamii ya Wakikuyu. Hii ni kwa sababu walitambua sababu ya kufanyika kwa baadhi ya mambo na pia walipendekeza tiba. Mtu alipopatwa na janga fulani kama la uchawi au '*guthemengwo*' (kuna watu waliosemekana kuwa na mate mabaya na kwamba wangealika maafa kwa mtu na yakampataa vile bila kutumia uchawi), alimwendea mganga ili aweze kutibiwa.

Wasichana walioishi kwa muda mrefu bila kupata waume walihimizwa kuwatembelea waganga ili waganguliwe kwa sababu jukumu la kimsingi la mwanamke katika jamii hii lilikuwa kuendeleza kizazi. Wasichana waliokuwa warembo waliolewa pindi tu walipotahiri. (Ifahamike kuwa kivumishi –eupe kilitumiwa kurejelea urembo). Kwa hivyo hakukuwa na haja ya kuwatembelea waganga. Kinyume na ilivyokuwa baina ya wanawake , haiba ya mwanamme haikuwa na umuhimu. Ndio maana Wakikuyu wakanena kuwa uzuri wa mwanamme si kuwa na meno yaliyopangika kama kete.

'Uthaka wa mundurume ti magego'

Urembo wa mwanamume si meno

Pia wao husema kuwa kuparara kwa mwanamme si hoja.

'Hunyu ni umwe na arume'

Kuparara ni kwa wanaume

Kama ilivyo katika jamii nyingi, urembo wa mwanamke ulitukuzwa sana. Isitoshe, urembo wa mwanamke ulitumiwa kama chambo cha kuwageuza maadui kuwa marafiki. Kupitia kwa njia hii tunamwona mwanamke akitumiwa kuinufaisha jamii nzima na palepale maisha yake yakiwekwa katika hatari. Nyakati zile hakukuwa na majukwaa ya kuutumia urembo huu kwa manufaa ya mrembo mwenyewe kama tunavyoona siku hizi katika mashindano ya urembo. Manufaa yake yaliisha pindi mrembo yule alipojipatia mchumba. Kwa sababu ya kuwa na wanaume kadhaa waliotaka kumchumbia mrembo huyu, wazaziwe walidai kiwango kikubwa cha mahari na kwa hivyo mwenye uwezo wa mali ndiye aliyeweza kujipatia kisura huyu.

Imebainika wazi kuwa mahari yalikuwa na umuhimu wa kuunganisha mbari mbili na vile vile kumtumikisha mwanamke. Kadiri mahari yalivyokuwa mengi ndivyo ambavyo ingelikuwa vigumu kwa wazazi wa msichana kuyarejesha pindi binti yao akosanapo na mumewe. Urembo kwa upande wa wanaume haukuwa na umuhimu wowote. Maadamu anaweza kulipia mahari, basi mengine si hoja. Kupitia kwa methali kama hii mwanamke alikumbushwa daima kuhusu maumbile yake- urembo ambao hakuwa na uwezo wa kuubadilisha, isitoshe hiki kilikuwa kigezo cha kugezea thamani yake. Ni muhimu kutambua kuwa jamii iliuhusudu urembo na ndio maana mwanamke mrembo aliolewa mapema. Wale waliokuwa na sura mbaya (ingawa jambo hili ni la kimjadala) waliishilia kubakia kwa wazazi wao kwa muda mrefu.

5.2.14 Kwi ngatha na nyagacu

(Tafsiri)

Kuna mke aliyependwa na aliyechukiwa

'Ngatha' ni mwanamke aliyekuwa amependwa na mumewe ilhali *'nyagacu'* ni yule aliyechukiwa. Mwanamume Mkikuyu aliyekuwa na zaidi ya mke mmoja aliheshimiwa kwa sababu hili lilikuwa dhihirisho kuwa aliweza kuwadhibiti. Alihitajika kuwakimu wanawake hawa kwa kila hali bila kuonyesha mapendeleo. Hii ndio maana alijenga nyumba yake *(thingira)* kando ya zile za wakewe ili aweze kuwahudumia kwa zamu. Wanawake kwa upande wao walihitajika kunadhifisha *'thingira'* na kuhakikisha ya kwamba mume wao ana chakula cha kutosha wakati wote. *Ngatha* na *Nyagacu* ni majina ya lakabu yaliyowakilisha wanawake waliokuwa wameolewa na mume mmoja.

Kama binadamu, kulikuwa na uwezekano wa mume huyu kumpendelea mke mmoja zaidi ya mwingine. Mwanamume alipojikuta katika hali hii ni bayana kuwa angeitumia methali hii kuhalalisha madharau kwa mwanamke mmoja. Hili lilikuwa jambo lililotendeka sana kama tunavyobainishiwa na methali isemayo: -

'Ciakorire Wacu mugunda'

(Bahati ilimwandama Wacu hadi shambani)

Methali hii ilichipuka kutokana na kisa kifuatacho-:

Inasemekana kuwa kulikuwa na wake wenza wawili. Mmoja alipendwa na mumewe (*Ngatha*) na wa pili (*Wacu*) alichukiwa.

Ilitukia kuwa watu walipanga kuja kumchumbia binti wa Wacu (aliyekuwa amechukiwa). Kwa sababu ya chuki aliyokuwa nayo mume kwa mke huyu, hakuruhusiwa kuwepo wakati wa sherehe hizo. Badala yake mumewe alimshurutisha kwenda shambani kulima. Wacu, kama mwanamke mwingine yeyote wa Kikikuyu alimtii mumewe na kuelekea shambani.

Kule nyumbani sherehe ziliendelea. Ilikuwa kawaida kwa mbuzi na kondoo kadhaa kuchinjwa wakati wa hafla kama hizi. Wanyama hawa walipochinjwa kuna jinsi ambavyo yale matumbo yalitengenezwa kwa kuwekwa vipande vidogovidogo vya nyama laini , damu na mafuta (*ngarango*). Matumbo haya baada ya kutayarishwa vile yalichukua umbo la soseji kubwa zilizojulikana kama '*ndundiro* ,*mahuu* au *mutura'*. Mitura hii ilikuwa na ladha tamu na ilipendwa sana na Wakikuyu.

Ilitokea kwamba wakati '*mitura'* hii ilikuwa ikichomwa mwewe alikuja na kunyakua mmoja na kutoroka nao. Kwa sababu ulikuwa ungali moto, alipofika shambani karibu na alipokuwa Wacu, alishindwa kuvumilia kuubebana kwa hivyo akauangusha. Wacu aliuchukua '*mutura'* ule na kuula. Alichonyimwa Wacu kilimwandama hadi shambani. Ni dhahiri kutokana na methali hii kuwa ubaguzi na mapendeleo yaliyoendelezwa na mwanamume yalisababisha kutoelewana baina ya wake wenza. Kulingana na King'ori (2005), mwanamume aliegemea zaidi upande wa mwanamke aliyemtumikia na kumtii. Methali hii ilitumiwa kuwahimiza wanawake wajibiidishe katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili wapendwe na waume wao. Jamii ilijaribu kupalilia maadili mema kwa wanawake kupitia kwa matumizi ya maneno ya nasaha kama haya.

5.2 Methali zinazolenga malezi

5.3.1 Karegi nyina gatihonaga

(Tafsiri)

Mtoto wa mbuzi akisusia titi za mamaye mwishowe hufa

Methali hii huelezwa watoto walio watundu. Mtoto wa mbuzi akisusia titi za mamake bila shaka atadhoofika kwa kukosa lishe na mwishowe atakufa. Mtoto alipokosa kufuata mawaidha ya wazazi wake aliambatwa na maafa kwa sababu ya laana ya wazazi wake. Wakikuyu husema kuwa laana ya mtu aliye hai ni mbaya kuliko ya mfu.

Ukweli huu ulidhihirika katika maisha ya mtu kama huyu. Mamake mtu sio mama mzazi tu ila ni watu wanaoshirikiana katika malezi ya mwanajamii. Mtu alipokosa kuzingatia mashauri ya watu kama hawa aliishi maisha ya shida na mwishowe akafa.

Methali hii inatufunulia umuhimu wa kuwasikiliza wazazi wa kike. Methali hii imemtumia mbuzi na mwanambuzi kama jazanda inayowakilisha mama na mwanawe. Inashadidisha ukweli kuwa mwanamke alikuwa na jukumu kubwa katika malezi ya wanawe. Titi zinawakilisha chakula anachokitegemea mtoto akiwa mdogo ili aweze kukua. Jambo hili linakiri ukweli kuwa katika Jamii ya Wakikuyu, ni mwanamke aliyekuwa na jukumu la kuilisha jamii, kuwaadabisha watoto na kuwaelekeza. Kwa sababu ya kazi hii nzuri, watoto walitahadharishwa dhidi ya kupuuza mawaidha ya wazazi wao. Haikuwa ajabu kumwona mwanamke akiadhibiwa na mumewe kwa sababu mwanawe wa kike amepata mimba. Wazo kuu linalopatikana hapa ni kuwa mtoto asipomtii mama hudhurika. Methali hii inamkweza hadhi mwanamke kwa kumsawiri kama mzazi anayestahili kuheshimiwa na kutiiwa na watoto wake.

5.3.2 Kuguna mwana no ta kuguna nyina

(Tafsiri)

Kunufaisha mtoto ni sawa na kunufaisha mamake

Ukimtukuza mtoto kwa kumtendea wema, mtoto huyo husimulia mamaye jambo hili. Naye mamaye hufurahia sana jambo hili. Zamani zile wanawake ndio waliokuwa na jukumu kubwa la malezi kwa sababu kazi zao zilikuwa za pale nyumbani. Kwa sababu ya kuoanisha jukumu la ulezi na hulka ya watoto, wanawake wakati mwingine walijikuta katika hali ngumu ya kuchukua lawama ya makosa ya watoto wao. Mtoto alimtambua zaidi mama yake kuliko baba yake. Mtoto alipochunwa au kuchokozwa na yeyote alikimbia kushtakia jambo hili kwa mama yake. Kwa hivyo uhusiano wa mama na mtoto ulikuwa mkubwa sana na ulipunguka tu baada ya mvulana kutahiriwa au msichana kuolewa. Wakikuyu waliamini kuwa ukitaka kumfurahisha mama unaweza kufanya hivyo kwa kumfurahisha mtoto.

Methali hii inatusisitizia umuhimu wa jukumu analotekeleza mama. Kwa mujibu wa Nga'nga (2005) hakuna mtu anayemfahamu mtoto kama mamaye.

Anauelewa udhaifu wake na vilevile uzuri wake. Kwa sababu ya ukuruba huu, unapofurahisha mtoto unakuwa umemtendea mama heshima. Hii ni mojawapo ya methali zinazomlenga mama/mwanamke na juhudi zake za ulezi - jukumu linalompa mwanamke heshima kubwa.

5.3.3 Guciara kunaga irigu ngingo

(Tafsiri)

Kuzaa huufanya mgomba wa ndizi kuvunjika

Mgomba wa ndizi ni kiwakilishi cha mwanamke na kuvunjika kwake ni kule kudhoofika au kutambarajika kwa mwanamke baada ya kuzaa. Mwanamke alitaabika sana alipokuwa akilea mimba. Pia uchungu wa kuzaa ulikuwa mkubwa sana na wanawake wengi walikufa walipokuwa wakijifungua. Baada ya kuzaa, mwanamke alikuwa na jukumu la kumlea mtoto huyo hadi atakapofikia utu uzima. Kipindi cha kulea kilikuwa kipindi cha shida kwa wazazi kwa sababu kama mtoto huyo angelifanya jambo ovu, ni wazazi ambao walitoa faini. Ingawa mbari nzima ilisaidiana katika kuwaadabisha watoto, wazazi hasa wa kike walichukua nafasi ya kwanza kutekeleza jambo hili. Mtu mzima alimkanya au hata kumwadhibu mtoto aliyekutikana akifanya tabia mbaya.

Watoto nao waliwaheshimu watu wazima. Methali hii inadai kuwa urembo wa mwanamke ulipungua kiasi alipojifungua.

Mgomba wa ndizi hapa umetumika kama kiwakilishi cha mwanamke. Si ajabu kuwa katika jamii nyingi, mgomba wa ndizi huwekwa kwenye lango la mahali panapofanyiwa sherehe za ndoa ili uwe kama sala ya kuomba Maulana awajalie maharusi watoto. Mwanamke anasawiriwa kama ndiye anayelemewa zaidi na mzigo wa uzazi. Hii inatokana na maumbile yake kwa sababu mwanamume hana uwezo huo. Vile vile alikuwa na jukumu la kuhakikisha ya kwamba wanawe wanakua kwa njia nzuri.

Katika jamii ya Wakikuyu, mwanamke alipojifungua alishonewa mbeleko iliyotengenezwa kwa ngozi ya kondoo (*Ngoi*). Mwanamke alitumia mbeleko hii kubebea mtoto. Ikiwa hakuwa na watoto wengine wakubwa ambao wangemsaidia kubeba mtoto, alilazimika kuendelea na shughuli zingine kama vile kulima akiwa amembeba mwanawe mgongoni. Methali hii inamwangalia mwanamke kwa mkabala wa anavyochakaishwa na kitendo cha kuzaa.

Imani hii iliwafanya wasichana waliozalia nyumbani kwao kuonekana kama waasi. Kupungua kwa thamani yao kulithibitishwa na kupungua kwa kiasi cha mahari atakacholipiwa iwapo atabahatika kupata mchumba.

5.3.4 Muiritu njong'i akiuhwo nyina athekaga na kamwena

(Tafsiri)

Kuposwa kwa msichana mwenye sura mbaya humfurahisha mamaye.

Msichana aliye na sura mbaya hakuwa na uwezo wa kuwavutia wachumba na kwa hivyo ilikuwa nadra kupata mtu wa kumchumbia. Hii ndio iliwafanya Wakikuyu kusema kuwa msichana mrembo hamhitaji mganga kwani hakuwa na shida ya kupata mchumba.Wasichana warembo waliolewa pindi tu walipotahiri. Hata wakati mwingine wazazi wa binti mrembo walidinda kuchukua mahari ikiwa mahari ile ilikuwa kidogo kwa sababu walijua binti yao anaweza kuchumbiwa na mtu mwenye mali. Msichana mwenye sura mbaya alipendwa tu ikiwa alikuwa na sifa nyingine ya kando kama vile bidii kazini. Msichana kama huyu alimfanya mama yake kuwa na huzuni kwa sababu asipopata mchumba na kwa bahati mbaya apate mimba nje ya ndoa ,basi mamake atakuwa na jukumu kubwa la kumlea mtoto huyo. Msichana kama huyu akipoposwa mama yake alifurahi kwa sababu ya kuondolewa kwa hofu ile. Methali hii inatuonyesha kuwa mwanamke alisikitishwa na kuwa na mtoto mwenye ulemavu fulani wa mwili.

Mwanamke mrembo kama nilivyoeleza katika sehemu ya 5.2.6, alitukuzwa sana katika jamii ya Wakikuyu. Hii ni kwa sababu wazazi wake wangepata faida kubwa kupitia kwa mahari itakayotolewa wakati atakapoposwa. Kwa upande wake, msichana mwenye sura mbaya alishauriwa kujibiidisha sana kazini. Kama tulivyoona katika sehemu ya ujamiishaji sehemu ya 4.3, Wakikuyu walithamini sana arthi kwani ilikuwa uti wa mgongo wa maisha yao. Kutokana na jambo hili, sifa nyingine ambayo ingempa mwanamke aliye na sura mbaya nafasi ya kupata mchumba kwa haraka ni bidii shambani.

Ingawa methali hii inaweza kuhusishwa na udhaifu wa kitu chochote anachokiuza mtu na kilicho na udhaifu fulani, mfano huu unatuonyesha kuwa udhaifu wa mwanamke hasa wa sura ulipigiwa kimbirikizi zaidi.

Mwanamke kama mzazi anaonyeshwa kulemewa zaidi na udhaifu wa wanawe. Muegemeo wa kiuana unadhihirika waziwazi kwani mwanamume wa sura mbaya hakuwa na tatizo lolote la kupata mchumba.

5.3.5 Ndugu ya mwana imatagio ni nyina

(Tafsiri)

Urafiki wa watoto hushamirishwa na mamao

Urafiki kati ya mtoto na mwingine ulijulikana na mama zao kwa sababu mama ndiye aliyekuwa karibu sana na watoto. Iwapo urafiki huu haukumfurahisha mama, alimwonya mwanawe dhidi ya kuendelea nao. Ikiwa aliufurahia urafiki huo alimhimiza mwanaye aendelee kuhusiana na mtoto huyo. Hata ikimbidi, aliwafurahisha watoto hawa kwa njia kadhaa ili waendelee kudumisha urafiki wao. Mwanamke kwa hivyo alikuwa na kazi ya kuwaelekeza wanawe hasa kuhusu mahusiano yao na watu wengine.

Mama ndiye anayeweka misingi ya maisha ya mtoto. Imedhibitishwa kuwa wazazi waliweza hata kuwatafutia watoto wao wachumba. Kutokana na methali hii tunamwona mama kama mzazi aliyekuwa na jukumu kubwa la kuadaa maisha ya baadaye ya mtoto wake. Mzazi huyu wa kike alikuwa katika nafasi nzuri ya kuhimiza mwanawe aendelee na urafiki na wenziwe au kuwatahadharisha dhidi ya urafiki kama huo. Kinachosisitizwa hapa ni jukumu analotekeleza mzazi wa kike katika malezi ya watoto akilinganishwa na yule wa kiume. Kulikuwa na visa vya wazazi hasa wa kike wa kuwapendekezea watoto wao wa kiume msichana atakayeolewa. Msichana alipoolewa alikaa kwa muda na mama mkwe. Walipika, kulima na kufanya shughuli za pale nyumbani kwa pamoja. Msichana huyu alishauriwa kujibiidisha kazini na kumpendeza mama mkwe. Kufanya hivi kulimchongea nafasi nzuri katika jamii alimoolewa. Iwapo mama mkwe hakupendezwa na mkaza mwana huyu, angeweza kumshauri mwanawe amtaliki mapema kabla ya wao kupata watoto.

Methali hii inamtukuza mwanamke hasa kwa sababu ya jukumu analotekeleza na papo hapo kumsawiri kama anayeweza kudhalilisha maisha ya mwanamke mwengine (mkaza mwana) kwa kumfitini kwa mumewe iwapo hafurahishwi naye.

5.3.6 Mwana amenyagwo ni nyina

(Tafsiri)

Mtoto hujulikana vema na mamake

Mamake mtu ni wa maana sana katika maisha ya wanajamii. Sababu ni kuwa ndiye aliye na jukumu la kuwatunza na kuwalea watoto tangu wakiwa wadogo. Kwa sababu hii wazazi waliwajua watoto wao vizuri nao watoto wakawajua wazazi hasa mama. Mama ndiye hutambua kama mtoto ni mgonjwa au ana njaa. Wakati wa kale kazi za wanawake zilikuwa za pale nyumbani na kwa hivyo ilikuwa nadra kwa mwanamke kumwachia mtu mwingine wanawe awalee. Wanawake walipaswa kubakia nyumbani na kuwalea watoto hadi wawe watu wazima.

Kwa sababu ya maingiliano baina ya mzazi wa kike na watoto wake, mzazi huyu aliweza kuwafahamu watoto wale vizuri zaidi. Zaidi ya kumfahamu mwanawe kwa sura ,mama aliweza pia kufahamu hulka ya kila mtoto kulingana na mahusiano yake na aila yake pale nyumbani. Methali hii sawa na iliyotangulia inatuibulia nafasi ya mama katika malezi ya wanawe, nafasi ambayo haina kisawe. Katika jamii ya Wakikuyu, wavulana wanapotahiriwa walijiainisha zaidi na baba zao.

Methali hii inamtukuza mwanamke kwa kuonyesha umuhimu na jukumu analotekeleza katika malezi ya watoto.

5.3.7 Mwana mukigu aturagia nyina na maithori

(Tafsiri)

Mama mwenye mtoto mtundu huishi daima na machozi

Mtoto mtundu ni yule mtoto ambaye hufanya vitendo viovu na vya aibu. Mtoto kama huyu huwapa wazazi wake hofu kubwa na hasa mamake kwani ndiye anayekuwa naye wakati wote. Kama angeharibu kitu cha wenyewe ni wazazi wake ambao walilipa. Mtoto kama huyu alisababisha kuwepo kwa vita kila mara pale nyumbani kati ya baba na mamake. Mama ndiye aliyeadhibiwa kwa sababu ya kumfedhehesha mumewe kupitia kwa tabia mbaya ya mwanawe. Kulikuwa pia na watoto waliokuwa na akili punguani. Watoto hawa hawakuwa na uwezo wa kujifanyia lolote na kwa hivyo ilimbidi mama kukaa pale nyumbani na kumtunza. Ingawa kakake na dadake mtoto kama huyu wangesaidia katika malezi, kazi kubwa ilikuwa ya mamao.

Jukumu la kulea mtoto ni jukumu linalohitaji uvumilivu mwingi. Mtoto mtukutu aliwafedhehesha wazazi wake na wakati mwingi alimfanya mamake kuchapwa na mumewe kwa sababu ya kosa la mwanaye. Mtoto mjinga kwa mujibu wa methali hii ni yule asiyeweza kufuata mbeko na maadili ya kijamii. Mtoto kama huyu aliwatia huzuni wazaziwe kwa sababu alijiingiza wakati mwingi katika hatari au mambo ambayo yangewaathiri wazazi wake. Watoto waliokuwa na akili punguani pia waliwekwa katika tapo hili. Mtoto kama huyu alihitaji kuangaliwa daima ili asiingie katika hatari yoyote. Kazi hii ilikuwa ya mama. Mbali na haya, mtoto aliyetenda vitendo viovu au vilivyolete madhara aliwaletea wazazi wake hasara ya kulipa fidia. Mwanamke katika mkabala huu anatazamwa kama asiye na uwezo wa kukabiliana na matatizo yanayomkumba hasa matatizo yanayohusiana na malezi. Kwake njia ya kujiauni kutokana na mchafuko huu wa hisia ni kupitia kitendo cha kulia. Wanasoshiolojia wamethibitisha kuwa hii ni njia mojawapo wa kumpatia mhasiriwa afueni. Hata hivyo njia hii si mwafaka katika kutatua matatizo yanayomkumba mtu. Mwanamke alipaswa kuchukua hatua madhubuti za kutatua matatizo yake. Tatizo lililoko ni kuwa mwanamke alikuwa na nafasi haba ya kutoa maamuzi kuhusu mambo yaliyomzunguka. Alihitajika wakati mwingi kutafuta ushauri kutoka kwa mumewe.

5.3.8 Haro ni ya muka uri ihii.

(Tafsiri)

Vita haviishi kwa mwanamke mwenye wavulana

Vita vinavyozungumziwa ni magombano au sintofahamu inayoweza kusababishwa na watu kutoelewana. Katika jamii ya Wakikuyu, wavulana ambao hawajatahiriwa bado wanajulikana kwa vita na kufanya mambo maovu. Ndio maana wavulana kama hawa walikatazwa kwenda kwa wakwe wakati wa kupeleka posa kwa sababu huenda wakatenda mambo ya aibu. Katika kusisitiza mtazamo wa wanajamii hawa kuhusu wavulana, wavulana hawa walipigiwa methali ifuayo-:

'Ihii citithiaga uthoni'

Wavulana ambao hawajatahiri hawapaswi kwenda kwa wakwe

Kwa wakwe ni mahali palipotakikana kuheshimiwa. Watoto wa kiume ni tofauti na wa kike.

Katika kulelewa kwao, watoto wa kike walielimishwa kuwa wao wanastahili kuwa wapole na watulivu. Wasichana waliofanya tabia kama vile kupanda juu ya miti waliitwa '*Wanja kihii*'. Hii ina maana ya msichana aliyekuwa na tabia kama za wavulana. Kuna zile tabia zilizokuwa zikitarajiwa kutoka kwa wavulana na vilevile kutoka kwa wasichana. Uchokozi ulihusishwa sana na Wavulana.

Ujamiishaji wa watoto wa kike umeonyeshwa kuwa tofauti kabisa na ule wa wale wa kiume. Mtoto wa kike amelelewa kwa njia inayomwonyesha kuwa anapaswa kuwa mpole, mnyenyekevu na aliye tayari kutumikia. Hii ndio maana vita na magombano hayakutarajiwa kutoka kwa watoto wa kike. Nafasi hii aliyotengewa mwanamke tangu utotoni inamtayarisha kuikubali hali yake ya utumishi anapokuwa mtu mzima. Hali hii iliyokubalika na jamii inazima uwezo unaoweza kuweko ndani ya mwanamke na badala yake inaotesha mbegu ya kukubali kuongozwa, kuchokozwa na hata kutumikishwa. Mwanamke aliyeenda kinyume na matakwa haya ya jamii alionekana kama muasi na vituko vyake vilielezwa daima na wanajamii. Ingawa methali hii inaeleza kuhusu vita na mafarakano kati ya watoto wa kiume, inatubainishia pia kuwa haya ni mambo yaliyotarajiwa na jamii. Kinyume chake ni kuwa mwanamke anastahili kuwa mpole na mnyenyekevu tangu utotoni tofauti na ilivyo kwa mwanamme.

5.4 Methali zinazolenga kazi

5.4.1 Mundu muka na kioje ni undu umwe

(Tafsiri)

Mwanamke na kiwete ni sawa

Kiwete ni mtu yeyote aliye na ulemavu wa namna fulani. Kulingana na Wakikuyu wenyewe, ulemavu huu waweza kuwa unaonekana au uwe hauonekani. Mwanamke alitazamwa kama asiye na nguvu za mwili na hivyo kushabihishwa na kiwete. Katika jamii hii, kiwete au mtu aliyekuwa na ulemavu wa aina yoyote hakuruhusiwa kwenda vitani. Wanawake vilevile hawakuruhusiwa kwenda vitani au kufanya kazi zilizokuwa na hatari fulani kama vile kuwinda. Walemavu sawa na wanawake hawakuruhusiwa kufika kwenye shina la mkuyu ambapo kafara ilikuwa ikitolewa.

Walibakia hatua kadhaa kutoka mahali pale na kazi yao kubwa ilikuwa kupokezana sala na wale wanaume waliokuwa wakitoa kafara ile.

Methali hii ilitumiwa kuwaonya wanaume dhidi ya kuwaingiza wanawake kwenye hatari au kuwaumiza .

Hata hivyo jamii ya Wakikuyu iliwatazama wanawake kama wenye upungufu fulani. Badala ya kuwaona wanawake kama walio tofauti kimaubile na wanaume, waliwaona kama wiliopungukiwa na hivyo kuwekwa kwenye tapo moja na walemavu.Sababu kuu ya kufanya hivi ilikuwa ili kuwafanya wanawake kuhurumiwa.

Ibainike kuwa katika jamii hii, kazi za sulubu zilitekelezwa na wanaume. Tukichukulia mfano wa ukulima, mwanamume, alishiriki katika ufyekaji na ulimaji wa kichaka mara ya kwanza. Hii kulingana na jamii hii ndiyo iliyokuwa kazi ngumu. Alifanya hivi kwa madai kuwa uvunjaji ardhi kwa mara ya kwanza ni jambo ngumu. Ingawa hii ni kweli uvunjaji huu au ulimaji huu hufanyika mara moja. Baada ya hii mwanamke alihitajika kushika usukani na kuhakikisha kuwa konde lake lina mimea na limelimwa vizuri mwaka baada ya mwingine.

Hali hii imekaririwa na mwalimu Julius Nyerere (1983:3) katika Lugano (1989: 108) anaposema:

> "Mwanamke wa sehemu za mashambani huanza kufanya kazi kabla ya jua kuchomoza mpaka baada ya jua kutua katika mwaka mzima. Mapato ya kazi yake ni chakula wanachopanda, nguo na vitu vingine ambavyo bwana zao wameamua kuwapa"

Hii ni idhibati ya kutosha ya kuonyesha kuwa mshabaha huu haulengi ndipo. Ingawa methali hii ilinuiwa kuwalinda wanawake kutokana na zahama, ilitumiwa kuwashushia hadhi wanawake kutokana na ukweli kuwa hawakuruhusiwa kushiriki katika shughuli hii muhimu ya kidini. Udhaifu wa mwanamke unapigiwa chuku sana na methali hii. Ingawa ni ukweli wa kimaumbile kuwa mwanamke hana nguvu nyingi akilinganishwa na mwanamume, udhaifu ule haupaswi kushabihishwa na ule wa mlemavu. Lengo kuu la Wanaufeministi ni kupigana na hali hii ambayo inaonyeshwa na wanajamii kama kaida ya kimaumbile. Jamii ya Wakikuyu imeendelea kushadidisha imani hii kupitia kwa methali zinazomsawiri mwanamume kama aliye na chembe ya nguvu za kiungu. Mfano mzuri ni kama vile:

'Anake ni cienyu cia Ngai.'

Vijana wa kiume ni sehemu moja ya Mungu.

Imani hizi zinakuwa kasumba inayokoleza kudunishwa kwa mwanamke. Cha kushangaza ni kuwa imani hizi zimepata makao katika akili za wanawake wenyewe. Ingawa hawakupendezwa na jambo hili, wasailiwa wa kike walikiri kuwa ndivyo walivyojamiishwa.

5.4.2 Atumia matithiaga ita

(Tafsiri)

Wanawake hawaendi vitani.

Vita vinavyozungumziwa hapa ni vita baina ya makabila. Zamani Wakikuyu walikuwa wakishiriki vita na makabila yaliyowazunguka kama vile Wamaasai na Wakamba. Mvulana alipotahiri alikabidhiwa mshale, upinde na mkuki. Ala hizi zilitumika katika vita na katika usasi. Wanawake hawangeweza kushirikishwa vitani kwa sababu ya udhaifu wa miili yao. Kazi ya mwanamke ilikuwa kutunza watoto na mumewe pamoja na kufanya kazi zingine za nyumbani. Kazi iliyohusiana na vita na ambayo mwanamke aliruhusiwa kufanya ni kuwapikia waliokwenda vitani na kuwaimbia waliposhinda. Yamkini ndio maana kuna methali katika jamii ya Wakikuyu iliyosema kuwa vita vya wanawake havihitaji utakaso wa mbuzi.

'Haro ya atumia ndiri horohio'

Methali hii inatusawiria picha ya mwanamke aliye dhaifu kiasi kwamba hawezi akaipigania jamii yake. Jamii hii inamwona mwanamke kama aliyeumbwa akiwa dhaifu. Kutokana na jambo hili mwanamke alihitajika kubakia nyumbani na kufanya kazi ambazo hazikuhitaji nguvu nyingi za mwili. Huu ni ukweli uliokubalika katika jamii nyingi za Kiafrika kama anavyosema Ndungo (1998).

Ukosefu huu wa nguvu sawa na za mwanamume ulimfanya mwanamke kupuuzwa. Hakuwa anapewa nafasi ya kutoa maoni yake hasa pale ambapo jamii ilikuwa inapanga uvamizi. Methali hii inatufunulia tofauti ya kimajukumu kati ya wanawake na wanaume. Lililowaepuka wahenga katika jamii hii ni kuwa kulikuwa na wanawake waliokuwa na uwezo wa kupigana sawa na wanaume. Wanawake kama hawa wangeifaa jamii zaidi kama wangepewa fursa ile ya kushiriki katika vita.

5.4.3 Mundu muka ndatumagwo thiiri-ini

Tafsiri

Mwanamke hatumwi kwenda kudai deni

Wakikuyu walikuwa na namna maalum ya kudai deni. Njia hii ilipaswa kuhakikisha kuwa wanajamii waliishi kwa amani na masikizano. Mtu alipokosa kutimiza ahadi yake ya kulipa deni (*thiri*) mwenye kudai alitengeneza pombe iliyotokana na miwa na kumpelekea mdeni wake. Kitendo hiki kilinuiwa kumshawishi mwenye deni kulipa kile alichodaiwa. Alipokosa kulipa baada ya tendo hili, mdai alitafuta wazee wawili aliowatuma kupeleka pombe kwa yule mdeni kwa mara nyingine.

Tendo hili lisipofua dafu, yule mwenye kudai deni alifikisha malalamiko yake kwa wazee wa baraza (*kiama)* wazee hawa waliamua siku ya kusikiswa kwa kesi ile. Uamuzi wa wazee (*kiama*) ulizingatiwa na hakuna mwanajamii yeyote ambaye angedhubutu kukiuka amri yao. Mwanamke alionekana kama kiumbe dhaifu ambaye angeweza kudhuriwa kwa urahisi iwapo pangetokea vita. Mwanamke alilindwa na jamii kutokana na kazi kama hizi ambazo zinaweza kuwa hatari kwake. Wazo linalompata mtu anapoisoma methali hii ni kuwa mwanamke anathaminiwa.

Wazo la kumtazama mwanamke kama asiyekuwa na uwezo wa kutekeleza baadhi ya kazi imeibuliwa na Imbuga (1988) kupitia mhusika Kezia anaposema :-

> Kezia :...ndio, kumbuka ukweli haulali njiani. Kiti cha mwanamume si cha makalio ya mwanamke.Aminata anapaswa kujua hivyo (uk 35)

Taswira tunayochorewa hapa ni ya mwanamke aliye dhaifu kutokana na maumbile yake na hivyo asiyeweza kutekeleza baadhi ya kazi. Methali hii inamsawiri mwanamke kama mtu spesheli anayepaswa kulindwa na jamii kutokana na hatari. Hata hivyo hatari kubwa iliyomkabili mwanamke si ya kughilibiwa na wadeni bali ni ya kutumikishwa na ya kutoshirikishwa katika halmashauri za kutunga sheria. .

5.4.4 Mundu utaumagaraga augaga no nyina urugaga wega

(Tafsiri)

Mtu asiyetembea hufikiria ni mamaye pekee ajuaye kupika

Mama ni mtu wa maana sana katika maisha ya mtu. Kazi ya mama katika jamii ya Wakikuyu ilikuwa kutunza na kuwapikia watoto na pia kuhakikisha kuwa mumewe ameshiba. Mwanamke aliposhindwa kutekeleza majukumu haya aliadhibiwa na hata kurudishwa kwa wazazi wake. Zamani katika jamii hii, wanaume hawakuruhusiwa kupika au kuingia jikoni. Kile ambacho waliruhusiwa kupika ni '*ngarango*' (Nyama za mafutamafuta zilizopikwa kwa makusudio ya kuchanganywa na damu ili ziweze kutengeneza aina ya soseji zijulikanazo kama '*mutura*'.

Methali hii ilitumiwa kuwaonyesha wanajamii na hasa wanaume kuwa wanapaswa kutembea ili waone jinsi ambavyo watu wengine walikuwa wakiendesha mambo yao. Kuwatembelea watu wengine kulimfanya mwanajamii kujifunza mambo mageni ambayo yangemfaa.

Methali hii inatudhihirishia jukumu alilotengewa mwanamke wa Kikuyu. Ingawa jamii nyingi za Kiafrika zinazozingatia itikadi ya kuumeni zilitazama jukumu la kupika kama ni janibu ya wanawake pekee, jukumu hili lilitumiwa kama msingi wa kumfunga mwanamke nyumbani. Jamii ya Wakikuyu ilikuwa jamii iliyothamini ukulima. Hivyo baada ya mwanamke kushinda siku mzima kondeni, alihitajika kuhakikisha ya kwamba familia yake itapata chakula. Wanawake wanapewa majukumu mazito kama vile kulima na kukidhi mahitaji ya chakula ya familia nzima. Mwanamke alilaumiwa wakati familia ilikumbwa na njaa iliyosababishwa na uzembe. Hii ni kwa sababu Wakikuyu huamini kuwa ,ili kuridhisha mtu, lazima kwanza utosheleze mahitaji yake ya tumbo. Wao husema kuwa;

'*Mwana mwega no nda.*'

Mtu aliyeshiba ni mtulivu.

Mwanamume aliishi kwenye nyumba maalum iliyoitwa *'thingira'*. Kule ndiko mwanamke alihitajika kupeleka chakula baada ya kupika. Iwapo mwanamume huyu ana zaidi ya mke mmoja (jambo ambalo lilikuwa la kawaida sana miongoni mwa Wakikuyu), wote walihitajika kupeleka chakula mle *'thingira'*. Alipokila na kusaza, mwanamume aliwaita wanawe wa kiume ili wale chakula kilichobakia.

Kazi alizozifanya mwanamke shambani na jikoni zilimnyima nafasi ya kushiriki kikamilifu katika shughuli muhimu kama vile utungaji sheria na uamuaji kesi. Maeneo haya yangemsaidia kudhihirisha ustahilivu na hekima yake.

Hali hii ilimfanya yeye kuendelea kutumikishwa kwani hawakuwa na nyenzo ya kutolea malalamiko yao kama kikundi. Tetesi za binafsi ziliishia kualika adhabu na kwa hivyo ingewabidi kuungana wakiwa wengi ili kupaaza sauti yao.

Mwanamke kama kiumbe cha kukidhi mahitaji ya chakula ya jamii ni taswira inayoendelezwa na methali nyingi katika Jamii ya Wakikuyu. Kama mama mlezi, alikuwa hana budi kujitumikisha kwani asipofanya hivi familia yake ingepatwa na baa la njaa.

5.4.5 Muici na mundu muka atigaga kieha akua

(Tafsiri)

Aliyeshirikiana na mwanamke katika kuiba hubakia na wasiwasi hadi wakati atakapofariki

Kuiba ni kule kuchukua kitu cha mtu bila idhini yake. Wizi ulijulikana katika jamii ya Wakikuyu hata ingawa haukuwa umefikia kiwango cha wizi unaoendelea sasa. Wakikuyu waliamini kuwa kulikuwa na familia zilizojulikana kwa wizi. Wanajamii walitahadhari sana walipohusiana nao. Msichana kwa mfano hangeruhusiwa kuolewa katika familia hizi na vilevile mvulana hangeoa kule. Wezi hawa waliiba vitu vidogovidogo. Kitu cha thamani ambacho wangeiba ni mbuzi.

Wakikuyu walikuwa wameamini kuwa ukiiba au kutenda jambo la siri na mwanamke lazima angekusaliti. Wanawake walionekana kuwa na umbeya na kwa hivyo hawakuweza kuficha siri zao. Jambo lingine ni kuwa ilikuwa rahisi kumshawishi mwanamke iwapo unataka kitu kutoka kwake.

Methali hii ilitumiwa kuwaonya wanaume dhidi ya kuwafunulia wanawake siri zao kwa sababu wangewaeleza marafiki zao. Jambo hili liliaminika kiasi kwamba wanaume wengi walikuwa wanapanga mipango yao bila kuwashirikisha wake zao. Jamii ya Wakikuyu inamtazama mwanamke kama kiumbe kisichoweza kuweka siri. Hii ndio maana anayeshiriki wizi naye huhofia daima kusalitiwa. Hii ilimfanya mwanamke wa Kikikuyu kutohusishwa katika mipango iliyohusu mbari nzima, hasa ikiwa mipango hii ilihusu uvamizi au kesi. Hakushirikishwa sawa na mvulana asiyetahiriwa kama inavyobainishwa na methali ifuatayo:-

'*Muici na kahii atigaga kieha giakua*'

Anayeshirikiana na *'kihii'* (mvulana asiyetahiri bado) katika wizi huishi na wasiwasi wa kusalitiwa hadi atakapokufa.

'Kihii' ni dhama inayotumika kimadharao kurejelea mvulana ambaye hajatahiriwa. Wavulana wa umri huu walijulikana katika jamii ya wakikuyu kama wasio na adabu na wanaoweza kusababisha balaa mahali popote. Jukumu lao kubwa katika jamii lilikuwa ni kuchunga. Uovu wao ulitiliwa chuku mno kiasi cha kupigiwa methali ifuatayo:-

'Ihii citithiaga uthoni'

kumaanisha kuwa wavulana hawapaswi kishirikishwa wakati wa kupeleka mahari au kutembelea wakwe. Ifahamike kuwa wakwe ni watu waliotaadhimiwa sana. Watu walichukua tahadhari zote kuhakikisha kuwa wamedumisha heshima na wakwe zao. Ilihofiwa kuwa iwapo wavulana watahusishwa, huenda wakawakosea adabu wakwe na hivyo kuvunja heshima iliyostahili kulindwa kwa ghera. Wanawake basi waliwekwa kwenye kumbo moja na wavulana hawa. Hili ni dhihirisho kuwa wanawake walishushiwa hadhi. Jamii hii inamchukulia mwanamke kama msaliti. Picha ya juu juu tunayoipata kuhusu mwanamke ni kwamba dhamiri yake haimruhuzu kijihuzisha na visa vya jinai. Akifanya hivyo basi roho yake haitatulia hadi pale atakapokiri yale makosa.

Wazo hili linaenda sambamba na yanayotokea katika jamii ya Wakuria. Kulingana na Wachege (1992) mwanamke hakuruhusiwa kuzungumzia vita ambavyo mumewe anashiriki. Kwa sababu hii, mwanamke hakufahamishwa lolote kuhusu vita hivi asije akashawishika kumsaliti kwa maadui.

5.4.6 Nyamacucu kanua ni koinagirwo ithigi

(Tafsiri)

'*Nyamacucu*' ni bora kuufunga mdomo wako

Nyamacucu ni mwanamke aliyekuwa na udaku mwingi. Methali hii ina maana sawa na iliyotangulia.litumiwa kuwashauri wanawake wasipayuke ovyo ovyo na wajaribu kuhifadhi siri.

Katika jamii ya Wakikuyu, mwanamke alikuwa na jukumu muhimu la kuitunza familia yake. Alifanya hivi kwa kujibidiisha shambani ili azalishe chakula cha kutosha kuikimu jamii na kuwafadhili wageni.

Shamba lilitazamwa kama jukwaa ambamo mwanamke alidhihirisha bidii na umakinifu wake. Aliyeshindwa kufanya kazi vizuri shambami aliitwa *'kihunguiyo'* yaani asiye na thamani. Isitoshe, mvulana alipovutiwa na msichana fulani, kwanza alichunguza jinsi msichana huyo alivyofanya kazi shambani. Aliwatuma marafiki zake kujificha karibu na eneo alilofanyia kazi msichana yule ili kuona kama kazi yake ni kuegemea mpini mchana kutwa. Marafiki hawa walipeleka habari kwa mwenzao kuhusu ufaafu wa binti yule.

Yalikuwa mazoea ya wanawake kuwaalika wenzao ili wasaidiane katika kazi hii ya kupanda, kupalilia mimea au kuvuna. Wakati wa shughuli hizi, ilikuwa kawaida ya wanawake kusimulia walichokisikia au kukiona. Baadhi ya hadithi hizi zilikuwa uvumi tu au masengenyo kuwahusu watu fulani katika jamii. Wakati mwingine visa vilivyosimuliwa vilikuwa vya ukweli lakini vikapigiwa chuku. Habari hizi wakati mwingine zilimfikia mwenye kusengenywa na hapo kusababisha mtafaruku na sintofahamu kati ya msengenyaji na msengenywaji. Wanawake wengine waliishilia kutoa siri za wengine na kueleza kuhusu mahusiano ya unyumba kati yao na waume zao. Huu ulionekana kama udaku na hivyo kupigiwa methali hii. Wamaume walihusika na kazi ambazo zilikuwa hazihitaji ushirikiano wa watu wengi kama vile kuchunga na kutengeneza ua . Kwa sababu hii walinusurika kutokana na lawama ya umbeya. Hata hivyo hapakukosekana mmoja au wawili waliotoa siri za wengine au kusengenya. Licha ya haya jamii haikutoa hukumu au wosia kwao katika umbo la methali. Mwanamke ndiye aliyeonekana kuwa nguli wa kilimilimi. Jambo hili linatilia shaka haki inayotendewa mwanamke na jamii. Hii ni kwa sababu licha ya kujibidiisha mchana kutwa ili kuikimu jamii, jambo ndogo kama masengenyo linatia dosari uzuri wote huu.

Tafiti zilizofanywa zinadhihirisha kuwa lawama dhidi ya mwanamke ni jambo ambalo limesakini sana katika jamii nyingi za Kiafrika. Mfano kamili ni ule wa methali ya Kikisii isemayo:-

'Abakungu nabaya nememwa yabasaririe .'

Yaani wanawake ni wazuri lakini umbeya unawaharibu.

5.4.7 Mutumia ndaturaga mutwe

(Tafsiri)

Mwanamke hapaswi kupasua kichwa cha mbuzi.

Uchinjaji wa mbuzi ulifanywa mara kwa mara katika jamii hii hasa wakati wa hafla mbalimbali za kijamii. Wanaume ndio waliokuwa na jukumu la kuchinja. Wanawake walikaa mbali na eneo hili kwani wakati mwingi mbuzi hawa walichinjiwa malishoni. Mwanamke hangeruhusiwa kupasua kichwa cha mbuzi kwa sababu huo ulikuwa mwiko. Kichwa cha mbuzi kilitayarishwa kwa kuchomwa manyoyaye. Baada ya kufanya vile kichwa hiki kilipasuliwa vipande vinne na kisha kikachemshwa ili kupata mchuzi. Wanaume ndio waliofanya kazi hii . Kazi ya wanawake ilikuwa ni kuchemsha kichwa hiki. Wakati mwingi mbuzi walichinjiwa malishoni na kuchomewa kuko huko. Sehemu zilizostahili kupikwa na wanawake zilipelekwa nyumbani baada ya wanaume kushiba. Wanawake walitengewa kazi ambazo hazihitaji nguvu nyingi. Ndio maana utawasikia Wakikuyu wakisema kuwa kinachomshinda mwanamume Kimekwishasukwasukwa-

'Kirema arume ni kigariure'

Methali hii kama iliyotangulia katika sehemu ya 5.4.1, inatuibulia ukweli kuwa wanawake walikuwa na kazi zao maalum zilizoamuliwa na maumbile yao. Ingawa hili ni jambo lililokubalika katika jamii nyingi, hali hii ilitumiwa kuwanyima wanawake fursa ya kushiriki kikamilifu katika kazi fulani fulani.

Mburu (2005) anasema yakwamba kuna nyakati ambapo wanaume waliamua kuwachinja mbuzi wakiwa malishoni. Baadaye waliwasha moto na kuwachomea mbuzi hawa kuko huko malishoni. Wanaume walizila nyama hizi hadi wakashiba. Ni baada tu ya kushiba ndipo walipokumbuka kupeleka masazo nyumbani ili yaliwe na wanawake na watoto. Jambo hili lilimfanya mwanamke kuonekana kama aliyetengewa kazi za sulubu tu bila kushirikishwa kikamilifu katika ugawanyaji wa matunda ya kazi hizo.

5.4.8 Nyoni ya njamba ndiri gitara

(Tafsiri)

Ndege wa kiume hajengi kiota.

Ni jambo lililo wazi kuwa ndege wengi hujenga kiota ili wapate mahali pa kutagia mayai na kujikinga na baridi pamoja na hatari zingine. Wakikuyu huamini kuwa ujenzi huu hufanywa na ndege wa kike kwani ndiye atakayetaga mayai. Yule wa kiume huwa kama mgeni mahali pale.

Wanaume walishabihishwa na ndege huyu wa kiume kwa sababu hawakuyajua mambo ya nyumbani kwao hasa yanayohusiana na chakula na malazi. Mwanamke alikuwa na jukumu la kutengeneza boma lake. Kazi ya mwanamume ilikuwa nje ya nyumba. Mfano wa kazi hizi ni kutengeneza ua, kuchunga mifugo na kuwinda. Hata ingawa wanaume wale waliishi katika *'thingira'* (nyumba maalum ya mwanamme wa Kikikuyu), nyumba ile ilinadhifishwa na mwanamke.

Kiota ni mahali ambapo ndege alipata pumziko baada ya kazi zake za mchana kutwa za kujitafutia riziki. Vivyo hivyo binadamu huhitaji makao au mahali ambapo ataweza kurejea na kupata maliwazo. Hii huenda ndio sababu iliyowafanya wahenga kuamba kuwa ng'ombe anapovunjika guu malishoni hujikokota hadi zizini akasaidiwe. Kwa hivyo zizi, kiota au nyumbani ni mahali ambapo mhusika yeyote anaweza kupata kitulizo cha mambo mengi. Wanaume waliojihusisha na ukahaba waliitumia methali hii kuhalalisha vitendo vyao viovu. Hii ndio maana jamii haikutoa hukumu kali kwa wanaume waliokuwa na tabia kama hizi, kinyume na walivyomfanyia mwanamke.

5.4.9 Mbu ya arume itikaguo ni athamaki

(Tafsiri)

Mbiu ya wanaume huitikiwa na wafalme

Kutokana na methali hii ni dhahiri kuwa unyende wa mwanamume haukuwa wa kawaida. Hii ni kwa sababu mfalme ni mtu mashuhuri sana ambaye hashughulikii maswala madogo madogo. Wanaume walifunzwa kuvumilia uchungu hasa wale waliokwishatahiriwa. Haikuwa kawaida kuwasikia wanaume wakipiga kite. Waliofanya hivi walirejelewa kimadharau kama 'wanawake'. Hivyo iliaminika kuwa kilio cha maumivu kutoka kwa kundi la wanaume kilitokana na jambo lisilo la kawaida. Hivyo ni mfalme pekee aliyedhaniwa kuwa angeweza kuleta afueni au suluhisho la jambo kama hili. Ifahamike kuwa jamii hii haikuwa na kitengo cha watu waliojulikana kama wafalme kama tunavyowafahamu leo hii.

Utawala uliendelezwa na wazee waliochaguliwa kwa misingi ya umri, tajiriba na hekima yao. Wazee hawa waliunda halmashauri ya wazee (*kiama)* ambao walikuwa na uwezo wa kutoa maamuzi kuhusu maswala fulani katika jamii.

Methali hii ni njia ya kuupigia chuku ukuu wa wanaume. Ni bayana kuwa methali hii imekusudiwa kuendeleza fikra kuwa wanaume katika jamii hii wana uwezo zaidi ya wanawake.

Kinaya ni kwamba kelele za wanawake zinaonekana kama jambo la kawaida hasa kwa sababu jamii hii inahalalisha kuadhibiwa kwa mwanamke alipokosa au hata alipodhaniwa na mumewe kuwa amekosa. Jamii hii huendeleza mafunzo haya kwa vijana baada ya tohara.Wasichana hufunzwa kuwatii wanaume na kuwatumikia. Mhusika Regina katika riwaya ya Rosa Mistika ukurasa wa 17 anamshauri bintiye kumpigia magoti babaye anapompelekea chochote. Hali hii ya kuamini kuwa mwanamume anamfuata Mungu katika msururu wa wenye uwezo imepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa mafunzo kama haya. Huku mwanamume akikwezwa ngazi ya kijamii, mwanamke alibakia kuwa chini yake katika maswala mengi.

5.5. Methali zinasohusu utawala

5.5.1 Gutiri mucii uri kahii utakarigwo mutwe.

(Tafsiri)

Nyumba iliyo na mtoto wa kiume lazima itapikwa kichwa cha mbuzi, kondoo au ng'ombe wakati mmoja

Wanaume na watoto wa kiume ndio waliokuwa na jukumu la kuchoma kichwa cha mbuzi au kondoo alipochinjwa. Mtoto wa kiume alishuhudia sherehe nyingi kwa sababu ya ukweli kuwa alibakia palepale nyumbani tofauti na wa kike. Alimsaidia babake kufanya mambo mengi na alipitia hatua nyingi zilizohitaji sherehe.

Hivyo mtoto wa kiume alipendelewa sana na jamii ya Wakikuyu na ndio maana alipozaliwa alikaribishwa kwa vigelegele vitano. Alipotahiri alipewa mbuzi na kijisehemu cha shamba na babake. Mbuzi hawa walipozaana na kuongezeka alikuwa na uhuru wa kuwaalika marafiki zake washerehekee kwa kumchinja mbuzi mmoja. Baada ya kuchinja mbuzi hawakuwa na budi kupasua kichwa kwa sababu hili lilikuwa jukumu la mwanamume.

'*Kahii*' ni dhana inayotumiwa kumrejelea mvulana ambaye hajatahiriwa bado. Katika jamii ya Wakikuyu,wavulana walithaminiwa sana. Mvulana alipozaliwa, wanawake

wanaomsaidia mama kujifungua pamoja na mkunga walihitajika kupiga vigelegele vitano. Hii ni tofauti na ilivyokuwa msichana alipozaliwa. Msichana alipigiwa vigelegele vinne. Hii ilinuiwa kawafahamisha waliokuwa kule nje pamoja na baba mzazi jinsia ya mtoto aliyezaliwa. Kutokana na kitendo hiki, ilikuwa dhahiri kuwa mwana wa kiume alirundikiziwa thamani kubwa tangu alipozaliwa.

Wasichana walitazamwa kama wageni waliotembea mle kwa kipindi kifupi kisha waondoke. Pindi walipovunja ungo na kupashwa tohara waliozwa na kuonekana kama watu waliozihama familia zao milele.

Kwa mintarafu hii, wavulana walionekana kama wanachama wa kudumu wa familia zao. Wazo hili lilisakini katika jamii nyingi za Kiafrika. Ukweli huu unabainishwa na waandishi wengi wa fasihi. Mhusika Chahe katika tamthilia ya *Mke Mwenza* (Chacha, 1982 :10) anasema;

> "Sijali hayo. Tumaini langu ni kuwa nioapo mke wa pili, ataweza kunizalia mvulana, mrithi wa mali yangu. Mvulana atakayeendeleza jina la ukoo wetu"

Kama walivyofanya Wakikuyu, mhusika huyu anaona suluhisho la kumpata mtoto wa kiume likiwa katika uoaji wa wake wengi. Wakati wote mwanamke alionekana kama ndiye aliyekuwa na kasoro. Jambo hili linakinzana na ukweli wa kisayanzi kwamba ni mwanamume anayesababisha haya.

Kwa sababu sherehe nyingi miongoni mwa jamii ya Wakikuyu, zilihusisha uchinjaji wa kondoo au mbuzi, methali hii ilitumiwa kabainisha ukweli kuwa mvulana atakuwa mshiriki katika sherehe na tamasha zote zitakazoendelea katika familia ile. Atakuwa na uhuru wa kufurahia na marafiki zake katika sherehe hizi. Nafasi ya mwanamke wakati mwingi ilikuwa ya kushuhudia yanayoendelea. Hali hii katika jamii ya Wakikuyu inaenda sambamba na tunachoibuliwa na Kezilahabi katika Rosa mistika.

Tunamwona Regina, mkewe Zakaria akitusiwa na kubughudhiwa kwa sababu ya kumzalia watoto wa kike peke yao. Mwandishi anatufunulia madhila ya Regina anaposema:-

> "Regina alikuwa na watoto watano wasichana wote wazuri kama yeye.
> Matumaini yake ya kukaa pamoja na watoto hao kama

alivyoambiwa na bwanake yalikuwa katika mimba ya miezi mitano alivyokuwa nayo sasa." (uk 8).

Kasumba ya kuwa mtoto wa kiume ni bora zaidi kuliko wa kike ilikolezwa akilini mwa wanajamii tangu pale utotoni. Mtoto wa kiume alipozaliwa wanawake wenyewe walimpigia vigelegele vitano. Mtoto wa kike alipigiwa vigelegele vinne. Hii bila shaka ilidhihirisha kuwa mtoto wa kiume alipendelewa zaidi. Mapendeleo haya yalidumaza uwezo wa mwanamke wa kutumia vipawa alivyojaliwa na Maulana.

5.5.2 Mundu muka ndoragagwo

(Tafsiri)

Mwanamke hapaswi kuuliwa

Kuanzia zamani za kale, wakati wa mababu zetu ilikuwa kosa kumuua mwanamke. Hii ni kwa sababu mwanamke ana roho nyepesi na kwa hivyo hana uwezo wa kudhuru. Wakati jamii hii ilipokuwa ikipigana na Wamaasai wanawake na watoto hawakuwa wakiuawa kwa sababu wao ni viumbe wasiokuwa na nguvu za kupigana. Methali hii ilitumiwa kuwaonya wapiganaji dhidi ya kuwaua wanawake, mtoto au hata kilema. Kama wangethubutu kufanya hivyo, Wakikuyu waliamini kuwa wangekumbwa na hatari fulani au hata kushindwa vitani.

Wanatazamwa kama kundi la watu dhaifu. Huu ni ukweli unaokiriwa na methali kama:

'*mundu muka na kioje ni undu umwe*'.

(mwanamke na kiwete ni sawa).

Huku ni kumsawiri mwanamke kama aliye dhaifu kiasi kwamba hawezi kupigania haki yake. Dosari iliyoko kwenye makisio haya ni kuwa jukumu analotekeleza mwanamke haliwekewi uzito unaotakikana. Uchunguzi uliofanywa na Umoja wa Mataifa kulingana na Mies Bennholdt na werlhof (1998: 150) inadhibitisha kuwa wanawake hufanya thuluthi mbili (2/3) ya kazi zote ulimwenguni, hupata asilimia kumi (10%) ya mapato yote na humiliki asilimia moja (1%) ya nyenzo za uzalishaji mali. Ni dhahiri kutokana na tarakimu hizi kuwa mwanamke ana nafasi duni ya kujiendeleza. Ingawa anafanya kazi kubwa, faida ya yanayopatikana kutokana na jasho lao hayamnufaishi ipasavyo.

Sababu nyingine ya kutomuua mwanamke ni kuwa ametunukiwa jukumu la kuendeleza kizazi. Akitazamwa kwa miwani hii basi itakuwa haki kudai kuwa methali hii inainua hadhi ya mwanamke kwa kumlinda kutokana na hatari anazoweza kkukumbana nazo.

5.5.3 Bara ya aka ndiri horohio

(Tafsiri)

Vita vya wanawake havihitaji kutolewa mbuzi.

'Horohio' ni sadaka ya utakaso aliyotoa mtu baada ya kumjeruhi mwingine. Sadaka hii ilikuwa ya mbuzi ambaye ilitolewa kwa aliyejeruhiwa ili kuondoa mawaa yaliosababishwa na umwagikaji wa damu. Wanawake walidumisha sana hasira zao. Husemekana kwamba hasira za wanaume hazidumu kama zile za wanawake. Hii inatokana na ukweli kuwa wanawake waliweka kisasi kiasi kwamba walipokutana na maadui wa zamani, walifufua uadui ule. Hii ilisababisha kuzuka kwa vita vya maneno au vya mwili. Kwa sababu ya udhaifu wa mwili vita hivi vilikuwa vya kugaragazana arthini na kwa hivyo hakukuwa na umwagikaji wa damu. Kwa sababu hii wanawake hawangepewa kazi iliyohitaji nguvu nyingi.

Tunatambulishiwa kuwa vita baina ya mwanamke mmoja na mwingine havikuwa hatari kama vile vya wanaume. Wanjiku (2005) anadai kuwa ilikuwa nadra kwa wanawake kupigana. Mara nyingi walipigana vita vya maneno tu. Hasira zilipozidi, wanawake wale waligaragazana arthini na ala ya pekee waliyoitumia katika vita hivi ni meno. Kwa sababu hii hawakuweza kutiana majeraha makubwa. Ifahamike kuwa katika jamii ya Wakikuyu, mtu alipomjeruhi mwingine kwa kusababisha umwagikaji wa damu, alihitajika kumtoa mbuzi awe kama sabuni ya kumsafisha na kumtakasa aliyejeruhiwa. Iliaminika kuwa wanawake walikuwa dhaifu na kwa hivyo hata walipopigana hawangeweza kutiana majeraha na kwa hivyo hakukuwa na haja ya mbuzi wa utakaso.Ifahamike kuwa katika jamii hii, mtu alipomuua mwanamume, alihitajika kulipa fidia ya mbuzi mia moja. Ikiwa aliyeuliwa ni mwanamke, mtu huyo alihitajika kulipa fidia ya mbuzi thelathini. Ni bayana kutokana na methali hii kuwa ilikuwa nadra kwa mwanamke kuua. Methali hii licha ya kumbeza mwanamke inamsawiri kama binadamu anayedhamini uhai na asiye na uwezo wa kudhuru wenzake.

5.5.4 Nguku ya mutumia niimenyaga gugikia no iroraga mukanye wa ya njamba.

(Tafsiri)

Kuku wa kike hutambua kunapokucha lakini huutazama mdomo wa jimbi

Ni jambo linalojulikana kuwa ni jogoo awikaye. Wakikuyu waliamini kuwa ukitaka kwenda mahali mapema itakubidi umweke jimbi karibu na mahali utakapolala ili akuamshe. Sababu ni kuwa alijua kulipokucha. Ingawa wa kike alijua kulipokucha hana uwezo wa kuwika.

Hawa sio kuku wanaozungumziwa hapa ila ni binadamu. Wakikuyu wanadai kuwa Mungu alikuwa amempa mwanaume hekima ya hali ya juu na kwa hivyo aliweza kuyatambua mambo kabla ya mwanamke. Kwa sababu hii mwanamume alikuwa na jukumu la kumwonyesha mwanamke jinsi ya kutenda mambo. Ilikuwa ni sharti kwa mwanamke kufuata amri za mumewe.

Wakikuyu kama jamii iliyozingatia itikadi ya kuumeni ilimtunuku mwanamume madaraka yote ya kuamua lila na fila. Kabira (1994:77) akimnukulu mhojiwa wake katika jamii ya Wakikuyu anasema-:

> "Mwanamke anapaswa kunyamaza ili apewe maelekezo. Mwanamke hastahili kupewa uhuru. Wanapopewa uhuru huwarusha waume zao nje. Huwezi kumpa nyoka kidole ili kuona kama atakiuma. Mwanamke ni kama huyo nyoka mwenye sumu na kwa hivyo huwezi kucheza naye"
> (Tafsiri yangu)

Mwanamke katika jamii hii hakuwa na uhuru wa kufanya uamuzi kuhusu maswala fulani hata wakati ilikuwa dhahiri kuwa jahazi linakwenda mrama. Alimsubiri mumewe ili kujiepushia dhawabu ya kiboko. Yeye alibakia pale kuonekana wala si kusikika. Ruganda (1992:49) akilizungumzia jambo hili anasema:-

> " Mzee kabla ya ukoloni katika Afrika alikuwa bwana wa mazingira aliyoyadhibiti ili kuyakimu mahitaji yake mwenyewe. Uwepo wake ulihusishwa na uadilifu na uwezo mkubwa ."
> (Tafsiri yangu).

Waweru (1990 :5) katika riwaya yake ya *Judy the Nun*, Judy ambaye ni mhusika mkuu anapanda ngazi kutoka kiwango cha mwalimu wa shule ya msingi hadi kuwa mhadhiri wa chuo kikuu.

Anakumbana na Joel Kamati ambaye anamuona kama duni kwake. Anasema kuwa hawezi kujadili chochote naye, kwani wanaojadiliana sharti wawe wa hadhi sawa.

Hili ni dhihirisho la taasubi ya kiume iliyosakini katika jamii nyingi za Kiafrika.

Katika riwaya ya Nuru ya Bhoke Gesimba, mamake Bhoke anaibua wazo lili hili. Anapoulizwa maoni yake kuhusu elimu ya mwanawe anadai kuwa yeye ni kama trela na hivyo kama gari linavyotegemea uongozi wa kichwa, ndivyo hata yeye ananvyotegemea maelekezo ya mumewe. Maoni yake ni kuwa trela haliwezi kutangulia kichwa kinachoivuta, kwani kufanya hivyo itakuwa kualika ajali mbaya.

Methali hii inamshushia hadhi mwanamke kwa kumchora kama anayetegemea uamuzi wa mwanamume. Hata ingawa ana uwezo wa kutambua mambo, uhuru wa kuchukua hatua au kudhihirisha jambo unatokana na mwanamume.

5.5.5 Aka matiigagwo ndundu

(Tafsiri)

Wanawake hawahifadhi siri

Usiri wa hali ya juu ulihitajika hasa pale ambapo wazee wa baraza walikutana ili kujadili jambo au kuamua kesi. Wakati wa mabaraza haya ya wazee wanawake hawakuruhusiwa kuwepo kwa sababu walionekana kama wangetoa nje siri za wazee. Wanawake walijulikana kwa kufanya kazi kwa ushirikiano. Wakati wa kufanya kazi hizi kulikuwa na umbeya mwingi ambao wakati mwingine ulisababisha kukosana kwao. Wanawake walionekana kuwa na maneno mengi kiasi kwamba maneno yao yalisemekana kuwa hayafaidi ila kupoteza (*matiri cia ndiiro no cia nyiniko*). Ingawa kuna methali isemayo kuwa Wakikuyu hujua kuficha shibe ila si maneno, wanawake walikuwa ndio waliokithiri.

Wanaume waliyaficha mambo yao na ilikuwa nadra kusikia kuwa mwanamume amesengenya fulani. Ndio maana utawasikia wazee wakisema kuwa mambo ya wazee yamepembuliwa-

'Cia athuri ni thure'

Methali hii inatusawiria mwanamke ambaye hawezi kuhifadhi siri. Kutokana na sifa hii wanaume walichelea kuwapa wanawake siri zao na hivyo kutowashirikisha katika mabaraza na kamati zao za kujadili kesi au mambo yaliyomfika mwanajamii.

Picha inayoibuliwa hapa ni ya mwanamke domokaya asiyeweza kuaminiwa hasa katika uhifadhi wa siri.

5.5.6 Atumia moi kuhitha ndia matiui kuhitha uhoro

(Tafsiri)

Mwanamke hujua kuficha chakula lakini hajui kuficha habari

Wanawake walijulikana kwa udaku wao. Wakati mwingi wanawake walifichwa mambo kutokana na ukweli kuwa wangesambaza habari hizo na kusababisha kukosana kwa watu. Hii ndio sababu kuu ya kudai kuwa wanawake hawajui kuficha habari.

Methali hii inamsawiri mwanamke kama bahili na mroho ambaye hawezi kumfadhili yeyote kwa chakula. Yuko tayari zaidi kumpa mgeni habari alizozisikia kuliko kumpa chakula. Ili kusisitiza hoja hii, Wakikuyu wana hadithi kumhusu mwanamke mmoja aliyejulikana kama *Wambimbi*. Mwanamke huyu inasemekana alikuwa mchoyo kiasi cha kutoweza kumfaidi sisimizi. Wakati mmoja alipokuwa akipika uji ,mgeni alibisha mlangoni pake. Kwa sababu hakutaka kumpa mgeni uji, aliamua kuuficha uji ule. Aliuepua kutoka jikoni kwa harakaharaka na kuuficha '*itara*' (Hapa ni darini mahali palipotengenezwa kwa minajili ya kuweka kuni mbichi ili zikauke). Baada ya kuuficha uji wake alimfungulia mgeni wake. Kwa sababu alikuwa ameuweka ule uji kwa haraka, sufuria haikuwa imewekwa vizuri. Sufuria ile iliteleza na kumwangukia. Uji wote ule ulimmwagikia na kumchubua mwili kwa sababu ulikuwa ungali moto.

Hadithi hii ilitumiwa kushadidia imani kuwa wanawake wana uchoyo.

Kwa upande mwingine methali hii hutumiwa kuonyesha kuwa wanawake hawajui kuweka siri. Kwa kuzingatia imani hii wanaume katika jamii hii walichelea kutoa siri zao kwa wake zao kwa hofu kuwa wangewafunulia siri zile watu wengine ambao hawakupaswa kuzijua. Hii ilikuwa sababu kubwa ya kumnyima nafasi ya uongozi.

5.6 Methali zinazolenga umilikaji mali

5.6.1 Mundu muka ni mutuga kwene.

(Tafsiri)

Mwanamke hana faida kwa mbari yao.

Methali hii inatuonyesha kuwa mwanamke hana manufaa kwa mbari yake lakini huenda kufaidi mbari tofauti. Mtoto wa kike alipozaliwa, Imani hii imejikita katika methali ifuatayo-:

'Mutumia ndenjagirwo bui kwao'

Ni muhali kwa mwanamke kuishi kwao hadi akaota mvi ilikuwa bayana kuwa si wa kudumu kule kwa sababu siku moja ataondoka na kwenda kuolewa. Methali kuwa mwanamke haishi kwao mpaka akapata mvi ni kiashiria cha jambo hili. Mtoto wa kike alijua kuwa siku moja ataondoka alikozaliwa na kujiunga na familia nyingine ambayo hana uhusiano wa kidamu nayo. Ataenda kutumikia watu wengine na wema wake au uovu wake utajulikana na jamaa nyingine.

Mtoto wa kike hakudekezwa sana kama yule wa kiume kwa sababu ya jambo hili. Wale wa kiume walipigiwa methali kuwa wao ndio ua la boma lao. Kutokana na jambo hili watoto wa kike hawakupewa urithi wowote. Wale wa kiume walitengewa sehemu yao ya urithi. Sehemu ya urithi huu walipewa walipotahiri. Hali hii inakaririwa na waandishi na watafiti wengi. Okindo (1995) akimnukuu Ndege (1992) anasema-:

> "Kijadi watoto wa kike hawakuridhi mali kutoka kwa wazazi wao. Msichana alizaliwa ili aolewe na hili halikuwa swala la kimjadala. Ingawa alikuwa nyumbani kwa baba yake alichukuliwa kwa tahadhari kama kwamba alikuwa mgeni ambaye siku moja ataondoka. Wakati mwingine wasichana waliolewa mapema katika umri pengine wa miaka kumi na minne hivi. Aliishi kwa miaka michache nyumbani kwa babake kuliko kwa bwanake. Hii ndiyo iliyokuwa sababu hasa ya baba kutompa sehemu ya arthi au ng'ombe"

Kama ilivyo katika jamii nyingi za kiafrika, mwanamke anapoolewa huhama kwao na kwenda kuishi katika familia ya mumewe. Jambo hili humfanya kuonekana kama mgeni katika familia anamozaliwa. Ni kutokana na jambo hili ambapo Wakikuyu wanasema kuwa mwanamke huwanufaisha watu wengine ila si jamaa yake. Kutokana na mtazamo huu, wanawake katika jamii hii hawana haki ya kudai urithi kutoka kwa babao. Mali aliyo nayo babao husemekana kuwa ni ya watoto wa kiume.

Jambo hili linamweka mwanamke katika njia panda. Hii ni kwa sababu kwao hakubaliki na vilevile kwa mumewe yeye ni mgeni. Hali hii ilikuwa imekubalika miongoni mwa wanajamii hawa kiasi kwamba ndoto ya kila msichana ilikuwa kupata mchumba na kupata watoto. Mwanamke hakuwa na chake.

Kipande cha shamba alichogawiwa mumewe na baba mkwe ndiyo iliyokuwa raslimali yake kubwa. Hii ni kwa sababu aliitumia kuzalishia chakula cha kuikimu familia yake.

Kupitia kwa methali hii mwanamke anatazamwa kama mkimbizi asiye na haki ya kumiliki chochote kwa wazazi wake na pia kwa mumewe. Alichokuwa na uhuru wa kudai kuwa ni chake ni watoto wake pekee.

5.6.2 Mundu muka na iguru itimenyagirwo

(Tafsiri)

Ni vigumu kumuelewa mwanamke kama ilivyo vigumu kutabiri mvua.

Mwanamke alishabihishwa na mbingu kwa sababu ilikuwa vigumu kumjua kwa uyakinifu. Ni kama yale mawingu ya mvua ambayo huwa mengi wakati fulani na hivyo kumfanya mtu adhani kuwa kutanyesha na kisha yanasukumwa na upepo na kupotea. Wanawake wanajulikana kwa kununa hasa wanapokasirishwa. Jambo hili linatokana na silika. Jambo lingine linalofahamika kuhusu wanawake ni kuwa wao huyumbishwa kwa haraka na mambo ambayo yanaonekana madogo kwa wanaume. Pia alidanganyika kwa urahisi. Kutokana na mambo haya wanawake walionekana kama wasio na msimamo.

'Iguru' katika muktadha huu ni dhana inayorejelea mawingu ya mvua.

Ingawa uwepo wa mawingu ni kiashiria cha kuja kwa mvua, inatambulika kuwa kuna uwezekano wa mawingu yale kusukumwa na upepo na hivyo kutonyesha.

Kupitia kwa methali hii, mwanamke amehusishwa na hali hii ambayo haitabiriki wala kubashirika. Anaonekana kuwa ni kiumbe ambaye ni kigeugeu. Tabia hii kulingana na Wakikuyu humfanya mwanamke kutoeleweka. Dosari iliyoko hapa ni kwamba haijaelezwa bayana ni maeneo yapi katika maisha ya mwanamke ambayo yamemfanya yeye kutoeleweka. Jambo hili halipatikani katika janibu za Wakikuyu pekee. Kupitia kwa maandishi ya kifasihi ukweli huu unafunuliwa. Mfano mzuri ni wa riwaya ya Said A. Mohamed, Tata za Asumini. Mwandishi anamsawiri mhusika Asumini kama msichana asiyejua akitakacho katika maisha licha ya kuwa amesoma hadi kufikia chuo kikuu. Hulka yake imenyongwanyongwa na kitendawili cha kutojitambua, jambo ambalo lilimwelekeza katika kutaka kujiua.

Ifahamike kuwa katika jamii ya Wakikuyu, mwanamke alihitajika kunyenyekea na kutopayuka ovyo ovyo.

Jina lake '*Mutumia*' ni nauni inayotokana na kitenzi '*tumia*' chenye maana ya nyamaa. Huenda basi katika jitihada ya kufikia mizani hii iliyowekwa na jamii, anajipata katika matata ya kubatizwa ' asiyebashirika'.

Kinachowaepuka wanajamii hawa ni kwamba kunyamaa kwa mwanamke ni utiifu tu wa kaida zilizowekwa na jamii pana ya Wakikuyu.

Kinaya ni kwamba anapozungumza na kueleza maoni yake kwa njia ya wazi anabatizwa '*kanya ka uhoro*' (kibuyu cha maneno) na anaponyamaa anaabiwa kuwa habashiriki.

5.6.3 Aka na ngombe matiri ndugu

(Tafsiri)

Wanawake kama vile ng'ombe hawastahili kuchezewa

Kulingana na mila na utamaduni wa Wakikuyu, sehemu ya mahari ijulikanayo kama '*ngurario*' (sehemu ya mwisho ya mahali iliyoitishwa na wazazi wa msichana) ilipopelekwa, msichana huyo alikuwa sasa amekubalika kabisa katika mbari ya mumewe. Kabla ya kufikia hatua hii, familia ya mwanamume tayari ilikuwa imekwishatoa mali mengi kwa akina msichana. Kwa sababu hii ilikuwa vigumu mno kwa mwanamke katika hatua hii kutoka kwa mumewe.

Sababu kuu ya kushabihishwa na ng'ombe ni kuwa ng'ombe walikuwa wa thamani kubwa na hawakupatikana kwa urahisi. Ilimbidi mwenye kumtaka ng'ombe kuwa na mali ili kuweza kugharimia bei yake. Ng'ombe walibadilishwa na mbuzi na nafaka kutoka kwa Wamaasai. Wakati mwingine Wamaasai waliwashambulia Wakikuyu na kuwachukua ng'ombe kama ngawira. Hivyo ng'ombe walilindwa sana. Mshabaha uliopo ni kuwa mwanamke alipolipiwa mahari alikuwa sasa ni mojawapo wa mali ya mwanamume na kwa hivyo hakutakikana kuchezewa na wanaume wengine.

Wazo tunalolipata hapa ni kuwa mwanamke anatazamwa na jamii hii kama binadamu aliyepungukiwa. Anamithilishwa na kiumbe kisichoweza kujiamulia mambo yake. Kwa sababu hiyo, anaonekana kama asiye na uwezo wa kufanya lolote bila kuelekezwa na mumewe. Thamani yake inalinganishwa na ile ya ng'ombe. Anakuwa kama mojawapo wa mali inayomilikiwa na mwanamume. Maadamu amelipiwa mahari, yeye si tofauti na ng'ombe aliyenunuliwa kwa fedha.

Mila na desturi za jamii hii kama zinavyobainika kutokana na methali zinamlazimisha mwanamke kuwa chini ya mwanamume hasa kupitia kwa asasi ya ndoa.

Methali hii inaibua wazo kuwa mwanamke kama mali ya mwanamume yuko chini ya mamlaka yake na kwa hivyo anaweza kumtendea lolote alitakalo.
Imani hii inashabihiana na ya Wayahudi. Katika Mwanzo 19:4-8, tunaelezwa kuwa Lutu aliwatoa binti zake kwa wanaume wa Sodoma ili waridhishe uchu wao. Lutu aliwatoa kama vibadala vya wanaume wawili waliokuwa wakitakikana na Wasodoma hawa . Pia katika Waamuzi 19 : 22 –30 kuna kisa cha mwanamume aliyetoa mke wake kwa Walawi. Mwanamke huyu alibakwa na kuteswa hadi akafa. Methali hii inamsawiri mwanamke kama kiumbe aliye na thamani kubwa na ambaye hapaswi kuchezewa.Hata hivyo lugha iliyotumika inatia dosari thamani hii.

5.6.4 Iri gukura iriagwo iguku ni aka

(Tafsiri)

Ng'ombe akizeeka huliwa nundu na wanawake

Wakikuyu walipohitaji kumchinja ng'ombe au mbuzi walitafuta wanaume wawili au zaidi ili waweze kuwaangusha na kuwadhibiti mifugo hawa. Hii ni kwa sababu wanyama hawa walikuwa na nguvu nyingi. Wanawake walijulikana kuwa dhaifu. Hii ndio maana waliambiwa kuwa ng'ombe ambaye wangeweza kumla ni yule aliyekuwa amezeeka sababu ikiwa kwamba alikuwa dhaifu.
Methali hii ilitumiwa kuonyesha kuwa mwanamume alipozeeka alishindwa kuwakabili watesi wake na hata kuwadhibiti wake zake. Methali hii ilitumiwa kuwakumbusha wanaume waliokuwa wakatili kwamba wakati mmoja watazeeka na uwezo wao utapungua.

Ng'ombe anapozeeka hutazamwa kama asiyeweza kumdhuru yeyote. Hii ni kwa sababu ya kupoteza baadhi ya meno yake na hivyo kutokuwa na uwezo wa kutafuna nyasi. Matokeo yake huwa kudhoofika kwa afya yake kutokana na kupungua kwa kiasi cha nyasi anazoweza kutafuna. Mwanamke kwa majibu wa wanaozingatia itikadi ya ubabeume ni viumbe dhaifu kimaumbile.

Jambo hili huwafanya kudhibitiwa na wanaume. Wazo linalojitokeza katika methali hii ni kuwa wanawake wanawekwa katika kumbo moja, wawe majagina au dhaifu. Ifahamike kuwa kuna wanaume wasio na nguvu za mwili na hivyo wanapaswa kuwekwa katika tapo la wala nundu. Ni kweli kuwa kimaumbile wanawake hawakutunukiwa nguvu kama za wacheza miereka lakini wana sifa fulani mzuri zinazoendeleza jamii. Kenyatta (1939:180) anakiri kwamba wanawake katika jamii ya Wakikuyu ndio hasa walezi wa jamii na bila wao, katika muktadha wa jamii ya Wakikuyu hakuwezi kuwa na maisha ya jamii.

Hili bila shaka ni jambo linalomstahilia mwanamke heshima kubwa. Hata hivyo anatawaliwa hadi pale ambapo mwanamume anazeeka na hivyo kupoteza uwezo wa kutawala.

5.6.5 Mureranirwo na ihii ni athararaga

(Tafsiri)

Msichana anayelelewa pamoja na wavulana hudumaa

Wavulana wasiotahiri bado katika jamii ya Wakikuyu walijulikana kwa tabia zao mbaya. Walijulikana kwa tabia ya kupanda miti kama nyani na kuwinda. Wasichana nao walikuwa watulivu na wapole. Msichana aliyelelewa pamoja na wavulana aliathirika kwa vile alichokozwa na kutumikishwa. Methali hii imetumia kitendo cha kudumaa kama kiashiria cha mwanamke kukosa mahitaji fulani. Wavulana waliweza kupigania vitu kama vile chakula na vitu vingine. Jambo ambalo msichana hangeweza. Methali hii ilitumiwa kuwashauri wanajamii washirikiane na watu waliokuwa na uwezo sawa. Sababu kuu ni kwamba wakishirikiana na wale walio na uwezo mkubwa watabidika kufanya mambo kama wao na huenda wakaumia.Yamkini ndio maana Waswahili walisema anayeshindana na ndovu msalani hupasua kibofu chake.

'Ihii' ni dhana iliyotumiwa kuwarejelea wavulana ambao walikuwa bado kupashwa tohara. Iliaminika kuwa wavulana hawa walikuwa na tabia mbaya na uchokozi mwingi. Hawakutofautisha kaida na kawaida na kwa sababu hii hawakuruhusiwa kushiriki katika shughuli nyingi zilizohitaji umakinifu. Jambo hili linatiliwa nguvu na methali isemayo:-

'Ihii citithiaga uthoni'

Wavulana hawashirikishwi katika shughuli za kupeleka mahari kwa wakwe.

Kiambishi i katika neno '*ihii*' hutumika kimakusudi kuleta wazo la madharau kwani kiambishi hiki huambatanishwa na majina ya vitu visivyo na uhai. Kipindi hiki cha maisha ni kipindi kilichoambatanishwa na mambo mengi maovu. Kazi kubwa iliyotengewa wavulana wa umri huu ilikuwa kuchunga. Wasichana kwa upande wao walikuwa na jukumu kubwa la kusaidia mwanamke kutekeleza kazi za nyumbani. Methali hii inamchora mwanamke kama binadamu mtulivu na anayedhurika anapowekwa pamoja na wanaume walio na uwezo uliozidi ule wake.

5.6.6 Giathi githaragio ni gaka kamwe

Tafsiri

Soko laweza kutibuliwa na mwanamke mmoja

Sokoni ni mahali ambapo watu wengi hukutanika kwa madhumuni ya kununua au kuuza. Mtu anayeweza kuharibu utaratibu wa kongamano kama hili bila shaka ana uwezo mkubwa. Methali hii inamsawiri mwanamke kama binadamu aliye na uwezo huu wa kuweza kuvuruga utaratibu fulani. Ingawa kwa juu juu methali hii inaonekana kama inayomtukuza mwanamke, kuna kinaya kikubwa. Kinaya kilichopo ni kuwa uwezo aliorundikiziwa mwanamke ni ule wa kuharibu, kuchafua na kutatiza.

Wanaume katika jamii ya Wakikuyu hutumia methali hii kama kizingizio cha kumnyima mwanamke nafasi ya kujua mengi yanayowahusu wanaume. Hawapewi nafasi ya kuathiri maamuzi ya halmashauri za wazee (*kiama*), wala kuongoza sherehe. Ifahamike kuwa katika sherehe za kutoa kafara wanawake hawakuruhusiwa kukaribia eneo linalotumika kama madhabahu. Wanaume ndio walioshika hatamu za utoaji wa kafara chini ya mti wa '*mugumu*'.Wanawake walibakia hatu kadhaa kutoka eneo la shughuli hii. Aidha, ngano nyingi katika jamii hii, hasa zinazohusu wakewenza huwaonyesha wanawake kama mazimwi na nduli wanaowasumu watoto wa wake wenzao na kuwahanithisha waume zao.

Wazo linaloibuliwa na methali hii ni kuwa wanawake wana uwezo ndio, lakini uwezo huu hautumiwi kwa manufaa ya jamii. Hii kwa hakika ni picha chakavu ya mwanamke.

Wazo hili linaenda sambamba na methali ya kihehe isemayo:

*'Akagulu ndamaa, ilidako ng'ambakwa'(*Madumulla:1994)

(Kiguu ni ng'ombe jike, tako ni ng'ombe ndume)

Ieleweke kuwa miguu huwa na jukumu kubwa la kutembea katika zile harakati za kutafuta lishe ili hali tako husubiri tu kunawirishwa kwa kilichopatikana. Miguu pia hupata uchafu mwingi wakati wa kutafuta chakula.

5.7 Muhtasari wa matokeo ya uchanganuzi kwa jumla

5.7.1 Maudhui.

Maudhui yaliyojitokeza katika methali zilizochanganuliwa yalijikita katika nyanja tano. Nyanja hizi ni ndoa, malezi, kazi, utawala na umilikaji mali.

Asilimia 31.8 ya methali zilizochanganuliwa ziliibua maudhui yanayohusiana na ndoa. Ndoa miongoni mwa Wakikuyu ni asasi inayomhitaji mwanamke kuwa chini ya mwanamume. Mahari anayolipiwa mwanamke inatumika kama leseni ya kumtumikisha na kumwadhibu mwanamke anapomkatalia jambo mwanamume. Thamani yake katika ndoa ilipimwa kwa mizani ya urembo, ubikira na uwezo wake wa kuzaa. Mwanamke aliyekosa uwezo wa kuzaa alihusishwa na laana na uchawi. Kwa sababu hii alikosa mtu wa kumuauni alipohitaji msaada. Alionekana kama mwenye kasoro na aliyestahili hukumu ya kutengwa na kuishi maisha ya upweke. Hali hii ilimwelekeza katika uke wenza.

Maudhui ya ulezi na utunzaji wa familia yalijitokeza katika asilimia 18.2 ya methali zilizochanganuliwa. Nyanja hii inampa mwanamke sifa nzuri. Ingawa watafiti wengi wanaiona hali hii kama inayomfunga mwanamke nyumbani, Wakikuyu wanakiri kuwa hili ni jukumu teule linaloenda sambamba na maumbile yake. Silika za kiuke alizotunukiwa mwanamke na Maulana zinakuwa mwongozo katika kutekeleza jukumu hili. Malezi ya mtoto wa kike yalimwelekeza na kumtayarisha kuwa mke, mama na mwanajamii mpole mwaminifu na mtiifu kwa mumewe.

Maudhui ya kazi yalijitokeza katika asilimia 20.5 ya methali zilizochanganuliwa. Maudhui haya yanawasilisha wazo kuwa mwanamke ni myonge na asiyeweza kufanya kazi ngumu na hatari.

Kupitia kwa ujamiishaji, mwanamke alifundishwa kuwa kazi yake kubwa ni ya kulisha na kutunza familia yake.

Kinyume na ilivyo katika jamii nyingi, wanaume katika jamii ya Wakikuyu walilishwa na wake zao ambao walibidika kushinda mchana kutwa shambani.Kazi ambazo wanawake walitengewa ni kulima shamba, kulisha familia, kunadhifisha makazi na mazingira yao, kulea watoto na kutunza mume. Kwa mujibu wa methali zilizoangaziwa, kazi ambazo hawakupaswa kufanya ni kuchinja mifugo, kuwinda, kushiriki katika vita, kujenga nyumba na kwenda kudai deni. Kazi hizi zilichukuliwa kuwa hatari kwa wanawake na zile ambazo hazikuwa hatari zilihitaji nguvu nyingi

Maudhui ya utawala yalijitokeza katika asilimia13.6 ya methali zilizochanganuliwa. Ilibainika kuwa mwanamke alinyimwa nafasi ya uongozi kwa sababu ya udhaifu wake wa mwili. Dhana hii inapigiwa chuku sana kiasi kwamba anamithilishwa na walio na uwezo wa chini sana kama viwete. Upungufu huu pamoja na wazo kuwa ana umbeya mwingi unamnyima mwanamke nafasi ya kushirikishwa katika utawala kupitia kwa zile halmashauri nne zilizokuwa nguzo ya utawala katika jamii ya Wakikuyu.

Maudhui ya umilikaji mali yalichukua asilimia 15.9 ya methali zilizochanganuliwa. Ilidhihirika kuwa mwanamke hana chake wala kwao kwani wazaziwe humtumia kama chambo cha kunasia mali kwa njia ya mahari. Wanawake katika jamii hii hawakurithi chochote kutoka kwa wazazi wao. Iliaminika kuwa wao ni wapita njia na kwa hivyo vyao vya halali watavipata kwa waume zao. Mali iliyopatikana kutokana na bidii yao shambani ilikuwa ya waume wao na alipokaribia kufa aliwaachia watoto wake wa kiume.

Kwa muhtasari, jedwali lifuatalo linaonyesha msambao wa maudhui yaliyojitokeza.

5.7.1.1 Msambao wa nyanja zilizoshughulikiwa

Nyanja	Idadi	Asilimia
Ndoa	14	31.8%
Kazi	9	20.5%
Malezi	8	18.2%
Umilikaji mali	7	15.9%
Utawala	6	13.6%

Kutokana na jedwali hili , inabainika kuwa maudhui ya ndoa yalijitokeza katika asilimia kubwa ya methali zilizochanganuliwa (31.8%). Maudhui yaliyofuatia ni yale ya kazi yaliyokuwa na 20.5%. Malezi yalichukua 18.2%, umilikaji mali 15.9% na utawala13.6%. Maudhui haya yanatuelekeza katika sehemu ya nyanja.

5.7.2 Nyanja

Katika kitengo hiki, mtafiti aligundua kuwa nyanja za ndoa, malezi, kazi, utawala na umilikaji mali zilitumika kama asasi za kumgandamiza mwanamke katika jamii ya Wakikuyu. Methali zinazohusu ndoa zilimchukulia mwanamke kama bidhaa inayonunuliwa na mwanamume mwenye uwezo wa kulipa mahari. Jambo hili lilimfanya yeye kudhibitiwa na mwanamume na kupoteza utambulisho wake kama binadamu huru. Kutokana na ukweli huu, nafasi yake ya kutoa maamuzi kuhusu maswala yanayomzunguka ni finyu. Malezi yametumika kama jukwaa kwa mwanamke la kudhihirishia uvumilivu na ustahilivu wake katika kuchonga hulka ya wanajamii wachanga. Mwanamke anajitokeza kama mama mlezi aliyetayarishiwa jukumu hili na maumbile yake. Kutokana na haya, anakuwa na uhusiano mkubwa na watoto wake.Nyanja hii inamtukuza mwanamke. Nyanja ya kazi inadhihirisha ubaguzi wa kiuana. Mwanamke kutokana na maumbile yake anapewa nafasi finyu ya kudhihirisha uwezo wake. Anatengewa kazi zinazomfunga nyumbani. Nyanja za utawala na umilikaji mali zinampa mwanamke nafasi duni. Hashirikishwi kikamilifu katika maswala ya sheria. Mali yote iliyoko nyumbani pamoja na yeye mwenyewe anachukuliwa kuwa ni mali ya mumewe.

5.7.3 Lugha

Ilidhihirika wazi kuwa methali nyingi zilitumia lugha ya kumkashifu na kumbeua mwanamke. Msamiati kama vile kiwete, ng'ombe, chungu (kifaa), kuku na ndizi imetumiwa kumrejelea mwanamke. Ingawa matumizi ya maneno haya ni ya kitamathali, vifaa hivi havina thamani inayoweza kulinganishwa na thamani ya maisha ya mwanadamu.

Katika methali ambazo mwanamume ametajwa sambamba na mwanamke, mwanamume amepewa msamiati unaosheheni nguvu na uwezo zaidi, kwa mfano jimbi na mtamba. Lugha inayozua dhana ya utiifu, unyenyekevu na upole pia imetumika kumrejelea mwanamke.

5.7.4 Maana

Maana ya kijumla iliyojitokeza kuhusu usawiri wa mwanamke ni kuwa jina mwanamke linafasiliwa kwa mujibu wa nafasi yake katika jamii ya Wakikuyu. Neno hili liliambatanishwa na utiifu, binadamu wa jinsia ya kike aliye chini ya mamlaka ya mumewe au babake na mlezi wa watoto anayepaswa kukimu mahitaji yao ya chakula na kuwaelekeza katika mkondo wa tabia unaokubalika. Pia ni mtenda kazi za sulubu hasa shambani na mhifadhi wa nyumba kupitia kuinadhifisha. Vilevile ni mkosa kwao kwani alikozaliwa ni kituo tu cha kumsubiri mchumba na anapoolewa anatazamwa kama mgeni. Maana nyingine iliyojitokeza ni kuwa anatumika kama chombo cha kumzolea babake mali kupitia kwa mahari na pia mumewe kupitia kwa kuzalisha mimea shambani.

5.7.5 Taswira

Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni anayetegemea hifadhi na fadhila za mumewe katika ndoa. Ameonyeshwa kuwa mdaku, asiye na uwezo wa kutenda baadhi ya kazi muhimu na kumithilishwa na kiumbe dhaifu kimwili na kiakili. Mwanamke amesawiriwa kama asiyeweza kutunza siri . Aidha, alichorwa kama asiyeweza kudumisha urafiki kwani huwasaliti anaoshirikiana nao (5.4.5) Kwa mujibu wa methali zilizochanganuliwa, picha ya mwanamke imesambaratishwa na kuchakaishwa

na asilimia sitini na moja nukta nne (61.4%) ya methali zote ilhali zinazomtukuza zimechukua asilimi thelathini na nane nukta sita (38.6%).

Jedwali lifuatalo linaonyesha uhalisia huu.

5.7.5.1 Jedwali linaloonyesha hadhi ya mwanamke kwa mujibu wa methali zilizochanganuliwa.

Methali	**idadi**	**Asilimia**
Zinazomdunisha	27	61.4%
Zinazomtukuza	17	38.6%

Kutokana na jedwali hili, methali ishirini na saba au asilimia 61.4 zilionekana kumshushia hadhi mwanamke ilhali 17 au asilimia 38.6 zinamtukuza mwanamke.

SURA YA SITA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti ataeleza maswala muhimu yaliyoibuka kutokana na utafiti huu.Vilevile atagusia matatizo na ufanisi wa utafiti huu. Mwishoni ametoa mapendekezo kuhusu sehemu zinazohitaji utafiti zaidi.

6.2 Hitimisho

Ilibainika kuwa Wakikuyu hupitisha na kuwarithisha wanajamii wake thamani ambazo husimbwa katika lugha wanayoitumia. Methali zilizochanganuliwa ziliafiki ukweli wa nadharia tete ya kwanza (1.4.1) inayodai kuwa methali za Kikuyu humsawiri mwanamke kwa njia fulani inayomdunisha. Jedwali nambari 5.7.5.1 linaakisi hali hii. Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe dhaifu na asiyeweza kutekeleza baadhi ya majukumu. Imani hii inamnyima nafasi ya kushiriki katika utungaji wa sheria kwani hana nafasi ya uanachama katika halmashauri nne zinazoendesha maswala ya kisheria katika jamii ya Wakikuyu.

Imedhibitika pia kuwa methali hubainisha nafasi na majukumu maalum ya mwanamke katika jamii ya Wakikuyu. Jambo hili linaafiki nadharia tete ya pili (1.4.2). Ilidhihirika kuwa mwanamke amepewa majukumu mahsusi muhimu ikiwa ni kutunza mume na watoto, kunadhifisha makazi yake na kuzalisha chakula shambani kwa kutumia nguvu na jasho lake.

Mwanamke kama mama anakuwa na uhusiano wa juu sana na wanawe. Hali hii inashadidisha nadharia tete ya tatu inayosema kwamba methali huibua uhalisia wa mahusiano kwa mujibu wa uana katika jamii ya Wakikuyu. Katika jamii hii, utiifu wa mwanamke kwa mumewe au babake si jambo la mjadala mbali ni kaida. Mwanamke anayekiuka kaida hii hana budi kufunzwa adabu. Tangu pale anapozaliwa, mwanamke hufuata mkondo aliotayarishiwa na uana wake , jambo ambalo linamuwezesha kukubalika katika jamii. Uzoefu wa tajiriba hii miongoni mwa wanawake uliwafanya kuikubali hali yao na kuiona kama iliyoratibiwa na Maulana.Thamani hizi zinazopokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine huelekeza na kuathiri mahusiano kati ya wanajamii wa uana tofauti.

6.3 Matatizo aliyoyakabili mtafiti

Ilikuwa vigumu kupata wahojiwa waliobobea katika nyanja hii. Ilimbidi mtafiti kuwasaka wahojiwa wa rika la *Irungu* ambao walikuwa wametawanyika katika eneo kubwa. Ilimbidi mtafiti kutembea masafa marefu kwa miguu ili kuwafikia wahojiwa hawa hasa wale walioishi mbali na barabara.

Changamoto nyingine ilikuwa katika kutafsiri. Data iliyokusanywa ilikuwa kwa lugha ya Kikuyu. Hii ilibidisha utafsiri ufanywe kama sharti la kazi hii. Baadhi ya dhana tulizozipata zilikosa kisawe katika lugha ya Kiswahili. Hii ilisababisha kuwa na maelezo marefu ambayo huenda yasiibue maana iliyokusudiwa katika muktadha asilia. Hata hivyo mtafiti alijaribu awesavyo kuleta uwiano kati ya lugha chanzi na lugha pokezi kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa.

6.5 Mapendekezo

Kuna mambo muhimu yaliyodhihirika kutokana na utafiti huu. Mtafiti aligundua kuwa tanzu zingine za fasihi simulizi kama vile vitendawili na nyimbo zinahitaji utafiti zaidi. Kilichomvutia mtafiti ni kutambua kuwa Wakikuyu sawa na Waswahili walikuwa na mashairi na tenzi *(Marebeta na Gicandi)*. Hii ni mboji yenye rutuba inayohitaji utafiti zaidi.

Imani potovu zinazoibuliwa na baadhi ya methali zimepitwa na wakati na kwa hivyo wanajamii wa leo wana wajibu wa kutunga methali zitakazoshamirisha uhusiano kati ya wanawake na wanaume na kuimarisha ushirikiano. Wizara ya elimu inapaswa pia kuhakikisha yakwamba methali zilizo na muegemeo wa kiuana hazipati nafasi katika vitabu vinavyopendekezwa katika ufunzaji wa fasihi simulizi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa elimu ina nafasi muhimu katika kupalilia mitazamo ya wanajamii kuhusu maswala ya kiuana sawa na maswala mengine. Isitoshe, methali hutumika sana katika mazungumzo ya kawaida zikilinganishwa na tanzu zingine za fasihi simulizi.

Wanaotetea haki za wanawake wana wajibu wa kutalii maeneo tuliyoyajadili ili waweze kutafuta mikakati mwafaka ya kuleta usawa wa kiuana kati ya wanajamii hawa sawa na jamii nyingi za Kiafrika.

MAREJELEO

Akivaga, K. na Odaga, A.(1982). *Oral Literature*: A School Certificate, Heinemann, Nairobi

Austin, B. Kabira, W. & Okombo, O. (1994). *Understanding Oral Lirerature*. Nairobi University Press, Nairobi.

Barra, G. (1939). *1,000 Kikuyu Proverbs*. Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Brown, L. W (1981*). Women Writers in Black Africa.* Nestport, Connecticut, Greenwood Press.

Chacha, N. C (1982). *Mke Mwenza*. Heinemann Educational Publishers, Nairobi

Chesaina, C. (1987). *Women in African Drama: Representation and Role.* Phd Thesis, School of English, University of Leeds.

Chesaina, C. (1991). *Oral Literature of the Kalenjin*. Heinmann Kenya Ltd, Nairobi.

Coates, J. (1986). *History of Islamic Law*. The scholar Press.

Collins, H. P. (1991*). Black Feminist Though.* Chapman and Hall Inc. New York.

Eangleton, M.(1986*). Feminist Literary Theory.* Basil and Blackwell, New York

Elsestein, Z. (1979). *Capitalist Patriarchy and the case for Socialist Feminism.* Monthly Review Press, New York.

Engels, F. (1975). *The Origin of The Family, Private Property and State*. Pathfinder Press, Moscow.

Finnegan, R. (1970). *Oral Litrature in Africa*. Oxford University Press, Dar es Salaam.

Halliday, M.A. (1978). *Language as Social Semiotics: The Interpretation of Language and Meaning* .London.

Imbuga, F. (1988). *Aminata*. Heinmann Kenya Ltd. Nairobi.

Kenyatta ,J. (1978). *Facing Mount Kenya*. East African Educational Publishers, Nairobi.

Kezilahabi, E, (1971). *Rosa Mistica*. East African Literature Bureau, Nairobi

_____(1974). *Kichwa Maji*. East African Literature Bureau. Dar es Salaam.

Khasiani na Njiru (1993). *The Women's Movement in Kenya*. Association of African women for Reseach and Development (AAWORD),Nairobi.

Kihumbu, T. (1975). *The African Civilization*. Kenya Literature Bureau, Nairobi.

King'ei, G. K. (1982). *Uhakiki wa Methali za Kikamba kwa Kufuata Misingi ya Methali za Kiswahili*.Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Lugano, R. S .(1989*). Mwanamke Katika Riwaya za Kezilahabi.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mandulla, J. S. (1995). *Proverbs and Sayings: Theory and Practice*. Institute Of Kiswahili Reseach. University of Dar es Salaam.

Matteru, M. (1982). *" The Image of Women in Tanzania Oral Literature*" Makala katika Kiswahili. Toleo 49/2. Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.

Mbilinyi, A.D.na Omari, C. (1996). *Gender Relations and Womens Image in the Media.* Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Mbughuni, P. (1982). "*The Image of Women in Kiswahili Prose Fiction*" Makala katika Kiswahili Toleo 49/1 .Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam Salaam.

Mies, D. S. & werlhof, C. (1988). *Women: The Last Colony*. Zed Books Ltd, London .

Milroy, J (1987). *Observing and Analysing Natural Language*. Basil Blackwell, London

Mineke, S. (1989). *Sourse Of All Evil: African sayings on Women*. Phoenix Publishers, Nairobi.

Momanyi , C. (1998). *Usawiri wa mwanamke Mwislamu Katika Jamii ya Waislamu Kama Inavyobainika Katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mugo, E. N. (1982). *Kikuyu People: Brief Outline of Their Customs & Traditions*. Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Munene, W. A. (1995). *'Muramati Mugikuyu'*. East African Educational Publishers. Nairobi

Mule, K. (1991*). Swala la Mwanamke Katika Tamthilia ya Kiswahili: Waandishi wa Kike Katika Njia Panda.* Tasnifu Ya M.A Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mutegi, J.N. (1985). *Maendeleo ya Kimaudhui Katika Tamthilia Tano za Ebrahim N. Hussein*, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mworia, H. (1994) . *I, the Gikuyu and White Fury*. East African Educational Publishers, Nairobi.

Myampala, M. (1965).*Waadhi wa Ushairi*. East African Literature Bureau. Nairobi

Ndege, S. M. (1992)."*Gender issues and concerns in Meru oral narratives*"(A case study of Mitiine community) Makala yaliyowasilishwa katika warsha ya KOLA, Novemba 1992.

Ndungo, C .M. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria.*Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Ndungo, C. M. (1998). *African Oral Literature: A Case of Kikuyu and Kiswahili Proverbs.* P.H.D Thesis of Kenyatta University

Ngumbu, N. (1968). *Gikuyu Proverbs With English Translation.* Oxford University Press. Nairobi.

Njogu, K. S. (1987). *Maudhui Ya Mapinduzi Katika Riwaya za Visiwani Zanzibar.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nyerere, J.(1985). Utangulizi katika ,"*The Arusha Strategies for the Development of Women in Africa*". O.A.U.

Oduyoye, M. na Fabeila, V. (1988). *With Passion and Compassion, Third World Doing Theology*, New York.

Okindo, A. O. (1995). *Sura ya Mwanamke Katika Methali za Ekegusii.* Tasnifu ya M.A , Chuo Kikuu cha Egerton.

Otiende, J. E. & Karugu, M.A. (1991). *History and Government.* Heinmann Kenya Ltd. Nairobi.

Ruganda, J. (1992). *Telling The Truth Laughingly.* Kenya Litho Ltd, Nairobi.

Ruthven, K.K. (1984*). Feminist Lirerary Studies: An Introduction.* Cambridge University Press,London.

Randall, V. (1982). *Women and Politics: An International Perspective*, Macmillan Press Ltd, London.

Seitel, P.I. (1972). *Proverbs And The Structure of Metopher.* P.H.D Thesis, University of Pennsylvania, Ann Arbo Michigan

Senkoro, F.E.M.K. (1988).*Ushairi: Nadharia na Tahakiki*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

_____(1992). *Fasihi,* Dar es Salaam Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.

Syambo, B. & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi.* East African Educational Publishers, Nairobi

Thiong'o, T. (1971). *The River Between.* Heinmann Kenya Ltd, Nairobi.

Toiwo, O. (1984*). Female Novelist of Modern Africa.* Macmillan publishers, London

T.U.K.I, (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Oxford University Press. Dar es Salaam .

T.U.K.I, (1996). *English Kiswahili Dictionary.* Oxford University Press. Dar es Salaam.

Uvetie, E. (1976). *Utamu wa Lugha.* Kenya Literature Bureau. Nairobi.

Venkatarayappa, K. N. (1966). *Feminine Roles* . Sangam Press P.V.T. Ltd, Bombay.

Wachege, P. N. (1992). *African Women Liberation: A Mans Perspective.* Industrial Training Works Ltd. Nairobi

Wambura, S. K. (1990). *Nuru ya Bhoke Gesimba.* Ruvu Publishers Ltd, Dar es Salaam

Wamitila, K. W. (2001) *Kamusi ya Methali.* Longhorn Publishers. Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi:Istilahi na Nadharia.* Focus Books Publishers. Nairobi.

Waweru, P.M. (1990). *Judy the Nun.* Longman Kenya Ltd, Nairobi

Were, S.G. & Derek, A.W. (1968). *East Africa Through a Thousand Years.* Evans Brothers Ltd. Nairobi.

Wandera , S. P. (1996). *Usawiri wa mwanamke katika ushairi wa kiswahili 1800-1900* : *Uhalisia au ugandamizwaji*? Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

WAHOJIWA

Jumanne tarehe 1-3-2005, katika kijiji cha Rwaitira wilayani Thika.

Mahojiano yalianza saa nane na dakika ishirini hadi saa kumi na moja.Nilimhoji Kariuki wakiwa na wake we wawili-Joice na Penninah.

1. Kariuki wa Karanja
2. Joice Nungari
3. Penninah Wanjiru

Tarehe 2-3-2005 katika kijiji cha Rwaitira Wilayani Thika. Saa tatu asubuhi hadi saa nne na dakika kumi.

4. Anjelina Wanjiru

Tarehe 10,11 na 12 mwezi wa tatu nilimhoji Simon na mkewe phillis katika kijiji cha Ngano wilayani nyandarua.Niliwahoji pia Muthoni ambaye ni mjane na Mburu kutoka kijiji hicho hicho.

5. Simon N'gan'ga
6. Phillis Wanjiku
7. Muthoni wa King'ori
8. Peter Mburu

Tarehe 21-24 machiniliwahoji wafuatao katika kijiji cha Rironi wilayani Kiambu;

9. Jane Wanjiku
10. David Murote
11. James Mwaura

Tarehe 29 na 30 Machi nilimhoji Wairimu katika kijiji Cha Kerwa Wilayani Kiambu

12. Cecilia Wairimu

Tarehe 15 Aprili nilimhoji Jane katika kijiji cha Gatunyu wilayani Thika

13. Jane wa Kinuthia

Tarehe 19 na 20 Aprili Nilimhoji Wacera katika kijiji cha Rironi.Alikwa amehamia sehemu hiyo kutoka Mweiga Nyeri.

14. Wacera kiarie

Tarehe 118-21 May niliwahoji Nyokabi pamoja na wahojiwa wangu wa kwanzaKaranja Joice na Penninah katika kijiji cha Rwaitira.

15. Nyokabi Mwirigi

KIAMBATISHO I

MASWALI YA MAHOJIANO

Sehemu ya A

Maitu / awa nonyende kumenya Agikuyu metikitie maimire ku na ni a mari maithe mao ma mbere.

Maitu /awa ndirenda undaririe uhoro wa miikarire ya ugikuyu.Ndirenda kumenya itina iria mundu ageragira kuma aciarwo nginya agakua. Ningi niingienda ujire uhoro wa mambura maria mari kuo na ni andu ariku matongoragia na niki.

Tafadhali ningependa unijulishe imani ya Wakikuyu kuhusu asili yao, ni akina nani waliokuwa wazazi wao wa kwanza.

Ningependa pia unieleze kuhusu maisha ya mwanajamii wa Kikikuyu. Unielezee kuhusu hatua ambazo mwanajamii huyu alipitia kuanzia alipozaliwa hadi pale alipokufa.. Pia ningependa unielezee kuhusu sherehe walizokuwa nazo wakikuyu na ni nani alikuwa na jukumu la kuongoza sherehe hizi.

Sehemu ya B

1. *Riu maitu /awa noudaririe thimo ni kii?*
   Wakikuyu walichukulia methali kuwa ni nini?
2. *Thimo ni ciari na bata muturireini wa Mugikuyu?Bata wacio wari uriku*
   Methali zilikuwa na umuhimu wowote katika maisha ya Wakikuyu? Umuhimu huu ulikuwa upi
3. *Thimo ciatumagirwo mahinda mariku na ni kii giatumaga cihuthirwo mahinda macio na ti mangi?*
   Methali zilitumiwa nyakati zipi na kwa nini?
4. *Ni andu ariku matumagira thimo muno miario-ini? Uu ni kwonania ati andu a marika mamwe matingiahuthirire thimo?*
   Ni watu wepi waliotumia methali sana katika mazungumzo?Na je kwa nini wengine hawakuzitumia?

5. *(a) No ungweterena undaririe thimo iria ciarongoreirio mutumia?*
   Tafadhali nitajie na unifafanulie methali zilizowahusu wanawake.

(b) Nikii giatumaga mutumia arongorerio thimo ino na ti mundurume?

Kwa nini methali hii ilimhusu mwanamke na si mwanamme

6. *(a) Thimo ino yatumagirwo mahinda mariku?*

Methali hii ilitumiwa nyakati zipi?

(b) Mahinda maya mari na utiganu uriku na mahinda mangi ma uturo?

Nyakati hizi zilikuwa na tofauti ipi na nyakati zingine za maisha?

7 (a) Thimo ino ina ndumiriri iriku?

Methali hii ina maana gani?

8. Thimo ino yatumagirwo gutara kana kurunga uu

Methali hii ilitumiwa kushauri nani?

9. Mundu uyu eragwo uguo niki?

Kwa nini mhusika huyu aliambiwa vile

10. Mutumia niakumitio kana nianyarairwo ruriri-ini rwa Agikuyu?.

Mwanamke katika jamii ya Wakikuyu aliheshimiwa au la

11. Ni thimo iriku ungigweta cia gukumia mutumia na ni iriku cia kumunyararithia

Unaweza kunitajia methali zilizomtukuza mwanamke na zile zilizomdunisha.

12. Nikii giatumaga akumio kana anyararuo?

Ni nini kilichoifanya jamii kumtukuza au kumdunisha?

KIAMBATANISHO II

ORODHA YA METHALI ZILIZOCHANGANULIWA

(a)Methali zinazohusu ndoa

1. *Gutiri njamba ya mwera umwe*
2. *Murega arume omburagwo na njuguma*
3. *Aka eri ni nyungu igiri cia urogi*
4. *Wahira ihu wi kironda niwe ukagura*
5. *Muiritu mwega ahitukagira thome wa ngia*
6. *Njamba ya ndurume irundagwo ni aka*
7. *Aka a kwene ni irima iriku*
8. *Mutumia angikura atari mwana ndangiona wa kumutahira mai.*
9. *Mwanake wi na indo ndoihanaga*
10. *Atumia matiri rika*
11. *Muka uri mwana ndoraga.*
12. *Muka mucangacangi ndaagaga mwana*
13. *Mwari mweru ndaraguragirwo*
14. *Kwi ngatha na nyagacu*

(b) Methali zinazohusu malezi

1. *Karega nyina gatihonaga.*
2. *Kuguna mwana no ta kuguna nyina*
3. *Guciara kunaga irigu ngingo*
4. *Muiritu njong'I akiuhwo nyina athekaga na kamwena*
5. *Ndugu ya mwana imatagio ni nyina*
6. *Mwana mukigu aturagia nyina na maithori*
7. *Haro ni ya muka uri ihii*
8. *Mwana amenyagwo ni nyina*

(c) Methali zinazohusu kazi

1. *Mundu muka na kionje ni undu umwe*
2. *Atumia matithiaga ita*
3. *Mundu muka ndatumagwo thiri-ini*
4. *Mundu utaumagaraga augaga no nyina urugaga wega*

5. *Muici na mundu muka atigaga kieha akua*
6. *Nyamacucu kanua nikoinagirwo ithigi*
7. *Mutumia ndaturaga mutwe*
8. *Nyoni ya njamba ndiri gitara*
9. *Mbu ya arume itikaguo ni athamaki*

(d) Methali zinazohusu utawala

1. *Gutiri mucii uri kahii utakarugwo mutwe*
2. *Mundu muka ndoragagwo*
3. *Mbara ya aka ndiri hororio*
4. *Nguku ya mutumia niimenyaga gugikia no iroraga mukanye wa ya njamba*
5. *Aka matigagwo ndundu*
6. *Atumia moi kuhitha ndia no matiui kuhitha uhoro*

(e) Methali zinazohusu umilikaji mali

1. *Uhii ni umagwo no uka ndumagwo*
5. *Mundu muka ni mutuga kwene*
6. *Mundu muka na iguru matimenyagirwo*
7. *Aka na ng'ombe matiri ndugu*
8. *Iri gukura iriagwo iguku ni atumia.*
9. *Mureranirwo na ihii ni athararaga*
10. *Giathi githaragio ni gaka kamwe*

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY